

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

## **BUNGE LA TANZANIA**

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

#### **MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Tano - Tarehe 9 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### **D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

#### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

##### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 *(The Annual Report and Accounts of the National Board for Materials Management for the year ended 30<sup>th</sup> June, 2002).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Fedha wa Barabara kwa mwaka wa fedha wa 2001/2002 *(The Annual Report and Audited Accounts of Roads Fund Board for the financial year 2001/2002).*

#### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 60

##### **Chama cha Msalaba Mwekundu**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa Chama cha Msalaba Mwekundu kilianzishwa kwa Sheria Na. 71 ya mwaka 1962 kwa lengo la kuwahudumia majeruhi wa vita, kupambana na maafa wakati wa amani na shughuli za afya ya Jamii:-

- (a) Je, Chama hicho ni *NGO* au ni kitu gani na kinasimamiwa na Wizara gani?
- (b) Kwa kuwa Mheshimiwa Rais ndiye Mdhamini wa Chama hicho, je, taarifa za shughuli zake za kila mwaka hupelekwa wapi, kwani hazijawahi kuletwa Bungeni na kwa nini hakipewi ruzuku kwa ajili ya shughuli zake kutoka kwenye Wizara husika?
- (c) Je, kwa nini Makatibu wake wa Mikoa hawajalipwa mishahara yao kwa zaidi ya miaka takriban mitatu na ni kwa sababu zipi za msingi za uonevu huo unaofanywa kwa watumishi hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Chama cha Msalaba Mwekundu ni *NGO*, yaani Shirika lisilokuwa la Kiserikali. Kabla ya hapo kilikuwa Tawi la Chama cha Msalaba Mwekundu cha Uingereza (*The Tanganyika Branch of the British Red Cross Society - TRCS*), ambacho kilianzishwa mwaka 1949. Hapa Tanzania kilitambulika kama Chama cha Kitaifa na kukubaliwa katika Jumuiya ya Msalaba Mwekundu baada ya Serikali kutia sainsi Mkataba wa Geneva tarehe 12 Desemba, 1962. Hatimaye Bunge la Jamhuri ya Tanganyika wakati huo, lilipitisha Sheria Namba 71 ya mwaka 1962 ya Kusimamia Uendeshaji wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanganyika (*Tanganyika Red Cross Society*). Taasisi hii haisimamiwi na Wizara bali na Bodi ya Utendaji kwa mujibu wa sheria niliyoitaja

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamaisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, Mheshimiwa Rais ni Mlezi (*Patron*) wa *Tanzania Red Cross Society* siyo Mdhambi (*Trustee*). Uendeshaji na usimamizi wa shughuli za taasisi hiyo unafuata Sheria Na. 71 ya mwaka 1962. Aidha, taarifa za utekelezaji wa shughuli za chombo hiki huwasilishwa katika Bodi yake na kinapata misaada kwa ajili ya huduma inazotoa kutoka kwa wahisani mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *Tanzania Red Cross Society*, hakuna Makatibu wa Mikoa wa Chama hicho ambao hawajalipwa mishahara yao kwa zaidi ya miaka mitatu. Endapo Mheshimiwa Mbunge anayo majina ya Makatibu hao ambao wanadai hawajalipwa mishahara, ayawasilishe Serikalini yaweze kuwasilishwa kwa wahusika ili hatua zinazofaa zichukuliwe.

(d) Mwisho, kwa niaba ya Serikali, napenda sana kuipongeza *Tanzania Red Cross*, kwa kazi nzuri sana ambazo imekuwa inafanya kwa muda wote hapa nchini. (*Makofi*)

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kutokana na ile Sheria Na. 71 ya mwaka 1962, Shirika hili linatakiwa lifanye kazi kwa ushirikiano na Wizara ya Ulinzi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, pamoja na Wizara ya Afya. Je, kwa nini Wizara hizi hazitoi fedha ili kuwawezesha kufanya kazi zao kama inavyotakiwa na hiyo sheria?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**

Mheshimiwa Spika, kila inapotokea maafa au shughuli fulani ambayo inahitaji msaada wa *Red Cross*, Wizara inayohusika huomba msaada kutoka *Red Cross* na Serikali hutoa msaada wa kukamilisha kazi hiyo maalum. Tulipokuwa na mafuriko ya *El-Nino*, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilishirikiana na *Red Cross* katika kurudisha baadhi ya miundombinu na kuhudumia watu kadhaa waliopata maafa hayo. Serikali kupitia Wizara hiyo, ilitoa msaada wa kuwawezesha *Red Cross* kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, hakuna ruzuku maalum inayotolewa kwa *Red Cross* kwa ajili ya kuendesha shughuli zile kwa sababu moja ya miiko ya *Red Cross Society* inatakiwa iwe *independent, neutral* na isimezwe na chombo cha Serikali.

Kutoa ruzuku ya kudumu ni sehemu ya kumeza chombo hiki. Ikionekana kuna dalili zozote za Serikali kuingilia au kukimeza chombo hiki, Kamati ya *Red Cross* na *International Red Cross* inaweza kukifuta chombo hiki. Kwa hiyo, Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ulinzi, kila mara inapokuwa na shughuli ambayo inahusisha *Red Cross* huwa inatoa fedha kwa *Red Cross* kwa ajili ya kushughulikia jambo hili maalum. (*Makofi*)

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa na swali dogo tu. Kwa kuwa katika jibu la Waziri lilisema kwamba *Red Cross* ni *NGO*, tumekubaliana ni *NGO* ambayo inafanya kazi nzuri sana.

Kwa kuwa *NGO* na sheria tuliyoipitisha mwaka jana zilikuwa chini ya Makamu wa Rais, *NGOs* zote. Sasa *NGO* hii mbona inafanya kazi nzuri, iko *specific*, ambapo Sheria ya mwaka 1962 sio Sheria ya mwaka 2003 ya *NGO*; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anatazamaje? (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**  
Mheshimiwa Spika, bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge amebonyea hapa hana la kusema ameniomba niseme mwenyewe. Kwa sheria hii tuliyoitunga ya *NGOs*, *NGO* hii itaratibiwa na Ofisi hiyo hiyo ya Makamu wa Rais kwa sheria hii kama *NGOs* nyingine zote.

Na. 61

**Fidia ya Waathirika wa Matukio ya Januari 26 na 27, 2001**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imedhamiria kuendeleza Utawala Bora wa Haki za Binadamu kwa mujibu wa sheria; na kwa kuwa taswira ya muundo na hasa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora umejitokeza katika Ibara ya 130(1)(a) - (f) ya Katiba ya Nchi; na kwa kuwa Tume ya Kuchunguza Matukio ya Januari 26 na 27 iliundwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa chombo chochote kinachoundwa katika mamlaka ya Mheshimiwa Rais, huwa na nguvu za Kisheria kwa lengo la kupatiwa ufumbuzi, sambamba na mapendekezo aliyoyotoa Mwenyekiti wa Tume hiyo:-

(a) Je, kwa nini fidia za waathirika hao hazijalipwa hadi sasa na muda uliopangwa kwa ajili hiyo umeshapita?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kutowalipa wahusika fidia zao ni dosari kwa mujibu wa muafaka, hasa kwa jamii yenye kujenga matumaini kwa Serikali inayojitangaza kuendeleza Utawala Bora na Haki za Binadamu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADEO D. NTAGAZWA(k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a) na (b) na ningependa kwanza kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Novemba, 2003 kwenye Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge lako Tukufu, nilijibu swali Na. 3103 (Namba 3 katika *Hansard*) la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwayi, ambalo linafanana sana na swali hili. Nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania ni nchi inayoendeshwa kwa Utawala wa Sheria na kuheshimu Haki za Binadamu. Kwa kuzingatia haya, Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, ilianzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Majukumu ya Tume hii yameainishwa katika Ibara ya 130(1). Nchi yetu ni nchi ya kwanza kuanzisha chombo kama hiki katika Afrika. Kwa msingi huo huo yalipojitokeza matatizo ya matukio ya Januari 26 na 27, 2001 huko Zanzibar, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliunda Tume ya Kuchunguza Matukio haya kwa lengo la kusafisha hali ya hewa iliyokuwa imechafuka kisiasa. Tume hii ilipewa nguvu na mamlaka ya kuchunguza na kisha kutoa mapendekezo ili kukomesha kabisa matukio kama hayo yasijirudie tena siku za baadaye.

Mheshimiwa Spika, muafaka wa vyama viwili vya siasa, Chama cha Mapinduzi (CCM) na *Civic United Front (CUF)*, umekuwa ni mfano wa kuigwa dunia nzima. Nchi nyingi zimekuwa zikituita ili tuwafundishe ni jinsi gani tumeweza kufanikiwa katika kutatua mgogoro kama huu. Lakini, kikubwa ni kuwa muafaka umetuwezesha kudumisha sifa yetu ya amani na utulivu na kuendelea kuwa na mshikamano, maelewano, udugu, umoja na kuweka msingi imara wa kuimarisha umoja wa wananchi wetu. Nasisitiza tena kuwa hili ni jambo la kujivunia na hatuna budi kulilinda kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kutoa kifuta machozi na wala si fidia kwa raia wake waliopata athari katika matukio ya tarehe 26 na 27 Januari, 2000. Taratibu zinaendelea kufanyika ili kutekeleza maamuzi haya. Kwa sasa Serikali inafanya maandalizi ili kuikamilisha zoezi hili kama

ilivyopendekezwa katika muafaka na pia na Tume ya Hashim Mbita. Maandalizi hayo ni pamoja na kukamilisha kufunguliwa kwa Mfuko wa Suluhu na Maendeleo (*Fund for Reconciliation and Development*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo au ufafanuzi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali bado inakamilisha maandalizi ili kuwalipa kifuta machozi walioathirika au familia za walioathirika na matukio ya Januari 26 na 27, 2001. Maandalizi haya ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Suluhu na Maendeleo (*Fund for Reconciliation and Development*). Maandalizi hayo yapo kwenye hatua ya kuridhisha na mara yatakapokamilika, wahasika watajulishwa mara moja.

(b) Muafaka wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na *Civic United Front (CUF)*, umetekelezwa kwa karibu asilimia tisini. Serikali itawalipa waathirika wa matukio ya Januari, 2001 na haijabadili msimamo wake. Kwa sababu hii, suala la kutia dosari Muafaka halipo. (*Makofi*)

Na. 62

### **Taasisi za Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi**

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kupiga vita umaskini kwa kuzishirikisha taasisi mbalimbali kushiriki katika mapambano hayo; na kwa kuwa idadi kubwa ya wananchi ni maskini hasa wanawake kutokana na majukumu yao mengi yakiwemo yale ya kulea familia, kilimo, kufanya vibarua, biashara ndogondogo na uchuuzi usio na faida na kadhalika; na kwa kuwa taasisi nyingi ndani na nje zimeitikia wito wa Serikali wa kutoa msaada katika kumsaidia mwanamke ili aondokane na umaskini uliokithiri na aweze kutekeleza majukumu yake kwa unafuu kidogo:-

- (a) Je, ni taasisi ngapi zinatoa huduma za misaada ya kumwezesha mwanamke kiuchumi?
- (b) Je, ni wanawake wangapi wamebahatika kupata misaada hiyo na ni kiasi gani cha fedha kilichotolewa hadi Desemba, 2002?
- (c) Kati ya hao waliobahatika kupata misaada hiyo, je, ni wangapi wamefanikiwa kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini na miradi yao bado inaendelea?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mwangunga, Mbunge wa Viti Maalum, ningependa nitoe maelezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, wanawake wengi zaidi kuliko wanaume wanaathirika na umaskini kutokana na hali mbalimbali, kama vile kukosa elimu ya kutosha na ujuzi wa kutosha kuwawezesha kupata ajira au kuweza kujijiri, kukosa mikopo kwa ajili ya biashara ndogo ndogo, majukumu ya uzazi na kulea watoto, majukumu ya kazi za nyumbani kama vile kutafuta kuni, kuchota maji, kupika na kufanya usafi. Haya yamechangia wanawake wengi kuwa nyuma kimaendeleo. Serikali imetambua yote hayo na kuchukua jukumu la kuanzisha mifuko mbalimbali ukiwemo Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa nia ya kusaidia walengwa kwa kuwapatia mikopo nafuu ili waweze kuendelea shughuli mbalimbali zinazolenga kuondokana na umaskini, hususan wa kipato.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Si rahisi sana kufahamu taasisi zote zinazotoa huduma za misaada ya kumwezesha mwanamke kiuchumi. Kupata taarifa sahihi inabidi ifanyike savei au sensa. Zipo taasisi chache ambazo zinafahamika, kama vile Mradi wa Kutoa Mikopo Midogo Midogo (*Small Entrepreneurs Loan Facility - SELF Project*), unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Mradi huu hutoa mikopo kwenye asasi za kifedha ili nazo ziweze kutoa mikopo nafuu kwa walengwa ambao wengi wao ni wanawake. Mfano wa asasi ambazo zimeweza kupata fedha toka mfuko huu ni Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*) Mkoa wa Pwani, Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida na Morogoro. Taasisi zingine ni Mfuko wa Wanawake wa Kikristo, Shirikisho la Vikundi vya Uchumi Singida (*SHIVU*), Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, *PRIDE Tanzania*, *COSIGA*, *CAVI*, *AFREDA*, *SELFINA* na Vyama mbalimbali vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*).

(b) Kulingana na takwimu za kuanzia Julai, 2002 hadi Juni, 2003, jumla ya wanawake 4,441 waliweza kupata fedha kutoka kwenye asasi zilizopata fedha toka Mradi wa *SELF* ukilinganisha na wanaume ambao walikuwa 2,605. Jumla ya fedha walizokuwa wamepata wanawake ni shilingi milioni 484.3. Aidha, upo Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*Equal Opportunity Trust Fund - EOTF*), ambao toka mwaka 2000 hadi mwaka 2002 wanawake waliosaidiwa ni 885, kwa kupatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 268. Mfuko wa Rais (*Presidential Trust Fund - PTF*), kuanzia mwaka 2000 mpaka 2002 wanawake 19,495 walipatiwa mikopo iliyogharimu shilingi 3,218,845,000/=.

Mheshimiwa Spika, pia upo Mfuko wa *Foundation for International Community Assistance (FINCA)*. Asasi hii ambayo maoni yake ni kutoa huduma za kifedha katika familia maskini sana duniani ili ziweze kujitengenezea ajira zenyewe na kwa hiyo kuweza kuinua kipato cha kaya, inalenga kuwasaidia wanawake tu na hapa nchini ilianza rasmi Oktoba, 1998 huko Mwanza. Toka ilipoanza kufanya kazi hapa nchini mpaka kufikia Juni, 2003, imetoa mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 17 kwa wanawake 26,000.

Mheshimiwa Spika, Mfuko mwingine ni ule wa Maendeleo wa Wanawake (*Women Development Fund*). Ili kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, imeendelea kuratibu na kuimarisha mfumo wa kutoa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Wizara imeingia mkataba na Halmashauri za Wilaya kuhusu fedha za mikopo za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza Halmashauri kuchangia asilimia kumi ya mapato yao katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Halmashauri zilipewa shilingi 4,000,000 kila moja ikiwa ni mgao wa mwaka uliopita.

(c) Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kuwa wanaopata mikopo wanachangia ongezeko la ajira nchini, lakini kupima ni wangapi wamejikwamua kiuchumi ni suala gumu kwani wengi hupata vipato mbalimbali kutokana na shughuli kadhaa wanazozifanya. Aidha, ni jukumu letu sote kuwaelimisha wakopaji kufuata utaratibu ulio wazi wa kupata mikopo kutoka kwa vikundi au taasisi zinazojulikana Kisheria. Wakopaji na wakopeshaji ni sharti wazingatie utaratibu wa utoaji mikopo ambapo utaratibu wa namna ya kupata mikopo na urejeshwaji huwekwa bayana bila kuleta athari upande wowote. Uzoefu unaonyesha kuwa, wakopaji wanaofuata utaratibu wa ukopaji, ikiwa ni pamoja na mikataba husika, wanafaidika. Jambo muhimu kwa wakopaji ni kutimiza masharti ya kurudisha mikopo ili wengine waweze kukopeshwa.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, yenye kina, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, *NGOs* zote alizozitaja nyingi ziko mijini na ina maana kwamba, wanaonufaika ni wafanyabiashara wadogo wadogo, akinamama na vijana walioko mijini. Je, asasi hizi lini zitakwenda vijijini na Serikali inatamka nini kuhusu jambo hilo. Ahsante? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge, inaonyesha mikopo mingi inabaki mijini. Lakini kwa utaratibu hizi *NGOs* na asasi zingine ambazo zipo Mikoani pamoja na Wilayani ni jukumu la viongozi kusaidia Serikali kwa ujumla kuwaelekeza wanaohusika kuhusisha pia akinamama pamoja na wakopaji wengine ambao wanaishi vijijini. Lakini upo ukweli pia asasi kama ya *SIDO*, kwa vile

wanapewa fedha ili wawape wale wanaokopesha, tunao ushahidi pia kwamba na wenyewe wanakwenda vijijini. Lakini nakubaliana naye kwamba, mara nyingi wa vijijini ndio wanaoathirika. Hata hivyo, mikopo ya akinamama ikipelekwa kwenye Halmashauri mara nyingi utakuta wanakopeshana mijini. Kwa hiyo, natoa wito kwa wote wanaohusika, kuwahusisha wananchi waishio vijijini katika mikopo hiyo.

Na. 63

### **Uchafuzi wa Mazingira Unaosababishwa na Taka za Plastiki**

**MHE. ALI MACHANO MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia mazingira ina mpango wa kuweka hali ya mazingira kuwa safi; na kwa kuwa mpaka sasa kuna taka nyingi za plastiki katika maeneo mengi tunayoishi kama vile za mifuko tunayonunulia vitu, chupa zinazowekewa maji na vinginevyo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa taka hizo zinaangamizwa ili kuhifadhi mazingira yetu?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba kuzagaa kwa takataka hizo za plastiki katika miji yetu inaonekana kuwa tuna miji michafu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mbunge wa Tumbatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Ali Machano Mussa kuwa, kuna taka nyingi za plastiki katika maeneo mengi tunayoishi kama vile mifuko ya plastiki, chupa za plastiki na nyinginezo nyingi. Tatizo hili ni sugu na kero kubwa kwa Jamii na kwa mazingira hasa mijini. Utupaji ovyo wa mifuko na chupa za plastiki na uchomaji wa taka hizi katika sehemu nyingi za miji, husababisha uchafuzi wa mazingira na pia athari kwa mifugo na afya ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua kadhaa za kukabiliana na tatizo hili. Hatua hizo ni pamoja na:-

- Kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi bora ya bidhaa za plastiki na namna ya kukusanya taka za plastiki;
- Kuhamasisha viwanda vinavyozalisha bidhaa za plastiki vijihusishe zaidi na kurejeleza taka za aina hiyo (*re-cycling*);
- Kuweka kodi ya mauzo ya mifuko ya plastiki kwa kiwango cha asilimia 15 kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004 kwa lengo la kuhamasisha uingizaji wa mifuko mbadala na kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki; na
- Serikali kwa msaada wa Serikali ya Norway kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*), imejenga kituo cha kurejeleza taka katika Jiji la Dar es Salaam. Ujenzi umekamilika na kituo kimeanza kufanya kazi kwa majaribio. Taka za plastiki na karatasi huchambuliwa na kutengenezwa malighafi ya viwanda vingine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua ambazo Serikali imezichukua kukabiliana na tatizo hili, baadhi ya matokeo katika miji na jamii yenyewe ni kama vile:-

- Katika Jiji la Dar es Salaam viwanda vya *Simba Plastics*, *Cotex*, *Poly Sacks* na *Centac Plastics* vimeanza kurejeleza taka za plastiki;

- Taasisi na vikundi mbalimbali visivyo vya Kiserikali (*NGOs* na *CBOs*) katika Jiji la Dar es Salaam vimeanza kushiriki katika ukusanyaji wa taka za plastiki na nyinginezo katika maeneo ya jiji kwa lengo la kuzirejeleza;
- Taasisi na vikundi mbalimbali visivyo vya Kiserikali vinashiriki katika maonyesho ya bidhaa mbalimbali zilizotengenezwa kwa kutumia plastiki rejea, kama vile madawati ya shule, meza na mabomba ya kupitishia nyaya za umeme; na
- Kampuni binafsi ya *DISPOSITEK* kutoka Afrika ya Kusini kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, imewekewa katika teknolojia salama ya kuteketeza taka ngumu na za plastiki. Kampuni hiyo imekamilisha ujenzi wa tanuru la kuteketeza taka za hospitalini katika Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam. Mtambo unatarajiwa kuanza kazi ifikapo Juni, 2004.

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa kinababa ili mambo yote yapendeze tunatakiwa tuwe karibu na akinamama na tuwasaidie; na kwa kuwa kinamama wa vijijini wanatengeneza mikoba ya ukili na vikapu na wamekosa masoko ya kuuzia vifaa hivyo; je, Mheshimiwa Waziri haoni imekuwa wakati mzuri sasa kupiga marufuku mifuko ya plastiki ili kinamama waweze kupata sehemu ya kuuzia bidhaa zao? (*Makofi*)

Pili, kwa kuwa taka za plastiki pamoja na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri kuna sehemu ambazo zinatakiwa zihakikishe kwamba taka za plastiki zinaangamizwa na wanajaribu kufanya hivyo; na kwa kuwa Kisiwani Tumbatu kumejengwa tanuru la kuchomea taka za plastiki na sasa taka za plastiki Kisiwani Tumbatu hakuna; haoni kwamba kuna haja ya kuwapata wataalamu kutoka Wizara yake wakafika Kisiwani Tumbatu na wakaona tanuru ya kuchomea taka za plastiki iliyojengwa kwa gharama ndogo wakaweza kujenga katika vijiji vingine? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADEO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nikubaliane naye kwamba, tutakapofikia hatua ya kupiga marufuku taka za plastiki, vile vikapu wanavyosuka akinamama kwa kutumia ukili, vitapata soko kwa sababu soko la plastiki litakuwa limepotea.

Mheshimiwa Spika, pili ningependa nikubaliane naye kwa namna moja kwamba, ni vizuri kwenda kuona hilo tanuru lililojengwa katika eneo lake Kisiwani cha Tumbatu. Lakini napenda niongeze kwamba, kama ni biashara ya kuteketeza taka za plastiki kwa vyovyote vile lazima masuala ya unafikiaje kule yatiliwe maanani kwa sababu sijui kama haitaongeza gharama kutafuta taka kama iwe ni Zanzibar na nafahamu Mtaa wa Darajani kuna taka nyingi za plastiki na nyinginezo. Lakini sina hakika kama gharama ya kuzipeleka Tumbatu itawezesha misingi ya biashara kukidhiwa.

Na. 64

#### **Nyumba Wanamoishi Mawaziri/Manaibu na Maafisa**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (k.n.y. MHE. HAROUB SAID MASOUD)** aliuliza:-

Kwa kuwa nyumba nyingi walizokuwa wanaishi Waheshimiwa Mawaziri/Manaibu na Maafisa wengine hapa Dodoma zimeuzwa na kulazimu kutafutiwa nyumba nyingine za kupanga kwa ajili ya wahusika niliowataja:-

(a) Je, kuanzia Januari, 2003 hadi sasa ni Mawaziri na Manaibu wangapi wamepangiwa nyumba za watu binafsi?

(b) Je, Serikali inatoa shilingi ngapi kwa kila mwezi kwa nyumba hizo kwenye sehemu ya (a) ya swali hili?

(c) Je, ni Mawaziri na Manaibu Waziri wangapi wanaoishi kwenye nyumba zao wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi haina takwimu ya nyumba za Mashirika au watu binafsi zilizouzwa au kutouzwa ambazo walikuwa wanaishi Mawaziri na watumishi wengine hapa Dodoma. Hii ni kwa sababu Wizara haiwajibiki na nyumba hizo mfano *NIC*, hivyo hivyo makubaliano ya kupanga au kutopanga yalikuwa kati ya wahusika na Shirika au mtu mwenye nyumba na mhusika.

Aidha, kuanzia Januari, 2003 hadi sasa, hakuna Mawaziri na Manaibu Waziri waliopangishiwa nyumba za watu binafsi hapa Dodoma. Serikali haitoi fedha yoyote kugharimia kuwalipia Mawaziri na Manaibu Waziri katika nyumba za watu binafsi na kwa mantiki hiyo kila Wizara kupitia Bajeti yake inawajibika kumhudumia Waziri/Naibu Waziri wakati akiwa Bungeni. Wapo Mawaziri waliopangishwa nyumba za Serikali zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia kitengo cha Wakala wa Majengo (*TBA*). Kuanzia Januari, 2003 hadi sasa kiasi cha Sh. 9,700,000/= kimekusanywa toka kwenye nyumba zilizopangwa na Mawaziri, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu hapa Dodoma katika nyumba za Serikali.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa kuna baadhi ya Mawaziri na Manaibu Mawaziri wameshajijengea nyumba zao wenyewe na wale wengine wanaendelea kulipiwa na Serikali kama alivyozungumza mwenyewe, ambao wamejipangia katika nyumba hizo ambazo amezeleza. Je, ni gharama gani Serikali imewalipa hao viongozi waliojijengea nyumba zao wenyewe?

(b) Kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali na kwa kuwa viongozi kama hawa ni vizuri kuishi katika sehemu moja inayolingana na yenye ulinzi mzuri kutokana na uzito wa nafasi zao na majukumu yao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatengea sehemu yao nzuri ili kuonyesha utambulisho wa nafasi zao na kuachana na ile tabia ya kuwakodishia nyumba ambazo amezisema? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama jibu la msingi lilivyokuwa likieleza, Serikali haiwajibiki kuwalipia Mawaziri walio na nyumba zao binafsi kwa sababu huo ni uhuru wake wa kujenga nyumba yake kama ambavyo Mbunge anaweza akajenga nyumba yake au kama Mtanzania mwingine alivyo na haki ya kujenga nyumba yake. Kwa hiyo, Serikali huwa haiwalipii fedha au kulipa nyumba za Waheshimiwa Mawaziri waliojenga nyumba zao binafsi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Waziri kama alivyo Mtanzania mwingine ana haki ya kuishi mahali popote badala ya kuwekwa *group* moja la Mawaziri tu au sehemu moja ya Wabunge tu na sehemu nyingine ya Makatibu Wakuu tu, kwa sababu wote ni Watanzania. Waziri anaweza akaishi karibu na Mbunge, *messenger*, kwa sababu Mawaziri na wananchi wengine wa Tanzania wana haki ya kuishi mahali popote.

Lakini katika suala la kutafuta nyumba hapa Dodoma, Wizara ya Ujenzi kupitia Kitengo cha *TBA*, ina mpango wa kujenga nyumba 300 kwa ajili ya Makazi ya wafanyakazi mbalimbali wakiwemo Mawaziri, Makatibu Wakuu na kadhalika. Tunategemea kusaini mkataba huo katika kipindi cha mwezi huu au mwezi unaokuja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Jeshi la Magezea wanataka kuzijenga hizo nyumba. Ahsante sana. (*Makofi*)



**Mikopo ya Zana za Kilimo kwa Wakulima wa Mtwara**

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME** aliuliza: -

Kwa kuwa baada ya uhuru Wananchi wa Mikoa ya Kusini waliendelea kupambana na kupigania ukombozi wa nchi ya Msumbiji na kwa kuwa kwa muda wote wa mapambano hawakuweza kujishughulisha vyema na kazi za maendeleo ipasavyo.

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu mkubwa sasa wa kuwapatia Wananchi mikopo mbalimbali ikiwemo ya zana za kilimo kama vile trekta, pembejeo na pampu za kupulizia dawa kwenye mazao mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahmadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo: -

Kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali, kuwapongeza, kuwapa pole na kuwashukuru Wananchi wa Mikoa ya Kusini, ukiwemo Mkoa wa Mtwara kwa kuvumilia madhara yaliyotokana na mapambano ya kuikomboa nchi ya Msumbiji zaidi ya miaka ishirini iliyopita. Mapambano hayo yaliathiri kasi ya maendeleo ya Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia Wananchi wake mikopo ya pembejeo na zana za kilimo na katika kufanya hivyo, haitoi upendeleo maalum kwa Mkoa wowote kutokana na madhara ya kihistoria. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeanzisha Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Aidha, Serikali inahamasisha kuanzishwa kwa Mifuko ya Pembejeo ya Halmashauri za Wilaya. Mipango inaandaliwa ya kuanzisha Benki ya Kilimo na Ushirika. Benki nyingine nazo zimeanza kutoa mikopo katika Sekta ya Kilimo.

Kuanzia mwaka wa 1995 hadi Desemba, 2003, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo, ilikuwa imetoa mikopo yenye thamani ya Sh.914,825,000/= kwa Mikoa ya Kusini. Mikopo hiyo ilitolewa kwa ajili ya kununua pembejeo na zana za zao la korosho yakiwemo madawa, mbolea, mbegu na mabomba ya kupulizia dawa. Aidha, katika kuendeleza matumizi ya zana bora, mwaka 2002 Wizara ilipeleka matrekta madogo ya mkono 6 Mkoani Mtwara kwa ajili ya kuwakopesha wakulima kupitia Halmashauri za Wilaya zao. Matrekta hayo kwa sasa yamekwishakopesha kwa wakulima.

Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo umeanza kutoa mikopo kwa ajili ya kukarabati matrekta mabovu na kununua matrekta mapya. Katika Mkoa wa Mtwara, Mfuko umekwishaidhinisha mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 36.6 kwa ajili ya kukarabati matrekta 12 na Shilingi milioni 35 kwa ajili ya kununua trekta moja jipya. Katika Mkoa wa Ruvuma Shilingi milioni 113 zimetolewa kwa ajili ya kununua matrekta matano mapya pamoja na zana zake, ambayo yatatumika kuanzisha kituo cha kukodisha matrekta. Aidha, Shilingi milioni 32 zimetolewa kwa ajili ya kununua trekta moja jipya la mkulima.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa wakulima wa Mikoa ya Kusini wengi sana wanalima korosho na ndiyo tegemeo lao kubwa la uchumi na kwa kuwa tatizo lao kubwa linalowadumaza katika mambo ya uchumi ni bei ndogo ya korosho ambayo inapangwa na wanunuzi wa korosho. Je, Serikali sasa haioni ni vema ikainua uwezo wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima kwa kuwapa mikopo ili kuweza kununua mazao, hasa zao la korosho na mazao mengine ili kuleta ushindani wa bei?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza bei haipangwi na wanunuzi wa korosho. Tulikwishasema hapa Bungeni wiki iliyopita kwamba, upangaji wa bei ya dira inapangwa na wadau wa zao husika, wanunuzi pamoja na wakulima. Kwa hiyo, bei haipangwi na wanunuzi wa korosho.

Pili, kuhusu uimarishaji wa Vyama vya Ushirika, ndiyo kazi tunayoifanya sasa hivi ya kuhakikisha kwamba Vyama vya Msingi vinaimarishwa ili viweze kununua mazao ya wakulima.

**MHE. ABDILLAH O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la Mtwara kwa upande wa korosho ni bei na upatikanaji wa *sulphur*. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta njia ya kuweka angalau Kiwanda Kidogo cha Usagaji wa *Sulphur* Mtwara ili upatikanaji wa *sulphur* uwe rahisi Mtwara na Lindi? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Usijali Kiswahili chake. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, bei ya korosho ipo, lakini ni bei kwa nchi nzima na siyo maalum kwa ajili ya Mkoa huo. Kwa hiyo, kama tatizo ni upatikanaji wa *sulphur* na *sulphur* inapatikana kupitia mkondo wa mikopo ya Mfuko wa Pembejeo, sioni umuhimu sana wa kujenga kiwanda maalum huko Mtwara badala ya kutumia utaratibu wa sasa wa kutumia mkopo kununua hiyo *sulphur*.

Na. 66

Utumiaji wa Mbolea za Chumvi Chumvi

**MHE. SOPHIA M. SIMBA (k. n. y. MHE. AZIZA SLEYUM ALI)** aliuliza: -

Kwa kuwa kilimo cha sasa hutumia sana mbolea za aina mbalimbali zikiwemo zile za chumvi chumvi ambazo zinasaidia kurutubisha ardhi na kukuza mazao ya wakulima na kwa kuwa mbolea hizo hutumika kwenye Mikoa yote ya Tanzania: -

- (a) Je, Serikali imeshafanya utafiti wa mbolea hizo ili kuona zina madhara yoyote kwenye ardhi yetu?
- (b) Je, mbolea hizo zina madhara gani kwa binadamu wanaotumia mazao yaliyolimwa kwenye maeneo ambayo mbolea hizo zimetumika kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Vitu Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mbolea za chumvi chumvi zimetumika duniani kwa miaka mingi tangu Mapinduzi ya Kilimo ya Ulaya katika karne ya 12 na 13. Tabia za mbolea hizo katika udongo zinajulikana, kisichojulikana ni wingi wa virutubisho vilivyoko katika udongo wa eneo fulani. Wanasayansi ya udongo hufanya uchunguzi wa udongo huo kubaini kiasi cha virutubisho vilivyopo na kushauri juu ya kiasi cha mbolea kinachohitajika kuongezwa ili kukidhi mahitaji ya mazao yatakayootesha kwenye eneo linalohusika. Huu ndio utafiti unaofanywa na Vituo vyetu vya Utafiti vikiongozwa na Kituo cha Mlingano kilichoko Tanga. Utafiti umeonyesha kwamba, matumizi ya mbolea ya chumvi chumvi zenye madini ya *sulphur* kwa mfano, *Sulphate of Ammonia (SA)*, huongeza tindikali kwenye udongo na hivyo kufanya baadhi ya madini muhimu kuwa katika hali ambayo hayawezi kutumiwa na mmea.

Aidha, utafiti mwingine umeonyesha kwamba zipo mbolea za chumvi chumvi kwa mfano, *Urea* na *Calcium Ammonium Nitrate (CAN)*, ambazo hazina madhara yoyote kwenye ardhi kama zikitumiwa kwa kiwango na utaratibu unaoshauriwa.

(b) Hakuna ushahidi unaoonyesha kwamba, mbolea za chumvi chumvi zina madhara kwa binadamu wanaotumia mazao yanayolimwa kwenye maeneo ambapo mbolea zimetumika. Pamoja na kutokuwepo na ushahidi, wapo watu wanaopendelea kutumia mazao yanayotokana na kilimo hai kwa madaai kwamba mbolea za chumvi chumvi zina madhara. Mbolea zinapowekwa ardhini huyeyushwa na unyevu uliopo na kutoa virutubisho ambavyo vinahitajika kwa ustawi wa mimea. Virutubisho hivyo ni chanzo kikubwa cha madini yanayohitajiwa na binadamu.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Serikali ilitangaza kwamba mbolea itapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu na kwa kuwa katika maeneo mengi bei imekuwa kubwa na imekuwa ikipanda kwa visingizio vya gharama za uendeshaji na usafiri. Je, Serikali inasimamiaje kauli yake ya mwanzo kuwa mbolea itapatikana kwa bei nafuu vinginevyo Wananchi hawatatuelew?

(b) Je, mbolea ya marejea imeishia wapi, mbolea hii ilikuwa inasaidia sana?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mbolea ya bei rahisi na bei nafuu ilielekezwa kwenye Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini na imefanyika hivyo. Suala la kupanga bei iwe nafuu ilikabidhiwa Kamati za Mikoa hiyo. Kila Mkoa una Kamati ambayo ilianguka gharama halisi pamoja na ruzuku ya Serikali ya kusaidia usafirishaji wa mbolea hizo kutoka Dar es Salaam mpaka Mikoa hiyo minne iliyohusika na mbolea zote zimekuwa kati ya Sh.10,000/= na Sh.14,000/= na kama kuna nyongeza iliyotokea ni kutokana na usafirishaji, lakini haya yote yalikusika na Kamati zile za Mikoa husika.

Kuhusu mbolea ya marejea ipo, lakini washabiki wake ni wachache. Ruvuma bado ina mbolea hiyo ya marejea na inafaa. Lakini pamoja na hivyo imegundulika kuwa, baadhi ya mazao yanahitaji mbolea za kemikali kwa ajili ya kuongeza virutubisho na kuimarisha uzalishaji na tija.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika suala hili la mbolea Serikali ilisema kwamba kuweka ruzuku katika usafirishaji ilikuwa ni hatua za mwanzo tu. Je, Serikali ina mpango gani ambao inauchukua mwaka huu ili ruzuku hiyo ya mbolea iweze kuongezeka na ili wakulima waweze kununua mbolea hiyo kwa bei nafuu zaidi kuliko ya mwaka huu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ruzuku imekuwepo na tunategemea kwamba itakuwepo. Kitakachofanyika baada ya msimu huu kupita ni kwamba, tutakaa na ku-*review* kuona mafanikio na matatizo na ndipo hapo tutaweza kutoa jibu kamili kulingana na mazingira ya wakati huo. Kwa sasa ni mapema mno, tutekeleze kwanza hiki tulichonacho.

Na. 67

### Umeme Kutoka Nchi Jirani

**MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU** aliuliza: -

Kwa kuwa ipo baadhi ya Mikoa hapa nchini inapata umeme kutoka nchi jirani: -

(a) Je, ni nini faida au hasara tunayoipata kwa kutumia umeme unaotoka nchi jirani?

(b) Je, kutumia umeme kutoka nchi jirani kwa baadhi ya Mikoa yetu hapa nchini ni sababu ya ujirani mwema na mahusiano mazuri tuliyonayo kwa nchi hizo au Serikali imeshindwa kubuni mipango mizuri ya kuwafikishia Wananchi wake umeme kwenye Mikoa husika?

(c) Je, Tanzania inatumia fedha kiasi gani kulipa au kulipwa kwa nchi hizo kwa matumizi ya umeme huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hakuna hasara inayopatikana kutokana na kutumia umeme kutoka nchi jirani. Faida kubwa ni kuwa na vyanzo mbadala vya kupata umeme pasipo kutegemea vyanzo vya nchini ambapo mara nyingine vinashindwa kukidhi mahitaji yetu.

Faida nyingine ni kufanikisha baadhi ya Mikoa hapa nchini kupata umeme kutoka nchi jirani badala ya kutegemea vyanzo vya ndani kutokana na ugumu uliopo kiufundi na kifedha kuendeleza vyanzo hivyo kwa ajili ya kufikisha umeme kwenye Mikoa husika.

(b) Mheshimiwa Spika, kutumia umeme kutoka nchi jirani kwa baadhi ya Mikoa hakutokani na ujirani mwema na mahusiano mazuri tu, bali pia kunatokana na manufaa kwa nchi yetu kiuchumi na kifedha.

(c) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kinacholipwa na *TANESCO* kwa Makampuni ya Umeme ya nchi jirani kinategemea na makubaliano ya ununuzi wa umeme pamoja na matumizi ya umeme kwa Mikoa hiyo wakati kwa wakati. Kwa mfano, kwa wastani *TANESCO* inanunua umeme toka Kampuni ya Umeme Zambia (*ZESCO*) wenye thamani ya Dola za Kimarekani 131,000 kwa mwezi na Dola za Kimarekani 165,000 kwa mwezi kwa umeme toka Kampuni ya Umeme ya Nchini Uganda.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa watumiaji wa umeme kutoka nchi jirani wakati mwingine tunapata matatizo ambayo yanakuwa nje ya uwezo wa nchi yetu kuweza kuzuia, mfano umeme unaotoka Zambia kwenda Sumbawanga una matatizo ya kukatikakatika na matatizo haya yanatokana na chanzo chenyewe huko ambacho sisi watumiaji hatuwezi tukasema lolote. Je, Serikali/*TANESCO* inaweza kuwa na mpango gani wa kusaidia ili umeme unaopatikana kutoka nchi ile unapokatika ziwepo pia jenereta za kujaribu kusaidia kuleta umeme ili Wananchi wasiathirike na ukosefu wa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni kweli kwamba, kumekuwa na matatizo ya hapa na pale ya kukatikakatika kwa umeme unaotoka Zambia kuingia nchini Tanzania, Mjini Sumbawanga. Napenda nichukue nafasi hii kukiri kwamba, tumekuwa tukipokea malalamiko ya aina hii kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo hayo akiwemo Mheshimiwa Mwananzila.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua ya kuwasiliana na Shirika la Umeme Zambia kupitia *TANESCO*, lakini napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, matatizo haya kwa mujibu wa taarifa za kiufundi ambazo tumezipata kutoka Shirika letu la Umeme la *TANESCO* na baada ya majadiliano na wenzao wa Zambia, ni matatizo ya kiufundi ambayo hata hapa kwetu yanatokea na Mashirika yote ya Umeme yanajitahidi kuboresha mifumo yao ya umeme ili suala hili la kukatikakatika kwa umeme tuweze kuondokana nalo.

**Mafuta Yasiyo na Madini ya Risasi**

**MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. ADELASTELA E. MKILINDI)** aliuliza: -

Kwa kuwa hapa nchini vipo vituo viwili tu vya mafuta vinavyouza mafuta ya magari yasiyo na madini ya risasi na kwa kuwa inasemekana kwamba madini hayo husababisha madhara mengi kwa binadamu yakiwemo yale ya kupoteza kumbukumbu na kwa kuwa sasa tunashuhudia magari mengi yanayotumia mafuta hayo hapa nchini na kusababisha kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha uchafuzi wa hewa: -

- (a) Je, ni madhara gani mengine yanayoweza kumpata binadamu yanayotokana na uvutaji wa hewa iliyochofuliwa na moshi wa magari yatumiayo mafuta hayo na je, zipo dalili zinazoonekana?
- (b) Je, zipo tiba zinazoweza kuponya madhara hayo na ni muda gani madini hayo yanaweza kukaa mwilini?
- (c) Je, Serikali inawaambia nini wauzaji na wanunuzi wa vyakula kama mikate, samaki, maandazi na kadhalika kandokando ya barabara zitumiwazo na magari hayo hasa ikizingatiwa kwamba vyakula hivyo mara nyingi havitumiki vikaisha siku hiyo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Adelastela E. Mkilindi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Wataalam wa Mambo ya Afya, madhara yanayoweza kumpata binadamu kutokana na uvutaji wa hewa iliyochofuliwa na moshi wa magari yatumiayo mafuta ya petroli yenye risasi ni kama ifuatavyo: -

- (i) Kupata uharibifu kwenye mfuko wa mishipa ya fahamu na ubongo. Uharibifu huu hupelekea kichwa kuuma, kupata ugonjwa wa akili na hatimaye kifo kutokana na ubaribifu mkubwa wa ubongo;
- (ii) Kupunguza nguvu za uzazi kwa wanaume na wanawake na hivyo kuwafanya wawe tasa;
- (iii) Kuzaliwa kwa watoto wenye mtindio wa ubongo na upungufu wa damu; na
- (iv) Kuharibika kwa figo na moyo na kupelekea magonjwa ya moyo na figo.

Athari hizi zitajitokeza kama kiwango cha risasi mwilini ni *150mg* kwa kila gramu 100 za damu au risasi ikiwa ni zaidi ya *350mg* kwa kila gramu 100 za mkojo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Wataalam wa Afya, tiba kwa tatizo hili ni pamoja na: -

- (i) Kumwondoa mgonjwa kwenye mazingira ya hewa yenye risasi;
- (ii) Kumpa lishe nzuri;
- (iii) Kumpa maji ya *drip* yenye madini ya chumvi chumvi; na
- (iv) Kumpumzisha mgonjwa kitandani kwa muda mrefu (*Complete Bed Rest*).

Mheshimiwa Spika, wauzaji wa vyakula barabarani wanashauriwa kutouza vyakula barabarani kwani kuna uwezekano mkubwa wa wafanyabiashara wenyewe kuathirika na moshi wa petroli yenye risasi. Aidha, vyakula vyenyewe vinaweza kupata madini ya risasi toka kwenye moshi na magari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuhifadhi mazingira na pia kwa kuzingatia umuhimu wa kuepusha athari za kiafya kwa Wananchi wetu, Serikali tayari imekwishachukua hatua za awali zinazolenga kutumia petroli isiyotumia madini ya risasi (*Unleaded Gasoline*).

Kamati Maalum ya Kitaifa iliundwa mwaka 2002 yenye Wajumbe kutoka Wizara ya Nishati na Madini, TBS, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Makampuni ya Mafuta. Uundwaji wa Kamati hii ulifuatiwa na warsha Mjini Dar es Salaam kujadili mapendekezo mbalimbali na hususan umuhimu wa kuanza kuchukua hatua za kusitisha kwa awamu (*Phasing Out*) uagizaji wa mafuta yenye madini ya risasi. Aidha, Wizara yangu tayari imeyaagiza Makampuni ya Mafuta nchini kuanza kuacha kuagiza mafuta yenye madini ya risasi na tayari Kampuni ya BP imeshaanza kuingiza nchini mafuta yasiyokuwa na madini ya risasi tangu Juni, 2003 na hivi sasa kuna vituo 10 na si viwili, vinavyouza mafuta ya petroli isiyo na madini ya risasi, katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaandaa Muswada wa Sheria mpya ya Kusimamia Biashara ya Mafuta Nchini, ambayo itakuwa na kipengele cha kupiga marufuku uagizaji wa mafuta yenye madini ya risasi. Ni matarajio ya Serikali kwamba, endapo Bunge lako Tukufu litapitisha sheria hiyo, nchi yetu itaweza kuondokana kabisa na matumizi ya mafuta ya petroli yenye madini ya risasi katika kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kuwa suala zima la matumizi ya mafuta ya petroli yenye madini ya risasi ni zito kiafya, kimazingira na kiuchumi, napenda kuchukua nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kuwa, Serikali itachukua hatua kwa umakini mkubwa ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuelimisha umma na katika kuandaa programu ya utekelezaji. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna madhara kwa binadamu, je, Mheshimiwa Waziri anasema nini juu ya mbogamboga zinazolimwa pembeni mwa barabara kwa mfano barabara ya Kijitonyama?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimesema umuhimu wa kutokuendesha biashara karibu sana na magari ambayo yanatoa moshi huu wenye madini ya risasi. Hapa Bungeni tumeshawahi kutoa kauli kama hii wakati tunajibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo katika Bunge lililopita kwamba, ni vizuri hawa wanaofanya biashara hizi wawe nje ya maeneo hayo au kama mita 10 kutoka maeneo ambayo magari haya yanapita na kusambaza moshi huo. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa haya magari ambayo yanatoa moshi kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba yanaleta madhara kwa binadamu badala ya binadamu kuvuta *oxygen* wanavuta *carbon monoxide* ambayo ni hatari sana katika maisha ya binadamu. Je, ni kwa nini magari hayo yasiipigwe marufuku?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nadhani kimsingi magari yote kwa njia moja au nyingine yanatoa moshi. Tunachozungumzia hapa ni viwango vyenye athari kama ambavyo nimevieleza kwenye jibu la swali la msingi. Hapa nchini suala hili kwa kweli pia ni la kihistoria. Kama tunavyofahamu, tulikuwa na Kiwanda cha Kuzalisha Mafuta cha *TIPPER*, ambacho kwa kiwango kikubwa ndiyo kilikuwa kinazalisha mafuta ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, tumesema kwamba, Serikali inachukua hatua ya kuweza kulihimili jambo hili hatua kwa hatua na ni lazima tukumbuke kuwa, suala la magari na suala la mafuta ya aina hii si suala la kiafya tu, lakini pia ni suala la uchumi. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ichukue hatua kwa makini kabisa kama nilivyosema awali, kwa kushirikisha wadau wote hatua kwa hatua (*Phasing Out*). Tukumbuke kwamba kuna nchi nyingi duniani hata zilizoendelea kama Marekani bado hawajaweza kabisa kukamilisha utaratibu wao wa kuondoa mafuta yanayotumia madini ya risasi. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo inabidi lichukuliwe kwa umakini mkubwa sana.

Na. 69

### **Mpango wa AGOA**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza: -

Je, tangu mpango wa *African Growth Opportunity Act of the Government of the United States of America (AGOA)* uanzishwe hadi sasa Tanzania imefaidika kwa kiasi gani na kwa vipi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Programu ya *African Growth Opportunity Act (AGOA)*, ilipitishwa na Serikali ya Marekani na kuanza kutumika tarehe 1 Oktoba, 2000. Lengo kuu la sheria hii ni kuweka mazingira yatakayoziwezesha nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kuuza mazao na bidhaa zao katika soko la Marekani bila kulipia ushuru na bila viwango (*Duty Free and Quote Free*). Bidhaa zilizoruhusiwa ni pamoja na mazao mbalimbali ya kilimo na maliasili, ngozi na bidhaa za ngozi, sanaa za mikono na bidhaa za viwanda kama mavazi na nguo.

Tanzania tulikidhi masharti ya kuingia katika mpango huu wa *AGOA (Visa)* Februari, 2002. Mpaka sasa bado Tanzania haijafaidika sana na mpango huu. Kiwanda kimoja tu cha *Sun-Flag* cha Arusha kimepeleka nje nguo zenye thamani ya Dola za Kimarekani 540,000 mwaka 2002. Viwanda vingine viwili vilianzishwa navyo ni *NIDA Textile* kutoka Pakistan na *Star Apparel* kutoka Sri-Lanka. Viwanda hivi tayari vimeanza uzalishaji wa nguo na vinategemea kupeleka bidhaa America kabla ya mwezi Juni, 2004. Ajira iliyopatikana kwa viwanda hivi viwili inategemewa kufikia zaidi ya watu 2000. Serikali imeweka mkakati maalum utakaotuwezesha Tanzania kufaidika na *AGOA*. Hii ni pamoja na kuandaa miundombinu mizuri, kutenga maeneo, kutafuta wawekezaji wenye utaalam na masoko na kuwawezesha kifedha kuanzisha viwanda hivyo vya nguo. Kwa mkakati huu ulioanzishwa na Serikali, tayari zimejitokeza Kampuni 6 na maandalizi ya kuanzisha viwanda hivyo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kwa mara nyingine tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wahamasishe wafanyabiashara kote nchini watumie fursa hii ya mpango wa *AGOA* kwa manufaa ya nchi yetu kwa ujumla.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina swali dogo la nyongeza.

Kuna bidhaa ambazo zinahitajika labda kutekeleza vigezo fulani fulani na mazao ambayo yanahitajika pia kutekeleza au kutimiza vigezo fulani fulani. Je, hivyo vigezo ni vipi na kati ya hivyo vigezo ni vipi ambavyo vinatutia katika matatizo sisi kama Tanzania na sisi tunafanya nini kuhakikisha kwamba hivyo vigezo vinaondoka kuhakikisha kwamba tunafaidi huu mpango wa *AGOA* kikamilifu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, labda nikumbushe kwamba, kuna bidhaa 1,800 ambazo zimekidhi katika kuingia soko hili la *AGOA* na kila bidhaa ina vigezo kuhusiana na soko la America. Kwa mfano, kama ni nguo ni lazima zifikie viwango vya Kimataifa na kwa

sababu sasa hivi Tanzania imepata *visa* ya nguo, vigezo vinavyohitajika vinawekwa na yule mnunuzi. Kwa mfano, mnunuzi anataka *jeans* au *t-shirt* ya aina fulani, anasema ningependa iwe ya ubora kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, vigezo vingine ambavyo vimewashinda Watanzania wengi ni kuhusu vyakula. Vyakula mfano mananasi, korosho, karanga au asali inahitaji ipimwe ifikie viwango vya Kimataifa. Siwezi kueleza kwa urahisi kwamba kigezo cha asali kifikie hivi, bali ni hapo atakapojitokeza mwekezaji anayependa kuweka, hapo anaweza akasaidiwa kwa kutumia Wizara yetu, *Tanzania Chambers of Commerce* na Ubalozzi wa America. (*Makofi*)

Na. 70

### **Mafanikio ya EPZ**

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa na programu ya kuanzisha maeneo huru ya biashara (*EPZ*), je, programu hiyo imekuwa na mafanikio ya kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdalla, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa programu ya *EPZ* kwa Tanzania Bara umeanza rasmi Aprili, 2003. Kimsingi kipindi hiki ni kifupi kuweza kutoa picha halisi ya mafanikio yake. Hata hivyo, yamekuwepo mafanikio kadhaa ya kutia matumaini kuwa mpango huu utakuwa na mafanikio makubwa. Mpaka sasa, *NDC*, wakala wa Serikali wa kusimamia utekelezaji wa sheria ya *EZP* amekwisha toa leseni sita. Leseni tatu zimetolewa kwa makampuni ya kujenga miundombinu, ikiwa ni pamoja na *NIDA Textile Mill*, *Millenium Bunsiness Park* na *Mwananchi Gold Company*. Makampuni mengine matatu yamepewa leseni za uzalishaji ndani ya maeneo ya *EPZ* ambao ni hao hao *NIDA*, Kiwanda cha *Tri Star Apparel* na vile vile Kiwanda cha *Reclaimed Appliances* na uzalishaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutoa ajira na kujenga uwezo wa nchi kuweza kuuza nje, programu hii imekuwa pia kichocheo kwa wawekezaji kwa kipindi kifupi na kwa miradi inayoendelea ni kiasi cha US\$ 19.86 milioni kimeweza kuwekezwa chini ya programu ya *EPZ*. Mbali na mafanikio haya kuna matatizo ya msingi hasa kwa nchi inayoanza programu ya *EPZ*. Licha ya kuwa Serikali imekwishatenga maeneo kwa ajili ya *EPZ* karibu kila Mkoa, kuna tatizo la ukosefu wa miundombinu ya kuaminika kama barabara, maji umeme, simu na kadhalika, ambayo itakuwa ina unafuu wa kuwavutia wawekezaji wa *EPZ*.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na Wizara kuwa na programu nzuri ya mpango huu, je, kuna dalili zozote za kuungwa mkono na wafadhili?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kusema kweli wakati *EPZ* inaanza nchi yoyote ile ni lazima tunahitaji fedha za wafadhili, Serikali yenyewe na mikopo kutoka benki kubwa kubwa kama Benki ya Dunia. Wenzetu Kenya walichukua mkopo wa dola za Kimarekani milioni 75 kujenga miundombinu kwa ajili ya *EPZ*. Sisi tuna mpango huo vile vile kwa sababu tumeona kwa sasa hivi Serikali hatuna uwezo wa kujenga miundombinu katika kila eneo kama tulivyokubaliana. Tunategemea kuomba fedha za Serikali kuweza kuanza majengo ya Dar es Salaam halafu hapo baadaye na sisi tutaomba Benki ya Dunia kama ambavyo nchi zingine zinafanya. (*Makofi*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mpango wa *EPZ* nia yake ni kuliwezesha Taifa kuuza bidhaa nchi za nje. Uzoefu uliojengeka katika maeneo mengi ni kwa *EPZ* ni maeneo ambayo ni *exclusive* nje ya maeneo wanayoishi wananchi. *EPZ* zilizoanzishwa hapa Tanzania zimeanzia katika viwanda vilivyoko katikati ya miji na hii italet



udhibiti mgumu sana wa bidhaa zisirudi katika soko la ndani. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba kuna udhibiti wa bidhaa hizi zisije zikarudi katika soko la ndani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIAHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Ni kweli *EPZ* katika nchi za wenzetu zimetengwa katika maeneo yaliyo nje ya miji, lakini Tanzania kwa vile tunaanza hata kujenga hayo maeneo nje ya mji hatuna. Tumeona tuanze katika viwanda vilivyopo na sasa hivi tumetoa leseni tatu, moja kama unaifahamu vizuri iko Dar es Salaam kule Gongomboto, ambako kidogo ni nje ya Mji. Vile vile *Tanzania Revenue Authority* wanaweka ofisi yao kabisa na mdhibiti katika kiwanda kama si yeye anavyosema. Kiwanda kingine tumetoa pale Ubungo ambao ndiyo *Tri - Star Apparel* na sasa hivi *TRA* wako katika harakati za kuweka ofisi yao ndogo na wamefika hata kukubali pale Mwanzo kwa sababu ilikuwa bado haijajengwa kufikia standard ya *EPZ* na sasa hivi ukuta unaongezwa na kuweka vibanda ili kuhakikisha kwamba, hakuna hata mali inayoweza ikaingia nchini.

Ningependa niwahakikishie Wabunge wasiwe na wasiwasi, hakuna fedha ya Serikali itakayopotea kwa mpango wa *EPZ*. (*Makofi*)

Na. 71

#### **Uhaba wa Maji Mji Mdogo wa Mangaka**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mangaka ni Makao Makuu ya Jimbo la Nanyumbu ambayo ina Taasisi mbalimbali zikiwemo Shule, Mahakama, Kituo cha Polisi na kadhalika; na kwa kuwa mji huo mdogo unakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wakazi wake; na kwa kuwa hapajawa na mpango kamambe wa kuupatia maji huo maji yenye kukidhi mahitaji ya wakazi wake:-

- (a) Je, Serikali ina mpango wowote wa muda mfupi, kati na mrefu wa kuupatia maji huo mdogo maji ya kutosha?
- (b) Endapo mipango hiyo ipo, je itaanza lini kutekelezwa na itahusisha maeneo gani mengine?
- (c) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa ipo haja ya kuwa na mpango wa kuupatia maji hivi sasa mji huo mdogo kutokana na umuhimu wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Mji Mdogo wa Mangaka haupati huduma ya maji ya kuridhisha. Mji wa Mangaka una wakazi wanaokadiriwa kufikia 6,000. Vyanzo vya maji kwa mji huu ni visima vitatu. Kisima kimoja ndicho kimefungwa mashine inayotumia dizeli. Kiasi cha maji kinachopatikana kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Mangaka ni lita 37,868 kwa siku ikiwa ni asilimia 16 ya mahitaji ya wakazi hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi wangu huo, naomba kuendelea kujibu swali kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali imeanza utafiti katika maeneo ya Shule ya Sekondari ya Mangaka na Ndwika kwa lengo la kupata vyanzo vipya vya maji chini ya ardhi. Utafiti huu utafuatiwa na uchimbaji visima na ujenzi wa mradi wa kusambaza maji. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya inashirikiana na *TASAF*

katika kugharamia mradi huu. Makisio ya awali yanaonyesha kuwa mradi huu utagharimu kiasi ya Sh. 29.8. *TASAF* wanatarajia kuchangia Sh. 24.3 na wananchi watachangia Sh. 5,524,000.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa kuhudumia Mji wa Mangaka umekwishaanza kwa kufanya uchunguzi wa vyanzo vya maji. Pindi vyanzo vya maji vikipatikana, ujenzi wa mradi utaanza kwa lengo la kuhudumia maeneo yote ya Mji wa Mangaka.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ipo haja ya kuwa na mpango wa kuupatia maji hivi sasa Mji Mdogo wa Mangaka na mpango uliopo ni kama nilivyoeleza katika jibu langu la sehemu (b).

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo: Kwa kuwa Mji wa Mangaka umebahatika kupatiwa Mradi wa *TASAF* kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa mradi huo sasa umekwama kutokana na kupungukiwa mabomba:-

(a) Sasa je, ni lini Mradi huu utakamilika ili kuwaondolea wananchi wa Mangaka adha hii ya kukosa maji?

(b) Kwa kuwa tatizo la maji limeenea katika sehemu zote za Jimbo la Nanyumbu na kwa kuwa *TASAF* wameshafanya *survey* kwenye maeneo ya Namasoko, Maneme, Mpwahia, Maratani na Mpombe ya kujenga mabwawa, lakini tangu *survey* hii ifanyike muda mrefu umepita. Je, ni lini sasa *TASAF* watakamilisha ujenzi wa mabwawa katika maeneo hayo ili kuwaondolea wananchi wa maeneo hayo adha ya kukosa maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, tunafanya *survey* kwa ajili ya kuupatia maji Mji wa Mangaka kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira. Pili, napenda nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, miradi yote ya *TASAF* inashirikisha wananchi kwenye maeneo.

Kwa hiyo, ningemwomba sana Mheshimiwa Mbunge, aongeze bidii ambayo imeifanya *TASAF* kufika kwa ajili ya mradi niliousema. Kwa hiyo, wako tayari kuchimba malambo kama wameshafanya *survey*, nina hakika kwamba wananchi wakihamasishwa na maombi yao yakipelekwa *TASAF*, kuna uwezekano mkubwa wa *TASAF* kuchangia katika uchimbaji wa malambo hayo. Lakini juhudi za Mheshimiwa Mbunge, ziendelee na nina hakika wananchi wataitikia juhudi zake.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza kwamba, kwa kuwa suala hili la uhaba wa maji katika Mji Mdogo wa Mangaka, linaonekana kabisa kwamba linahusisha sehemu kubwa ya Wilaya ya Masasi. Sasa ningependa kumwuliza Waziri, kuna mkakati gani au mpango gani maalum wa kuhakikisha kwamba hasa katika Mji wa Masasi kunapatikana maji ya kutosha na pia katika sehemu nyingine zinazoambatana na sehemu hizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipongeze juhudi zinazofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji kwa wananchi, kwa ushirikiano mkubwa akiwemo Mheshimiwa Mbunge. Lakini chini ya mpango wa mradi wa Japan (*JICA*), kuna baadhi ya visima vitachimbwa kwenye Wilaya ya Masasi kupunguza matatizo ya maji.

Lakini napenda nisisitize kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, visima hivi tungeomba wananchi washirikishwe kikamilifu katika kuvitunza na kuvihudumia, la sivyoyote matatizo yaliyojitokeza huko nyuma yanaweza kurudia chini ya mradi uliofanyika miaka ya 1970 uliokuwa *financed* na *Finland*. (*Makofi*)

**Maji Vijiji vya Mkoa wa Mtwara**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkoa wa Mtwara una Wilaya tano ambazo ni Mtwara Mjini, Mtwara Vijijini, Tandahimba, Newala na Masasi; na kwa kuwa baadhi ya vijiji vyake wana matatizo makubwa ya ukosefu wa maji ingawa mabomba yapo lakini hayatoi maji na vijiji vingine havina kabisa mabomba tangu tupate uhuru na wananchi wake hawajui maji salama wala maji safi:-

- (a) Je, Serikali inakumbuka kuwa imetamka kuwa ifikapo mwaka 2000 watu wote na vijiji vyote vitapatiwa maji safi na salama?
- (b) Je, Serikali inafahamu kuwa mwaka 2000 umeshapita na kuwa tatizo la kukosekana maji wanaoteseka hasa ni wanawake na watoto ambao ni Taifa la kesho?
- (c) Je, ni Kata ngapi ambazo hazijapatiwa maji katika kila Wilaya na kwa sababu zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Tangu tupate uhuru Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali ya kuwapatia wananchi huduma ya maji karibu na makazi yao. Kwa mfano, mpango wa miaka 20 wa maji kwa wote (1971 - 1991) na mpango wa maji wa Kimataifa wa miaka 10 (1981 - 1991), kwa pamoja ilifanikisha kuwapatia maji safi na salama karibu asilimia 87 ya wakazi wote wa vijijini katika Mkoa wa Mtwara. Mpango huu ulitekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Finland na vijiji 436 kati ya 528 katika Mkoa wa Mtwara kwa wakati ule, vilipata huduma ya maji safi. Mafanikio haya hayakudumu sana kutokana na usimamizi hafifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi, naomba sasa nijibu swali kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa Serikali ilipanga kuwapatia wananchi wote huduma ya maji ifikapo mwaka 2002. Mpango huu ulitegemea vitu vitatu muhimu ambavyo ni upatikanaji wa vyanzo vya maji kwenye maeneo ya vijiji, fedha za kutosha kujengea miradi na ushirikishwaji wa wananchi katika utekelezaji wake. Kufanya hivyo kunahitaji uchambuzi kamilifu wa kitalaam na vifaa vya kuchimbua visima ambavyo huhitaji fedha nyingi. Serikali haikuweza kufikia lengo lililowekwa kutokana na Serikali kutopata fedha za kutosha za kutekelezea mpango huo.

(b) Ni kweli kwamba, mwaka 2002 umeshapita na bado huduma ya maji haijawafikia wananchi wote vijijini. Hata hivyo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji kwenye mkoa mbalimbali ikishirikiana na Halmashauri za Wilaya na wananchi. Kwa upande wa Mkoa wa Mtwara, Serikali imeandaa mradi wa maji utakaohusisha vijiji 31 vya Mkoa wa Mtwara kutumia msaada wa Serikali ya Japan. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu wa 2004. Serikali imekwisha ingia kwenye mkataba na kampuni itakayoleta vifaa vya kutekelezea mradi huo.

(c) Mheshimiwa Spika, Mkoani Mtwara, Kata ambazo hivi sasa hazipati huduma ya maji ni Chiwala, Mpindimbwi, Mkululu na Mkundi Wilayani Masasi, Mihambwe, Michenjele, Naputa, Maindo, Kitama, Mkoreha na Makulwe Wilayani Tandahimba na Chitekete na Malatu Wilayani Newala.

Napenda kuchukua nafasi hii kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, baadhi ya Vijiji katika Kata hizi vimo kwenye mradi nilioutaja hapo juu, utakaoanza mwishoni mwa mwaka huu. Serikali itaendelea kutafuta fedha za hapa na za nje kwa ajili ya miradi ya maji katika vijiji vilivyobaki.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupewa nafasi hii. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, yenye matumaini makubwa katika Mkoa wa Mtwara, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa swali la msingi ni tatizo la maji katika vijiji vya Mkoa wa Mtwara na kwa kuwa ahadi za kila mwaka zisizotekelezeka ni kero sana kwa wananchi. Je, kwa nini Serikali leo isitamke ahadi hizo ambazo zinaweza zikatekelezeka? (*Makofi*)

(b) Pamoja na kuwepo hali mbaya labda ya Bajeti na kwa kuwa Mkoa wa Mtwara una matatizo makubwa ya maji na kwamba wanaoteseka sana hasa ni wanawake na watoto. Je, kwa nini Serikali isitenge fedha za kukutekeleza mipango yake ili wanawake wa Mkoa wa Mtwara wapate maji kwa uhakika na shule zake kwa ujumla? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, miaka ya 1970 Mkoa wa Mtwara ulikuwa na miradi ya maji yenye *coverage* ya asilimia 87 nadhani, ni kiwango cha juu sana kuliko mikoa mingi hapa nchini. Sasa matatizo yaliyojitokeza ambayo tusingependa yarudie kwenye miradi tunayoipeleka sasa hivi ni kwa wananchi kutokushirikishwa kikamilifu katika kutunza na kulinda miradi hiyo.

Hivyo, miradi yote karibu mingi iliharibika na haifanyi kazi. Kwa hiyo, chini ya Mradi wa *JICA*, ambao tunataka tuone jitihada za wananchi kama wameelewa vizuri ushirikishwaji na viongozi wetu ambao ni wazuri kwenye Mkoa wa Mtwara ikishirikisha Wabunge, nina hakika kwamba, mradi huu utafanikiwa na hata hivyo, Serikali sasa hivi imeanza mazungumzo na Benki ya Dunia, ili tupate fedha za miradi ya vijijini katika Wilaya zote 105. Kwa hiyo, Mkoa wa Mtwara na Wilaya zake itakuwa ni mojawapo ya Wilaya zitakazohudumiwa. (*Makofi*)

Na. 73

### **Alama ya Fimbo Nyeupe**

**MHE. MARGARETH AGNESS MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa fimbo nyeupe (*White Cane*) ni alama ya Kimataifa inayotumika kuwezesha walemavu wasioona kutumia barabara kwa usalama zaidi ili wasidhurike na matumizi ovyo ya vyombo vya usafiiri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuelimisha jamii kuhusu alama hiyo ya fimbo nyeupe?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mkanga kwamba, fimbo au henzirani nyeupe (*White Cane*) ni nyenzo inayotumiwa na wasioona kuwaongoza na pia ni alama ya Kimataifa ya kuwatambulisha wasioona.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuelimisha jamii na hasa madreva wa magari ili wawe waangalifu zaidi katika matumizi ya barabara. Kutokana na kutambua umuhimu huo, Serikali ilishiriki kwa ukamilifu katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Henzirani Nyeupe yaliyofanyika Dar es Salaam tarehe 15 Oktoba, 2003. Ili kuendelea kuihamasisha jamii kuhusu utambulisho wa henzirani nyeupe, Serikali kupitia Wizara yangu na kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Henzerani Nyeupe tarehe 15 Oktoba kila mwaka kwa kauli mbiu zitakazoeleza umuhimu wa henzirani nyeupe kwa jamii.

**MHE. MARGARETH AGNESS MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini kwa ruhusa yako nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa vifaa hivi ni muhimu kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri na kwamba watu wenye ulemavu wasioona inawasaidia sana, je, Serikali ina mpango wa kutumia vyuo vyetu vya ufundi mathalani viweze kutengeneza vifaa hivi ili viweze kuuzwa kwa bei nafuu kwa sababu kwa gharama za kutoa nje fimbo nyeupe ni ghali; sasa je, Serikali ina mpango gani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, alipotoa ombi hili Mheshimiwa Margareth Mkanga kwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Waziri alitoa maagizo kwa *VETA* na *VETA* wamejaribu kutengeneza *sample* ya fimbo hiyo. Kwa hiyo, fimbo hii ni tofauti kwa bei na zile zinazoagizwa kutoka nje zina bei ya shilingi 30,000 mpaka 40,000, hii itakuwa na gharama ya shilingi 10,000 tu. Kwa hiyo, tumetekeleza ombi. (*Makofi*)

Na. 74

### **Kupeleka Polisi Vijiji vya Piyaya, Arash na Wasso**

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA (k.n.y. MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa operesheni dhidi ya uvamizi wa majangili wa Kisomali kwenye Wilaya ya Ngorongoro na Monduli kwenye miaka ya 1997 - 1998, wananchi walihamasishwa na kuhimizwa kujenga Vituo vya Polisi kwa ajili ya ulinzi wao na kwa kuwa wananchi wa Vijiji vya Piyaya, Arash na Wasso Wilayani Ngorongoro waliitikia wito huo wa Serikali na kujenga vituo hivyo ambavyo mpaka sasa havina Askari Polisi. Je, ni lini Serikali itawapeleka Askari Polisi kwenye Vituo vya Piyaya, Arash na Wasso, Wilayani Ngorongoro pamoja na vitendea kazi kama vile magari, *radio call* na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhiti, Viongozi wa Wilaya ya Ngorongoro, akiwemo Mbunge, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, kwa kuwahamasisha wananchi wa Wilaya hiyo kuanza kujenga Vituo vya Polisi. Pia nawapongeza wananchi wa Vijiji vya Piyaya, Arash na Wasso, kwa kuitikia wito wa kuanza kujenga Vituo vya Polisi kwa njia ya kujitolea.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawapeleka askari katika vituo hivyo kwa kuwa ujenzi wa vituo hivyo bado haujakamilika kwa maana ya kuwa na ofisi muhimu za vituo pamoja na nyumba angalau chache za kuishi Askari Polisi. Kijiji cha Piyaya kimeweza kukamilisha nyumba moja yenye uwezo wa kuishi familia mbili za askari lakini hakijajenga jengo la ofisi. Kijiji cha Arash nacho hakijajenga Kituo cha Polisi na jengo linalotumiwa sasa na Polisi ni la Ofisi ya Mtendaji wa Kata. Aidha, Kijiji cha Wasso kimeweza kujenga jengo la Ofisi, lakini hadi sasa hakuna nyumba hata moja za kuishi askari na uwezekano wa kupata nyumba ya kupanga haupo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali iko tayari wakati wowote kuwapeleka askari na vitendea kazi katika vijiji hivyo, tatizo lililopo ni lile la kutokamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo kwa maana ya kuweza kupeleka askari huko. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Viongozi wa Wilaya ya Ngorongoro, wasichoke na waendeele kuwahamasisha wananchi, ili kukamilisha kazi zilizobakia. Baada ya hapo Serikali inatoa ahadi kuwa itapeleka Askari Polisi na vitendea kazi katika vituo hivyo kwa kadri ya uwezo uliopo.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na pongezi nyingi sana kwa wananchi wa Piyaya, Arash na Wasso. Kwa kuwa wananchi hao wamejitahidi sana mpaka mnawapongeza kwa juhudi zao kubwa. Je, Serikali iko tayari sasa kuwasaidia ili waweze kukamilisha majengo hayo kwa vile nguvu zao sasa zimewaishia? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, pongezi nilizozitoa ni za dharti na kwamba si kweli kwamba wananchi wameshaishiwa nguvu kabisa kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema. Wananchi bado wanazo nguvu, tunachoomba waendeleo katika ujenzi. Kwa mfano katika Kijiji cha Wasso tayari Ofisi ya *IGP* ilishapeleka mabati 60 katika kuhamasisha waendeleo na ujenzi na katika vijiji vingine kwa kadri watakavyoendelea na juhudi zao na sisi Serikali, tutandelea kuwapa msaada. Kwa hiyo, nasema tena wasichoke na wala nguvu hazijaisha na sisi Serikali bado tuko nao mpaka vituo hivyo vikamilike. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umekwisha. Kabla hatujaendelea kuna matangazo ya Vikao vya Kamati vya leo. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa Mheshimiwa, Mgana I. Msindai, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane katika Chumba Na. 219, ghorofa ya pili, mara baada ya *agenda* ya uchaguzi kumalizika. Kamati ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Omar Kwaangw', anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo vile vile wakutane Chumba Na. 133 mara baada ya *agenda* ya uchaguzi kumalizika. *Agenda* ni kufikiria Maazimio ya kuridhia, ambayo yamepelekwa kwenye Kamati hiyo. Kamati ya tatu ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 7.00 katika ukumbi Na. 428 ghorofa ya nne. Mwisho wa matangazo ya Kamati.

Lakini maelezo kidogo kuhusu *agenda* ya leo ni kwamba, ile *agenda* namba 4 ya uchaguzi, nilikwishaeleza siku za nyuma kwamba, tungekuwa na uchaguzi katika maeneo mawili, Mjumbe wa kwenda *SADC* na Mjumbe wa kuingia kwenye Tume ya Huduma za Bunge. Sasa uchaguzi wa Mbunge atakayeingia kwenye Tume ya Huduma za Bunge, umeahirishwa kwa sababu imetokea pingamizi dhidi ya mgombea mmojawapo. Sasa pingamizi hilo lazima lifanyiwe kazi kwa sababu katika Kanuni zetu hatujaweka utaratibu wa jinsi ya kushughulikia mapingamizi. Hatukudhani kwamba lingeweza likatokea. Kwa hiyo, nimeitisha Kikao cha Kamati ya Uongozi, ili waweze kuzingatia pingamizi hilo na kulitolea uamuzi. Kwa hiyo, uchaguzi wa Tume ya Huduma za Bunge utafanyika siku nyingine itakayopangwa na *Returning Officer*.

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

### **Kauli ya Serikali Kuhusu Ajira ya Watendaji wa Vijiji na Kata**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Ajira ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, cheo na nafasi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji, imeainishwa chini ya kifungu cha 56(2) cha Sheria ya Serikali za Mitaa Na.7 ya mwaka 1982, inayohusu Mamlaka za Wilaya na kifungu cha 14(c) cha Sheria za Serikali za Mitaa Na.8 vile vile ya mwaka 1982, inayohusu Mamlaka za Miji. Kazi ya kwanza ya Afisa Mtendaji wa Kijiji ni kuwa Katibu wa Halmashauri ya Kijiji na Halmashauri ya Kijiji imetoa majukumu ya utekelezaji kwenye ngazi yake yanayolingana na yale yote ya Halmashauri ya Wilaya au Mji. Kutokana na matakwa haya ya sheria ni dhahiri kuwa Serikali ya Kijiji inapaswa kuwa na uongozi kwa upande wa utendaji wenye ajira ya uhakika na kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1982 zilipotungwa Sheria za Serikali za Mitaa Na.7 na Na.8, hakukuwepo na ajira rasmi za Maafisa Watendaji wa Vijiji kwani waliokuwepo wakati huo walikuwa vile vile ni Makatibu wa Chama kilichokuwa madarakani kwa ngazi za Vijiji. Kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria za Serikali za Mitaa kupitia Sheria Na.8 ya mwaka 1992, ajira za utendaji wao kwenye Vyama vya Siasa zilikoma na hatimaye kubaki kuwa watumishi wa Halmashauri.

Kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 1994 na 1995, Serikali iliagiza Halmashauri kuajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji na kuwalipa mishahara yao kwa kutumia utaratibu wa *local payroll*, kisha kuwapatia majukumu ya kusimamia maendeleo na uendeshaji wa Serikali za Vijiji badala ya kuwafanya wawe mawakala wa shughuli za Vijiji au wakusanyaji wa ushuri na kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1994 hadi 2002, Serikali ilibaini kasoro za kiutendaji zilizojitokeza. Kwa mfano, hakukuwepo na ajira kwa Maafisa Watendaji walio wengi zilizofanywa na Halmashauri. Pili, kwa wale walioajiriwa na Vijiji au Halmashauri hawakulipwa mishahara kwa kipindi kirefu. Tatu, kutokana na kutolipwa mishahara, baadhi yao walitafuta njia za kujipatia riziki zao kwa kufanya shughuli zao binafsi badala ya kusimamia shughuli za maendeleo katika Vijiji vyao na nne, pamoja na kasoro zote hizo hapo juu, waliendelea kufanya kazi za Afisa Mtendaji wa Kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kurekebisha kasoro hizo zilizojitokeza, Serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

- (i) Kutoa uamuzi wa kuwalipa mishahara Maafisa Watendaji wa Vijiji kwa njia ya ruzuku kwa Serikali za Mitaa;
- (ii) Kuanzisha cheo cha Afisa Mtendaji wa Mtaa ambacho hakikuwepo na kukipatia majukumu kama yale ya Afisa Mtendaji wa Kijiji; na
- (iii) Kuandaa miundo ya utumishi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka 2003/2004, nililiarifu Bunge lako Tukufu, uamuzi huu wa Serikali wa kuwaajiri Watendaji hawa wa Vijiji na jumla ya Sh.5,745,060,000/= zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara yao hiyo kuanzia tarehe mosi Januari, 2004. Tarehe mosi Desemba, 2003, Halmashauri zote nchini zilijulishwa juu ya uamuzi huo kwa barua Kumbukumbu Na.CAB58/337/01A/2 na pia kuelekezwa kwamba kulikuwa kumetolewa kibali cha ajira cha nafasi 9,803 na hivyo kila Halmashauri ilipewa idadi kamili ya Maafisa Watendaji wa Vijiji waliohitajika. Aidha, Serikali ilitoa maelekezo mengine kuhusu suala hili kama ifuatavyo:-

- (i) Ajira mpya itafanyika kwa waombaji wenye sifa ya chini ya kuingilia kazini ikiwa ni kuwa na elimu ya kidato cha nne au cha sita pamoja na kuwa na mafunzo juu ya masuala yanayohusu uongozi, utawala, jamii au sheria ya miaka miwili. (*Makofi*)
- (ii) Ajira yao itakuwa katika utumishi wa umma chini ya masharti ya kazi za Serikali za Mitaa; na
- (iii) Misingi ya kuajiri itafuata Sera ya *Management* ya ajira katika utumishi wa umma na ikiwa ya ushindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote nchini zimeteteleza agizo la Serikali kwa viwango tofauti. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imepokea taarifa kutoka Halmashauri mbalimbali zikielezea matatizo yaliyojitokeza kama ifuatavyo:-

- (i) Halmashauri zimesitisha ajira zilizokuwepo za Maafisa Watendaji wa Vijiji bila kuchukua taratibu za kuwalipa stahili za kuachishwa kazi;
- (ii) Halmashauri zimewaondoa kazini Maafisa Watendaji wa Vijiji na kusababisha Ofisi zao kukosa huduma zilizokuwa zinatolewa;
- (iii) Kushindwa kupatikana kwa waombaji walio na sifa zote kama zilivyotolewa na Ofisi ya Rais, *Management* ya Utumishi wa Umma. Mathalan, Halmashauri ya Wilaya ya Newala, imepata waombaji wawili tu wenye sifa kati ya nafasi 125 zilizopo na Halmashauri ya Wilaya ya Kondo haikupata mwombaji yeyote mwenye sifa kwa nafasi zote 117 na hali iko hivyo hivyo kwa karibu Halmashauri zote;
- (iv) Sifa za kuingilia kazini zimekuwa za kiwango cha juu sana kiasi kwamba upatikanaji wa watu wenye kuwa nazo umekuwa mdogo; na

- (v) Kuwepo kwa uwezekano wa kufungwa kwa Ofisi za Vijiji kutokana na kutokuwepo kwa watumishi wa Maafisa Watendaji wa Vijiji kwa kipindi kirefu kisichojulikana mwisho wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kubaini dosari hizo zote nilizozielezea hapo juu, imeamua kutoa ufafanuzi ufuatao kuhusu ajira ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Maafisa Watendaji wa Mitaa.

- (i) Maafisa Watendaji wa Vijiji waliokuwepo kazini kabla ya uamuzi wa Serikali wataendelea kuwepo kazini kwa kupatiwa mkataba wa miaka mitatu kuanzia sasa; *(Makofi)*
- (ii) Wakati wa kipindi cha mkataba wa miaka mitatu, Maafisa Watendaji wa Vijiji wasio na sifa watalazimika kujiendeleza ili waweze kuwa na sifa zinazotakiwa na muundo wa Utumishi wa Maafisa Watendaji wa Vijiji kama zilivyotolewa na Idara Kuu ya Utumishi; na *(Makofi)*
- (iii) Maafisa Watendaji wa Vijiji ambao watathibitika kuwa na makosa ya nidhamu kama vile ubadhirifu wa mali ya umma, utumiaji mbaya wa madaraka, wizi, ulevi na mengineyo yaliyotajwa kwenye sheria kuwa yanaweza kumwondoa mtumishi kazini, basi Watendaji hao watachukuliwa hatua za kufunguliwa mashtaka kwa mujibu wa kanuni ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zimeelekezwa ziendelee kujaza nafasi zilizo wazi katika Vijiji kwa kufuata utaratibu mpya. Nafasi wazi ni pamoja na zile zinazotokana na kifo, kustaafu, kuacha kazi au kufukuzwa kazi. Utaratibu huu ndio utakaozingatiwa pia katika kuajiri Watendaji wa Mitaa.

Zoezi la kuajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa litaendelea kufanyika kwa awamu kadri nafasi zitakavyokuwa zinatokea kuwa wazi. Kwa hiyo, linalosisitizwa hapa ni kwamba Watendaji wote wa Vijiji walioko kazini wataendelea na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, zoezi hili ni kubwa na muhimu kwa jamii yetu na kwamba linastahili kushughulikiwa kwa uangalifu mkubwa. Hivyo basi, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zote nchini, kushirikiana katika kukamilisha zoezi ipasavyo.

Serikali kwa upande wake itajitahidi kusimamia suala hili kwa nguvu ili kuwezesha shughuli za maendeleo Vijijini kuendelea bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

#### **UCHAGUZI WA WAJUMBE WA SADC PARLIAMENTARY FORUM**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokwisha wataarifu mapema, kuna wagombea wawili wa nafasi hii, nao ni Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Mheshimiwa Sophia Simba. Utaratibu ni ule uliouzoea, tunawaomba hao wawili watoke nje ya Ukumbi kwanza halafu wataitwa mmoja mmoja kujieleza. Kwa kuwa wanakwenda kwenye chombo kinachosema lugha ya Kiingereza, watajieleza kwa lugha hiyo ili tuweze kupima uwezo wao. *(Kicheko)*

*(Hapa Wajumbe Husika Walitoka Nje ya Ukumbi)*

**SPIKA:** Wabunge tuko tayari kuanza, *Sergeant at Arms* muingize Mheshimiwa. Wamepangwa na wanaitwa kwa mpangilio wa *alphabet*. Mwrite Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya, aingie ndani ya Ukumbi.

*Hapa (Mhe. Dr. Lucy Sawere Nkya) Aliingia Ukumbini*



**SPEAKER:** *Dr. Nkya, you have up to three minutes to introduce yourself to the voters and you may answer any questions not exceeding three that may be asked. You may now proceed.*

**HON. DR. LUCY SAWERE NKYA:** *Honourable Speaker, Right Honourable the Prime Minister, Honourable the Cabinet Ministers, Honourable Members of Parliament, my colleagues, good morning?*

**MEMBERS OF PARLIAMENT:** *Morning.*

**HON. DR. LUCY SAWERE NKYA:** *Stand in front of you, I am Dr. Lucy Nkya, my credentials have been presented to you through the Office of the Secretary of the Parliament. I am standing here to request for your mandate to send me to the SADC Parliamentary Forum, to represent Tanzania and the Southern African Region. I believe that I have the capability to do that work because I have the right education and I have a good exposure in the Southern African Region and also internationally.*

*My colleagues, I believe that I have a sense of patriotism to go there with only one message to stand for the interest of this Nation and also to stand for the common interest of the region and that is to foster good understanding, economic development and the matters deemed to bring a good understanding and co-operation in the Southern African Development Community.*

*Colleagues, give me the mandate and I promise you that, I am not going to let you down. Thank you for your votes and I believe that you have the faith in me and you are going to send me.*

*Honourable Speaker, Honourable Right Prime Minister of Tanzania, Honourable Members of the Cabinet, Honourable Members of the Parliament, my colleagues, I beg and I humbly beg for your votes. Thank you very much.*

**SPEAKER:** *Thank you. Any questions? Any questions? Third time, any questions?*

**MEMBERS OF PARLIAMENT:** *No.*

**SPEAKER:** *No questions. Dr. Lucy Nkya, you may resume your seat.*

*Sergeant-at-Arms, sasa muingize Mheshimiwa Sophia Simba.*

*Hapa (Mhe. Dr. Sophia M. Simba) Aliingia Ukumbini*

**SPEAKER:** *Honourable Sophia Simba, you have up to three minutes to ask for votes. Introduce yourself to the voters and you should be prepared to answer any question that may come from the floor. You may now start.*

**HON. SOPHIA M. SIMBA:** *Honourable Speaker, Honourable Prime Minister, Honourable Ministers and Deputy Ministers, Honourable Members of Parliament.*

*It is indeed an honor for me to be allowed to stand here in front of you to solicit for votes, votes that will enable me to fill the vacant posts in the SADC Parliamentary Forum.*

*Mr. Speaker Sir, I have been in this House for the last eight years. I acquire experience from you Mr. Speaker, from the Prime Minister and from my fellow Members of Parliament that coupled with my professional qualification and the exposure in International, Regional and Local Forums which I attend as a Member of this House.*

*I will, I am sure, be able to serve in the SADC Parliamentary Forum as is expected by you and my country. (Applause/Laughter)*

**SPEAKER:** *Order, Order, proceed Honourable Sophia.*

**HON. SOPHIA M. SIMBA:** *Mr. Speaker Sir, Your Right Honourable Prime Minister, Cabinet Ministers, fellow Members of Parliament and fellow Members of Parliament from the Opposition, we have been together for sometime now. You know me well as a friend and a colleague. I beg for your votes. Kindly cast your vote for Sophia Simba. God bless you all. (Applause/Laughter)*

**SPEAKER:** *Thank you. Any questions Honourable Members?*

**MEMBERS OF PARLIAMENT:** *No.*

**SPEAKER:** *Any questions?*

**MEMBERS OF PARLIAMENT:** *No.*

**SPEAKER:** *Honourable Sophia Simba, you may resume your seat. (Laughter)*

*Sergeant-at-Arms* piga kengele ili Wabunge walioko nje waweze kuingia Ukumbini.

*(Hapa kengele ilipigwa ili Wabunge waliokuwa nje waingie ndani ya Ukumbi)*

**SPIKA:** Karatasi zigawiwe.

Pili, Serikali isaidie kugharamia suala la *marketing* kwa bidhaa zinazoweza kuzalishwa hapa hapa nchini.

Tatu, vikwazo kwa bidhaa za nje zenye mwelekeo wa kuuja soko la bidhaa za ndani viwekwe ndani ya sheria.

Nne, Serikali iwasaidie wenye viwanda kuziba pengo la bidhaa zao linapojitokeza kwa sababu ya kijiografia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninawatakia utekelezaji mwema.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kuuleta Muswada huu katika kipindi hiki cha kusimamia uchumi wa soko kwa jamii yetu ya Watanzania. Naunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia maeneo mbalimbali ya Muswada huu, napenda kutoa ushauri ufuatao ambao ni muhimu kuzingatia ili usimamizi wake ulete maana halisi: -

Kwa kuwa sheria haijumuishi Zanzibar katika kulinda bidhaa kutoka nje, je, huu hauwezi kuwa mwanya wa kupitisha bidhaa huko na baadaye kuingizwa Tanzania Bara? Pia, ni utaratibu gani utatumika kuzuia hali hii isitokee? Je, isingekuwa vizuri kwa wakati huu kuwashauri wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nao wakaja na Muswada kama huu ili twende sambamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kwa upande wetu tujue Serikali ina mpango gani wa kuimarisha uzalishaji bora katika viwanda vyetu ili nasi tusijiingize katika biashara ya kuzuia tu, wakati na sisi viwanda vyetu havina chochote kile cha kutoa kwa Wananchi kama mbadala wa maamuzi haya?

Je, ni mikakati gani Serikali inaiandaa ili na sisi tujiingize katika mashindano katika ulimwengu huu wa utandawazi?

Nchi nyingi nyingi duniani huingia katika mikataba kama hii kama kweli nchi inafaidika kwa njia moja au nyingine. Hili ni suala ambalo lazima kuanzia sasa lisimamiwe vizuri kama sera ya biashara inavyoagiza.

Ni kwa msingi huo, ndiyo maana nashauri ijumuishe wateja wote (wadau) wakiwemo wafanyabiashara wadogo wadogo (*Informal Sector*) na siyo waja watendaji wa Wizara mbalimbali. Wakulima angalau wawakilishwe vizuri kupitia Chama chao cha *TTCIA*. Tupate Wajumbe wenye uwezo mkubwa na utalaamu wa kutosha kusimamia hili.

Mheshimiwa Spika, tungeshauri Wizara isikubali aina fulani za bidhaa kuingia kama hazina, ubora wa aina tunayoitaka. Kazi hii ni budi sasa isimamiwe vizuri na *TBS* na tuendelee kukataa nguo za aibu na hasa za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa kila hali.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa naiunga mkono hoja hii na imekuja wakati muafaka. Pamoja na hayo napenda kuchangia machache yafuatayo: -

Kuna umuhimu wa viwanda vyetu kukazana sana katika suala la ubora wa bidhaa (*quality*) ili ziweze kuwa bora na/au kulingana na bidhaa za nje. Hii itasaidia kuhimiza watu wetu kutumia bidhaa za nyumbani yaani chetu ni bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la wingi wa bidhaa (*quantity*) zenyewe ili kutosheleza soko la ndani na hata kuuza nchi za nje. Suala la *economics of scale*, ili tuzalishe kwa wingi, bidhaa ziwe rahisi au nafuu na ili kuwe na ushindani mzuri (*Level Playing Field*). Kwa maana nyingine viwanda vyetu viungane na vingine katika *African Regional Blocks* kama *SADC, PTA, COMESA, EAC* na kadhalika. Hii itasaidia sana kuwa na viwanda fulani fulani kwa maeneo husika ili uzalishaji uwe kwa wingi na ili tutumie raslimali zetu vizuri (*Comparative Advantage*) kwa kila bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema tena naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nashukuru kwa kupata furasa hii ili nitoe mchango wangu katika Muswada huu wa *Anti-Dumping*.

Pili, nilikuwa nina mambo mengi sana ya kuchangia, lakini semina ya jana imepunguza maneno yangu sana. Kimsingi naikubali hoja hii na ninaiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naikubali Muswada huu kwa faida za kinchi zifuatazo: -

- (i) Tanzania kuhami uchumi wake dhidi ya ushindani usio halali toka nje. Hilo kiuchumi ni sawa;
- (ii) Kupata fursa nzuri ya kulinda viwanda vyetu dhidi ya ushindani wa nje usio halali.
- (iii) Kuvutia wawekezaji wengi zaidi; na
- (iv) Sheria hii itawaondolea shaka na wasiwasi wanaotaka kuingiza sayansi na teknolojia mpya kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ni nzuri sana, lakini katika kipindi cha mpito, Wananchi hasa maskini watakumbana na shida, matatizo na kero zifuatazo: -

(i) Vitu au bidhaa za bei nafuu zilizozeleka zitapungua sana katika soko mfano khanga za Sh.1,000/= hadi Sh.1,500/= zitapotea kabisa zitabaki za Sh.2,500/= hadi Sh.3,000/=. Kwa maskini kwake hiyo ni athari, viberiti bei itabadilika, ni athari kwa walaji wadogo, sukari bei itabadilika, ni athari kwa walaji wadogo, mafuta kadhaa bei itabadilika na itakuwa ni athari kwa walaji wadogo, zana za kilimo na pembejeo zake zitaadimika, mitumba (kuna shati la Sh.500/= hadi Sh.1,000/= ) (Kuna viatu vya Sh.500/= maskini ndio kimbilio lao). Asilimia 56 ambao ni maskini watalindwaje?

(ii) Gharama mbalimbali kwa mwananchi zitapanda mfano kama ifuatavyo: Gharama za elimu (kusomesha) mashuleni, gharama za usafiri na usafirishaji, vifaa au vyombo vya nyumbani, maziwa ya kopo na paketi, magari, baiskeli, vipuli vya viwanda, vifaa vya ujenzi na kadhalika.

Katika kipindi hiki cha mpito, Wananchi watalindwaje sambamba na kulinda uchumi wa nchi?

(iii) Vitu vifuatavyo ni muhimu katika maisha ya Wananchi wanyonge, Serikali ichangie ruzuku: Zana za kilimo kwa Wananchi, pembejeo za kilimo kwa Wananchi, baiskeli hutumiwa na maskini, redio ni za maskini, magazeti maskini wanunue Sh.100/= badala ya Sh.200/=.

Serikali ichukue hatua madhubuti katika kipindi hiki cha mpito kisiwaathiri sana walaji wadogo walindwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Kwanza, napenda kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha Muswada wa *Anti-Dumping* katika Bunge hili Tukufu. Muswada huu umekuja kwa wakati wake. Suala muhimu katika Muswada huu ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo ushindani wa haki katika soko la ndani na kuweka utaratibu utakaohakikisha kwamba haki hiyo inakuwepo. Tunao wajibu wa kulinda viwanda vyetu na soko letu dhidi ya ushindani kutoka nje. Kazi hiyo itakuwa rahisi iwapo viwanda vyetu vitazalisha kwa ufanisi wa hali ya juu unaolingana au kuzidi ule wa wazalishaji wengine duniani.

Katika kulinda viwanda na soko letu, tunaposema kuwa waangalifu ili tuisababishwe madhara makubwa zaidi katika uchumi na kwa walaji kama dalili kwamba viwanda vinavyolindwa dhidi ya ushindani kutoka nje, vinapandisha hii kiholela ili kujinufaisha na kwa kufanya hivyo huwaumiza walaji na watumiaji wa bidhaa wanazotengeneza. Kwa mfano, kiwanda cha Sukari cha Kilombero kinataka kutengeneza *industrial sugar* lakini bei yake itakuwa juu sana kiasi kwamba itaathiri viwanda vitakavyotumia sukari hiyo na hatimaye walaji.

Sheria hii ni nzuri lakini hajjaeleweka vizuri na inabidi wananchi watambue kuwepo kwa sheria na vyombo vingine vinavyolinda walaji na soko letu dhidi ya bidhaa zinazotoka nje.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia hoja hii naomba kulitakia Bunge lako Tukufu kheri za mwaka mpya na mafanikio na ufanisi tele kwa mwaka huu wa 2004.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara na Watendaji wake wa Wizara na bila ya kuisahau Kamati ya Bunge ya Uwekezaji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa kuleta na baada ya Kamati kuujadili Muswada huu Bungeni.

Muswada huu ulipaswa ufikishwe Bungeni mapema zaidi na hasa ungekuwa unawasilishwa mara moja baada ya uamuzi wa Serikali kuamua kubinafsisha mashirika ya umma. Nasema hili kwa sababu awamu ya kwanza chini ya Rais, Hayati Baba wa Taifa, sekta hii ya viwanda ilikuwa tayari imewekwa miundo mbinu muafaka, sekta ya viwanda vya nguo, mafuta ya kula, sukari, vyote hivi vilikuwa vimeandaliwa, hivyo basi ilikuwa ni wakati muafaka kuvilinda vile viwanda ambavyo viliuzwa au kuwekezwa na watu wa nje na ndani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuletwa Muswada huu hivi sasa utatumika kikamilifu utasaidia sana kulinda viwanda vyetu nchini.

Mheshimiwa Spika, nimepitia Muswada huu sehemu zake zote 13 naafiki muundo wa Kamati utakaoundwa kwenye kutekeleza Sheria, pia Muswada huu utakapopitishwa na Bunge lako Tukufu. Lakini kwa sababu sekta hii kabla ya ubinafsishaji ilikuwa kwenye hali duni, nashauri yafuatayo:-

(i) Ili kuwezesha Kamati ifanye kazi kwa unadhifu, Serikali iandae orodha ya viwanda ambavyo kweli vimefikia uzalishaji wa bidhaa zao kwenye viwanda vya Kimataifa kwa unadhifu wa

bidhaa na bei halisi kwenye soko huru. *Performing industrial supplies should be protected, non performance should be listed and encourage them to perform.* Tusilinde viwanda ili mradi tu ni kiwanda cha ndani, hapana. Nguvu zote za hali na mali za Serikali zilengwe kwenye viwanda vinavyofanya kazi vizuri kwanza; na

(ii) Serikali iandae mikakati ya kuviwezesha viwanda vya ndani kuboreka kiteknolojia na ufanisi wa utendaji kabla ya kuvihusisha na kulindwa na mafanikio ya upitishaji wa Muswada huu kuwa Sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu japo kwa maandishi. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu wake na Wataalam wa Wizara hii, kwa kuweza na kutenda kwa manufaa ya Watanzania wote na vizazi vijavyo.

Kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu kwa kumwezesha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kuipatia Tanzania Uhuru na hatimaye akatuanzishia viwanda vingi sana hapa nchini kwa manufaa ya Watanzania wote ili kuepusha kuagiza kila kitu nchi za nje. Kwa mchango wake huo, hatuna budi kumkumbuka na kumuenzi. Ninawaalani wale wote waliokabidhiwa viwanda hivyo wakavifilisi na kusababisha Watanzania kufikia hatua ya kuvaa magome ya miti kwa ukosefu wa nguo japo viwanda vya nguo vilikuwepo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, kwa busara zake kwa kutoa ruksa kuingiza bidhaa nchini kwa mfumo wa soko huria. Hapo ndipo Watanzania walivaa nguo kwa bei nafuu na foleni kwenye viwanda vya nguo ikaisha kabisa. Nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, kwa kutupa mwanaye Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, aliyemsomesha kwa dhiki kubwa naye akamtii kusoma na sasa ni Naibu Waziri wa Afya, mwenye kujua wajibu wake vizuri sana kwa manufaa ya Watanzania wote *like father - like son.*

Mheshimiwa Spika, baada ya mataifa ya nchi za nje kupiga darubini Tanzania ya kuona kuwa tuna mahitajio ya karibu kila kitu na viwanda vimekufa kwa uzembe wa waliokabidhiwa ndipo wakatumia ruksa ile kuleta kila aina ya bidhaa kwa bei rahisi na kudhoofisha kabisa biashara ya viwanda vya Tanzania alivyovifufua Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa njia ya ubinafsishaji. Sasa bidhaa zake zinaonekana siyo bora, bei kubwa na haziuziki ndani ya nchi wala nje ya nchi kiurahisi na kushiria viwanda hivi kufungwa kwa mara nyingine tena.

Nchi yetu ni shujaa kwa somo la usalama. Kwa kutumia utaalim wake wa upelelezi, upekuzi, upembuzi na utambuzi, hakika tunaweza kuhakikisha kuwa nchi yetu ya Tanzania siyo dampo la bidha za nje kuharibu mfumo wa viwanda na biashara zetu kwa viwanda vichache tulivyo navyo. Ni kwa kupitisha Muswada huu, ndipo tutapona kuwa dampo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Februari, 2004 tutatumia sheria hii ya *Anti-Dumping and Countervailing Measures Act, 2003* na kuziba mianya yote ya nchi za nje kufanya nchi yetu kuwa dampo kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa virusi vyote kwenye viwanda vyote kwa njia ya kuwapunguza kazi na kuacha Menejimenti Chapakazi na Watanzania Chapakazi;

(ii) *TBS* itembelee viwanda vyote mara kwa mara na kuvishauri viwango stahili kwa ushindani nchini na nchi za nje rushwa iachwe; na

(iii) Viwanda vitoavyo mahitaji ya Watanzania vianzishwe Wilayani kote hata kama ni vidogo kiasi gani ili mradi vinazalisha mahitajio. Viwanda hivyo ni kama kiwanda cha vyerehani na vipuri vyake, sindano za vyerehani na za kushona kwa mkono, vifungo vya nguo, zipu, bakozi, chanuo, nguo za ndani, chupi na sidiria, viatu, soksi, mikasi, nyembe, mikanda, tai, *clips*, suruali, mashati, makoti (*jackets*)

na suti, mavazi ya akina mama na watoto, mafuta ya kujipaka na vipodozi, masanduku na *brief case*, pipi, tofi na biskuti, zana za kilimo, matrekta, majembe, reki, mapanga, visu na plau, saa na mita mbalimbali, vifaa vya ofisini kama wino, kalamu, vifutio, kausho, rula, mashine za kunyolea ndevu na nywele, kucha, *toilet papers* na vifuko mbalimbali, vipuri vya magari, pikipiki, matrekta na vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, Waziri na Wataalam wa Wizara hii waende nchi za nje kushawishi na kuchukua mtaalam mmoja hadi viwanda nilivyovitaja kwenye *paragraph (3)* kukamilika japo nusu yake kabla ya Novemba, 2005. Wawekezaji hawa wapewe maeneo yaliyo wazi (*industrial areas*) kama za Himo Mkoani Kilimanjaro na Wilaya zenye miundo mbinu iliyokamilika. Wataalam wa Kitanzania waitwe kujenga viwanda wanavyovijua. Urasimu wowote ule uachwe kwanza ili tupate kwanza ndipo urasimu ufuatae.

Mwisho, ubunifu, motisha, usimamizi, uzalendo na uongozi bora ndiyo siri ya kuwa na viwanda vingi vilivyo bora na kuua kabisa biashara ya mazao ya viwanda vya nchi za nje na kuepusha nchi yetu kuwa jalala au dampo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka mjadala ulimalizika Ijumaa jioni, leo ni zamu ya Mtoa Hoja kuhitimisha hoja yake. Sasa namwita Waziri wa Viwanda na Biashara. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kuungana na wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, waliochaguliwa na Bunge hili kuingia katika Bunge la Afrika. Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuingia katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia Muswada huu kwa kauli na maandishi. Kwanza kabisa, naishukuru Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa mchango wao mkubwa tangu wakati wa Semina kwa Kamati wakati wa Kikao cha Wadau yaani *Public Hearing* na wakati wa kuipitia Muswada huu. Aidha, nakushukuru wewe binafsi, kwa kukubali kufanyika Semina kwa Waheshimiwa Wabunge. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kukubali kutufungulia Semina kuhusu Muswada huu. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote, walio meta fursa ya kuhudhuria Semina inayohusu Muswada huu na sasa nina hakika kuwa dhana ya *Anti Dumping* inaeleweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, waliochangia Muswada huu kwa kauli ni wafuatao: Kwanza ni Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, Mheshimiwa Semindu Kisange Pawa, Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wafuatao walichangia kwa maandishi: Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, Mheshimiwa Frank Michael Mussati, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mheshimiwa Major Jesse Jeremiah Makundi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Khalid Suru na Mheshimiwa Charles Keenja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kuwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kauli na kwa maandishi, wameunga mkono hoja hii. Hii ni pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Nyote nawashukuru sana. Napenda pia kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Maafisa wake, kwa kazi nzuri ya kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rita Mlaki, Mbunge wa Kawe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa msaada na ushirikiano katika kuendesha Wizara yetu. Vile vile napenda kumpongeza na kuwashukuru watumishi wenzangu wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Ahmed Ngemera, kwa kazi nzuri ya kunisaidia kuendesha Wizara na

kuandaa maelezo kuhusu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu hoja yangu ya Muswada wa Sheria ya *Anti Dumping*.

Mheshimiwa Spika, michango mingi iliyotolewa hapa Bungeni ilikuwa ni ushauri hasa kuhusiana na utekelezaji wa Sheria ya *Anti Dumping* pindi itakapopitishwa na Bunge lako Tukufu. Naahidi kuzingatia ushauri huu pindi Muswada huu utakapokuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nipitie hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza hoja zilizotolewa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara, suala la muundo wa Kamati. Wajumbe wawili zaidi kutoka sekta binafsi waongezwe kwenye Kamati na mmoja wao awe mwanamke. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Mbatia, kwa niaba ya Kamati na Serikali, imeafiki pendekezo hili na marekebisho ya Muswada yametolewa kuwezesha kutekeleza pendekezo hili. (*Makofi*)

Kamati ipewe uwezo wa kupata taarifa. Hili nalo lilitolewa na Kamati chini ya kifungu cha 75 cha Muswada huu. Kamati imepewa uwezo mkubwa pamoja na suala hili, pia chini ya makubaliano ya *WTO*, Kamati imepewa uwezo wa kupata taarifa hizo kutoka nchi wanachama wa *WTO*. Kazi za Kamati Ndogo ziainishwe kama ilivyo kazi za Kamati za Ushauri. Serikali inakubali hoja hii. Kazi hizo zitaainishwa katika Kanuni zitakazotungwa na Waziri kwa mujibu wa Kifungu cha 77 cha Muswada. Muda wa uchunguzi wa miezi 12 hadi miezi 18 ni mrefu na unaweza kusababisha uthari zaidi kwenye bidhaa na uzalishaji kwenye viwanda kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, muda huu ni wa juu kabisa lakini uchunguzi unaweza ukakamilika katika muda mfupi zaidi. Aidha, kifungu cha 31 cha Muswada huu kinatoa mwanya wa kuiwezesha Kamati kuchukua hatua kutegemea hali halisi ya uchunguzi inavyojitokeza. Pili kifungu cha 46 kinampa Waziri uwezo wa kuchukua hatua za dharura za kushughulikia tatizo wakati uchunguzi unaendelea. Kwa maana hiyo, jambo hili limekamilika.

Kuhamasisha na kuwaelimisha wadau mbalimbali kuhusu sheria inayotungwa ili iweze kutekelezeka bila kupoteza shabaha yake. Hii ni hoja ya msingi na Serikali inafiki na hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na Semina ya Waheshimiwa Wabunge iliyofanyika tarehe 5 Februari, 2004. Serikali itaendelea juhudi hizi ili kuwafikia wadau wote.

Bidhaa za Tanzania kushindwa kushindana na bidhaa kutoka nje ya nchi kwa sababu ya gharama kubwa ya uzalishaji inayosababishwa na bei kubwa ya umeme, maji, mawasiliano na usafirishaji. Tatizo hili linafahamika na linashughulikiwa katika Sheria zifuatazo: Sheria ya Udhhibiti wa Miundombinu ya nishati, maji, usafirishaji wa majini na nchi kavu na mawasiliano, yaani *SUMATRA* na *KEULA*. Aidha, Serikali imekwisha chukua hatua za makusudi za kupunguza gharama za uzalishaji umeme kutoka senti 13 ya senti za dola za Marekani mpaka senti 8 yaani dola za Kimarekani kwa kilowati kwa saa moja.

Hoja kutoka kwa Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, viwanda vingi malighafi yake inatoka kwenye sekta nyingine zaidi ya viwanda. Serikali ilinde malighafi zinazozalishwa hapa nchini kwa mfano, shayiri ingawa msisitizo wa Sheria hii uko katika kulinda viwanda, lakini mkulima wa shayiri akithibitishwa kuwa kuna shayiri ambayo inakuwa *dumped* au mkulima yeyote akithibitisha hivyo anaweza kupeleka malalamiko yake chini ya utaratibu wa sheria hii. Utafiti ufanyike ili kuona viwanda vingapi vinatumia malighafi ya ndani na vingapi vinatumia malighafi ya nje na uwezekano wa kutoa motisha kwa viwanda vinavyotumia malighafi ya ndani. Serikali inafiki pendekezo hili.

Ugumu wa sheria na umuhimu wa kuelimisha wananchi, hili nimelishalijibu na tunalikubali na tunalifanyia kazi. Wajumbe wa Kamati ya Ushauri wengi wanatoka Serikalini, ukiacha mjumbe mmoja anayetoka *CTI* na mwingine anatoka *TCCIA* na kwamba Sekta binafsi imesahaulika.

Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba, sekta binafsi imesahaulika. Maana hawa Wajumbe wawili hawa wanatoka sekta binafsi kwa kutumia vyombo vyao ambavyo wao wenyewe wameviunda. Lakini Sheria yenyewe hii inahitaji taaluma ambazo kwa sasa ziko katika Idara za Serikali. Hata hivyo, Serikali imeshakubali kuongeza Wajumbe wengine wawili kutoka sekta binafsi. Ungaliwe mkakati madhubuti wa utekelezaji wa sheria hii. Hili tunaliafiki na tutaendelea kulitekeleza. Sheria hii isipingane na utandawazi,

Serikali inaafiki pendekezo hili. Aidha, chimbuko la sheria lina msingi wa kuendeleza utandawazi chini ya Mkataba wa *WTO* na hivyo, haiwezi kupingana na utandawazi.

Mheshimiwa Leonard Derefa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, wamezungumzia kuhusu sheria hii isipoangaliwa vizuri inaweza ikaleta uhaba wa bidhaa nchini. Sheria hii haitarajiwi kuwa chanzo cha upungufu wa bidhaa nchini. Aidha, Sheria hii haizuii bidhaa kuingia nchini hata kama zimepunguzwa bei, isipokuwa Sheria hii hutoza ushuru wa adhabu yaani aidha *Anti-Dumping Duties* au *Countervailing Duties* au *levies* kama sheria inavyosema ama Muswada unavyosema kwa bidhaa zilizopunguzwa bei zikiwa tayari ziko kwenye soko. Hili linajibiwa na kifungu cha 55(i) cha Muswada huu.

Napenda pia kumjibu Mheshimiwa Ngawaiya kuwa, Sheria hii haizuii bidhaa kama matairi kuingia nchini. Lakini sheria hii inakataza *dumping* ya matairi na kwamba matairi duni yatadhibitiwa na Sheria chini ya *TBS*. Bidhaa za viwanda vyetu hazipatikani jimboni kwake, mathalani sukari na nguo. Sukari ya Kilombero haipatikani kabisa jimboni Mbozi Magharibi. Muswada huu ukizuia bidhaa hizi itasaidia nini? Hili lielezwa na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi.

Ni kweli baadhi ya viwanda vyetu havina uwezo wa kukidhi mahitaji, yaani *demands* ya Watanzania. Muswada huu nia yake siyo kuzuia bidhaa za nje kama sukari kutoka Zambia au Malawi. Bidhaa hizi zitatozwa ushuru wa adhabu pale tu tutakapothibitisha kuwa kuna *dumping*. Ni kweli pia nchi yetu haijitoshelezi katika uzalishaji wa sukari. Mahitaji yaliyopo ni kiasi cha zaidi ya tani laki tatu, lakini uzalishaji wa viwanda vilivyopo ni wastani wa tani laki moja na ishirini elfu. Hivyo ni wazi pengo hilo lazima lizibwe na sukari kutoka nje. Sukari kutoka Malawi au Zambia ni sehemu ya ushirikiano wa nchi yetu na nchi wanachama wa *SADC*. (*Makofi*)

Tumekwisha saina mkataba wa *Free Trade Area* tangu Agosti, 2000. Hili ni jambo jema. Aidha, nchi zetu chini ya utaratibu tuliojiwekea, tunahimiza biashara kupita mipaka yetu yaani *Cross Boarder Trade* ili kuondoa kero za wananchi katika kupata mahitaji yao. Tanzania pia inauza bidhaa zake katika nchi hizo. Hata hivyo, pamoja na makubaliano haya haituzuii sisi kudhibiti *dumping* katika sehemu zetu kutokana na bidhaa kutoka nchi hizo.

Uwezekano wa Sheria hii kuwezesha bidhaa zinazoweza kununuliwa na watu wenye uwezo tofauti kifedha katika jamii, Mheshimiwa Derefa, Sheria hii haizuii bidhaa kutoka nje kuingizwa nchini, isipokuwa kama bei zake zimepunguzwa kwa makusudi ili kuuwa viwanda au biashara yetu. Hivi sasa kuna bidhaa zinazokidhi mahitaji ya viwanda ya viwango mbalimbali vya uwezo wa kifedha hususan bidhaa za nguo na kadhalika. Lakini vile vile mitumba ya nguo imeruhusiwa kukidhi haja ya baadhi ya wananchi wetu.

Tuwasaidie wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa, walaji hununua wanachokihitaji tu, siyo wanachokitaka. Hili lilielezwa na Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail. Sheria hii haiwapigi vita waagizaji bidhaa kutoka nje. Sheria hii itawashughulikia wanaokiuka maadili ya biashara. Niseme pia kuwa mwenye uwezo hununua anachotaka, asiye na uwezo hununua anachokihitaji nia iwe hapo baadaye kuwezesha Watanzania wote hatimaye waweze kununua wanachotaka. Yaani ndiyo mfumo wa uchumi wa soko. Huko tunakokwenda shabaha iwe hiyo, lakini kwa sasa hatuwezi kwa sababu hatuna uwezo mkubwa.

Viwanda vitumie malighafi kutoka nchini, nakubaliana na ushauri huu wa Mheshimiwa Derefa. Hata hivyo, matumizi ya malighafi toka ndani ya nchi yetu yanategemea kwanza iwapo malighafi hiyo inakuwapo. Pili, inapatikana kwa bei ya ushindani. Tatu, ipo kwa wingi kutosheleza mahitaji ya kiwanda husika kwa kipindi chote cha uzalishaji unaotarajia kuleta faida.

Kuhusu suala la mafuta ya kula, ambalo limezungumziwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela. Kwanza, napenda kueleza kuwa hoja za kiuchumi huwa zinabadilika mara kwa mara kwa maana siyo sera zetu lazima zierendane na mabadiliko hayo. Katika sera zetu za kulinda uchumi tunazingatia kuendeleza wazalishaji wa mbegu ili viwanda vya mafuta vitumie mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Lakini ikumbukwe kuwa pia kuna viwanda vikubwa vilivyoanzishwa hivi



karibuni tu. Viwanda hivyo kwa mfano, *VIDCO*, kiko pale Mikocheni, kitakapokuwa kinazalisha kikamilifu kitakuwa kinazalisha tani 150,000 za mafuta ya kula.

Kiwanda kingine ni cha *MUZA*, cha zamani kidogo lakini sasa kimepanuliwa. Kina uwezo wa kuzalisha tani 80,000 za mafuta. *Bestigler* kiko Mbagala kule, kina uwezo wa kuzalisha tani mpaka 20,000. Kwa hiyo, jumla ya uwezo ni tani 250. Lakini mahitaji ya mafuta ndani ya nchi yetu ni tani 200 kamili. Lakini uzalishaji wa sasa ni tani 44,000 yaani asilimia 22 tu.

Kwa hiyo, huwezi kuzuia viwanda vikubwa hivi vizalishe kwa sababu *capacity* yetu tayati ni ndogo na Mheshimiwa Mzindakaya ametukumbusha kuhusu kujitegemea. Hapa ndiyo tunataka tujitegemee katika mafuta ya kula. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninachosema ni nini? Ninachosema ni hivi, njia mbadala lazima tuzitafute za kukidhi mahitaji ya viwanda hivi, la sivyo vitakuwa havina maana ya kuvivutia viwanda kutoka nchi za nje viingie ndani ya nchi yetu au kuwavutia Watanzania kujenga viwanda namna hii. Kwa hiyo, lazima kuwe na Kanuni au Sheria au taratibu tofauti ili kuviwezesha viwanda hivi vikidhi uzalishaji huu tunaoutaka. Viwanda vikubwa ambavyo vimejengwa Tanzania pia vimeweza kuongeza ajira kwa mfano, viwanda viwili tu kile cha *VIDCO* na *MUZA*. Viwanda vile viwili sasa vina uwezo wa kuwaajiri watu 1,500. Kwa hiyo, hauwezi kuwa uchumi mzuri kuvifunga. Lazima viendelee kuzalisha, kwa sababu hili ndiyo lengo letu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ambaye anasema *business physiology* na *attitude* za watu na wananchi wetu kuwa na tabia ya kupenda bidhaa za nje. Hili nakubaliana nalo. Itakumbukwa kwamba, nimekuwa nikisisitiza kampeni ya nunua bidhaa za Tanzania, jenga Tanzania na nimeshasema hapa Bungeni mara nyingi na kwingineko na kuliomba Bunge hili lisaidie katika kampeni hii na niliagiza pia mwaka 2003 kwamba, baadhi ya Miji, Minispaa na Jiji, waweke mabango ya kuonyesha hili, huu msimamo, nunua bidhaa za Tanzania, jenga Tanzania. Lakini mpaka leo hakuna mafanikio. Kwa hiyo, kuanzia sasa nimeagiza Wizara yangu ya Viwanda na Biashara, itaandaa utaratibu wa kuweka mabango haya yenye ujumbe huu wa nunua bidhaa za Tanzania, jenga Tanzania. Kwa kuanzia tu tutaweka mabango haya katika miji mikubwa na miji ya mipakani kama ifuatavyo: Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mwanza, Morogoro, Bukoba na Mbeya na ninasikia ya kwamba, tutakapokuja hapa kwenye Bajeti mabango haya yatakuwa tayari yameshawekwa na wenyewe wako kule wanasikia.

Gharazama za uzalishaji viwandani ni kubwa. Ni kweli gharama za uzalishaji ni kubwa, ukubwa wa gharama unatokana na sababu mbili. Kwanza, gharama ambazo udhibiti wake uko ndani ya uwezo wa viwanda vyenyewe. Pili, gharama ambazo udhibiti wake uko nje ya uwezo wa viwanda zitokanazo na matatizo nje ya viwanda hivyo. Kwa mfano, gharama ya umeme na gharama ya usafirishaji. Kutokana na hali hii natoa wito kwa wenye viwanda kwanza kuzingatia suala la kupunguza uzalishaji ndani ya viwanda vyenyewe, lazima wapunguze ili viwanda hivyo vizalishe bidhaa kwa bei nafuu zaidi. Aidha, upande wa umeme Serikali imeweza kupunguza gharama kama nilivyosema pale mwanzo kutoka senti 13 hadi senti 8 na tunaendelea na jambo hili siyo kama tumefikia mwisho, tunaendelea kulitazama hili suala. Kwa hiyo, tutalishughulikia.

Lakini vile vile, Serikali inajenga barabara kwa msimamo mkali zaidi ili kuwezesha huduma ya barabara ili kupunguza gharama za usafirishaji wa malighafi na vile vile usafirishaji wa bidhaa kutoka viwandani kwenda kwa watumiaji. Swali lingine ni pamoja na kuwepo sheria hii ya *Anti-Dumping*, bado upo uwezekano wa *dumping* kuendelea na hivyo kutokukidhi malengo na matarajio ya sheria. Hili alilisema Mheshimiwa Simpasa. Wizara imelitambua hili na itachukua hatua za makusudi kudhibiti hali hiyo. Wizara tayari imekwishaanza kuelimisha angalau Waheshimiwa Wabunge, tayari wamepata fursa hii ya kuelimishwa lakini tutaendelea juhudi kuwaelimisha wadau wengine ili waweze kuzingatia utekelezaji wa Sheria hii. Lakini vile vile ndani ya Wizara tutaongeza taaluma kwa wafanyakazi ili waweze kusimamia vizuri sheria hii. Wizara pia inatambua kuwa utekelezaji wa Sheria hii utategemea ushirikiano kutoka kwa wadau wote hivyo tutawashirikisha kikamilifu. Hatua nyingine ya kukabiliana na tatizo hili ni kuhakikisha kuwa, kwa kuwepo kwa kifungu cha *Anti-Dumping* na *Countervailing Measures* katika

mikataba baina yetu na nchi zingine yaani zile *Bilateral Agreements*, kila mara tutazingatia kifungu hiki kiwepo ili kuhakikisha *dumping* haifanyiki ndani ya jamii yetu.

Iwepo Bodi ya udhibiti licha ya Kamati ya Ushauri, hili limechangiwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Nakubaliana nalo lakini nitataka kwanza tuanze na Kamati ya Ushauri, hapo tutakapoona kwamba tumepata uzoefu kwamba tunahitaji Kamati ya Ushauri tu au Bodi ya Udhibiti, tutafanya hivyo. Kifungu cha 28 cha Muswada kinasema kama Kamati inaweza kuanzisha uchunguzi bila kusubiri malalamiko. Hili najibu hoja yake ya pili kwamba, hii Kamati inakaa tu, inasubiri tu. Haisubiri, yenyewe pia ni *full active* kwa maana hii.

Katibu wa Kamati asiwe Mkurugenzi wa Biashara. Hili alilieleza Mheshimiwa Shekiffu, Mbunge wa Lushoto. Sababu ya kumfanya Mkurugenzi wa Biashara kuwa Katibu wa Kamati hii, ni kuwa kiungo kati ya Kamati, wadau na Wizara. Lakini hii pia ni pamoja na kazi yake. Hata hivyo, atakuwa na wasaidizi. Atakuwa na Sekretarieti ili kuongeza ufanisi, ili Mkurugenzi wa Biashara ndiyo *repository* wa *instruments* za utekelezaji wa makubaliano ya *WTO*. Kwa hiyo, huyu hatuwezi kumkwepa, lazima awepo pale, maana bila huyu mambo yote haya ya *Anti-Dumping and Countervailing Measures* hayataweza kufanikiwa. Kwa hiyo, ni muhimu tuwe nayo.

Kamati iwe na wawakilishi wa *Consumers Association* na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Hili nalo limeelezwa na Mheshimiwa Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi. Nakubali kuwa *Consumers Association* na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni wadau. Lakini pia wapo wadau wengine wengi, siyo rahisi kuwa na wote hawa ndani ya Kamati. Ni vema tupate uzoefu na baadaye tutafanya marekebisho kwenye Muswada au Sheria. Tuwe na Mpango wa Taifa wa kujitegemea. Mfano baadhi ya sekta zimeanza kujitegemea. Kutokana na hatua madhubuti za kuinua uchumi ikiwa ni pamoja na ubinafsishaji wa viwanda, mashirika, kuvutia wawekezaji ndani ya nchi na ukarabati wa viwanda vyetu. Tumefanikiwa kwa sasa hivi kufikia hali ya kujitegemea katika viwanda vya Bia, viwanda vya Sabuni, viwanda vya Sigara, viwanda vya *Cement* na viwanda vya Ngano. Lakini kuna ushahidi kwamba hivi karibuni tutafikia kujitegemea katika viwanda vya mafuta ya kupikia. Kwa hiyo, hili jambo linaendelea vizuri.

Mheshimiwa Abu Kiwanga, anasema Serikali iandae orodha ya viwanda ambavyo vimefikia uzalishaji wa bidhaa zenye viwango na ubora unaokubalika. Hili tunalikubali na tumelifanyia kazi. Lakini napenda kusesitiza kwamba, viwanda vya namna hii vinajulikana na ni vile vyenye nembo ya ubora wa *TBS*. Viwanda kama sekta bado ni ndogo na mchango wake ni mdogo. Hili amelisema Mheshimiwa Balozi Diria. Nakubaliana na hoja hii kuwa sekta ya viwanda bado ni ndogo na changa. Katika nchi za Ulaya, sekta ya viwanda imechukua miaka mingi kupevuka. Sheria kama hii itatusaidia kukuza sekta ya viwanda. Kwa hiyo, kwa nini tumeanza na *Blanket Anti-Dumping Law*? Kwa sababu tunataka sheria hii iweze kulinda kwanza viwanda vyote baadaye huko tukikomaa ndiyo tutaanza ku-*focus* viwanda gani tunaweza kuvizua na ni viwanda gani tunaweza tukaviachia vipambane na ushindani bila mashindano.

Mheshimiwa Mutungirehi, alizungumzia suala la *subsidy*, siyo kitu kibaya anasema Mheshimiwa Mutungirehi. Anasema hata kule Marekani wanatoa *subsidy*, lakini Marekani na Ulaya ndiyo wahalifu katika eneo hili na sisi tunasema tuondoe ruzuku kwa sababu ruzuku hii inaharibu biashara yetu. Kwa sababu sisi hatuwezi kupeleka kule katika masoko yao. Wao wanapeleka kwenye masoko yetu, wao masoko yao wanayazuia. Sasa hili tunasema Marekani, Jumuiya ya Ulaya, Japan, wasitumie *subsidies* kuharibu biashara ya Kimataifa. Huu ndiyo ubishi tuliofanya kule *WTO* kule Mexico mwaka 2003. Ubishi wetu wa kuvunjika yale mazungumzo kwa sababu ya suala hili kwamba *subsidy* hizi lazima ziondolewe na siyo vizuri sisi nchi maskini kushabikia *subsidies*, maana hatutashinda kuwakemea wakubwa hawa.

Naomba sasa nimalizie kwa kusema kwamba, kwa mujibu wa maelezo na michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli Sheria hii au Muswada huu wa *Anti-Dumping* sasa unaeleweka, siyo kama pale mwanzo. Kwa hiyo, nina hakika watatuunga mkono katika kuupitisha Muswada.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kukabiliana na Bidhaa Kutoka kwa Wawekezaji wa Nje Wenye Nia ya Kuua Ushindani wa Ndani wa Mwaka 2003**  
*(The Anti-Dumping and Countevailing Measures Bill, 2003)*

**SPIKA:** Nieleze kwamba, Muswada kama mnavyouna Waheshimiwa Wabunge, una vifungu 77 vilivyopangwa katika sehemu 13. Kwa hiyo, kwa utaratibu wetu tuliokwisha kuuzoea, badala ya kwenda kifungu kimoja kimoja, Katibu ataita sehemu halafu tutawahoji kama mnakubali vifungu vyote vilivyomo katika sehemu hiyo vipitishwe. Tunaanza kwa utaratibu huo.

Sehemu ya 1

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 2

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 3

Sehemu ya 4

Sehemu ya 5

Sehemu ya 6

Sehemu ya 7

Sehemu ya 8

Sehemu ya 9

Sehemu ya 10

Sehemu ya 11

Sehemu ya 12

Sehemu ya 13

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kukabiliana na Bidhaa Kutoka kwa Wawekezaji wa Nje Wenye Nia ya Kuua Ushindani wa Ndani wa Mwaka 2003**  
*(The Anti-Dumping and Countevailing Measures Bill, 2003)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kujihami na Bidhaa Kutoka Nje zinazouzwa kwa bei ya chini kwa makusudi ili kujipatia soko na hatua za kuzuia na kufidia athari zake yaani *Anti-Dumping and Countevailing Measures Bill, 2003* na kuukubali sehemu kwa sehemu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kuwa Muswada uitwao *the Anti-Dumping and Countevailing Measures Bill, 2003* kama ulivyojadiliwa, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Mabadiliko katika Sheria ya  
Ardhi wa Mwaka 2003 (*The Land (Amendment) Bill, 2003*)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao *The Land Amendment Act, 2003* kama *Bill Supplement* Na.1 ya 9 January, 2004 na orodha ya mabadiliko yaliyoambatishwa kwenye orodha ya shughuli, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukutakia wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kheri na baraka nyingi kwa mwaka huu wa 2004. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge, namtakia kila la kheri. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Toleo la Kwanza la Muswada huu lilichapishwa tarehe 17/10/2003 na kusomwa mara ya kwanza humu Bungeni mwezi Novemba, 2003. Baada ya hapo, Serikali iliupitia tena Muswada huo na kufanya marekebisho kidogo na ukachapishwa upya kwa Toleo la Tarehe 9/1/2004. Tarehe 19 na 26/1/2004 vilifanyika vikao vya kuwashirikisha wadau kupitia Muswada huu na kutoa maoni yao. Tarehe 27/1/2004, Kamati ya Kilimo na Ardhi ilikaa na kuupitia rasmi Muswada huu na kutoa uamuzi wake kama utakavyowasilishwa na Mwenyekiti mhusika.

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo vyote ulitolewa ushauri, maoni na mapendekezo mazuri ya kuboresha maudhui ya Muswada. Serikali iliyapokea na kuyakubali mapendekezo kadhaa yaliyotolewa na kuamua kufanya mabadiliko katika Muswada wa pili. Kwa hiyo, Muswada ukachapishwa upya lakini tarehe ikabakia ile ile tarehe 9/1/2004 na Toleo hilo jipya ndilo lililowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu pamoja na orodha ya mabadiliko machache.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali nzuri ya ushirikiano iliyojionyesha katika zoezi hili, napenda kutumia nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Eliachim Simpassa, Mbunge wa Mbozi Magharibi na Waheshimiwa Wabunge wajumbe wa Kamati kwa uchambuzi wao wa kina, ushauri na maelekezo muhimu waliyotoa kuhusu maudhui ya Muswada huu na mikakati ya utekelezaji kwa jumla. (*Makofi*)

Pili, nawashukuru wadau wote ambao wameshirikiana nasi katika nyakati na ngazi mbalimbali hadi hapa Bungeni kwa takribani miaka miwili sasa kushauriana na hatimaye kufikia makubaliano ya msingi ambayo yamo kwenye Muswada huu. Tatu, Muswada huu usingeweza kuwasilishwa mbele ya Bunge hili Tukufu bila msaada na kazi kubwa iliyofanywa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge na timu yake ya wataalam. Wote kwa pamoja nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba mwezi *February, 1999* lilipitisha Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, sheria hizo mbili zilipitishwa ili kutekeleza Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Mara baada ya sheria hizo mbili kupitishwa wadau kadhaa walianza kutoa malalamiko na hoja za kuelezea kasoro au mapungufu yaliyomo katika baadhi ya vifungu vya Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999. Miongoni mwa wadau hao ni Mabenki na taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa wananchi. Hoja nyingi ambazo zimekuwa zikitolewa zinalenga Sehemu ya Kumi (*Part Ten*) ya Sheria hiyo inayohusu rehani ya ardhi (*mortgages*) katika utoaji mikopo ya fedha. Baada ya mashauriano ya muda mrefu kwa kuwahusisha wadau wanaowakilisha wakopeshaji na wakopeshwaji, tumefikia makubaliano ya msingi ya kufanya mabadiliko ya baadhi ya vifungu vya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada na mabadiliko yake ni kuweka mazingira mazuri kwa wakopeshaji kutoa mikopo kwa wakopeshwaji kuweka ardhi rehani kwa utaratibu ulio rahisi na wa haki kwa pande zote mbili. Lengo ni kuondoa vikwazo vya msingi vinavyolalamikiwa na wadau ili waweze kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya msingi yako katika maeneo mawili ya Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999. Eneo la kwanza linahusu vifungu vya 2, 19, 20 na 37 vya sheria hiyo. Kifungu cha 2, mabadiliko yanayopendekezwa hapa ni kuongeza tafsiri ya neno *sale*, kama ilivyo kwenye Ibara ya 2 ya Muswada huu. Tafsiri inayopendekezwa ni uhamisho wa miliki kwa masharti ya miliki yaliyoainishwa katika Hati Miliki. (*Makofi*)

Kifungu cha 19, mabadiliko yanayopendekezwa hapa ni kufuta Kijifungu 2 na kuweka kipya kama kilivyoandikwa kwenye Ibara ya 3, ukurasa wa nne wa Muswada huu. Mabadiliko haya yanafafanua kwa upana zaidi masharti ya upangishwaji na ukodishaji ardhi kwa wageni, yaani watu ambao sio raia.

Kifungu cha 20, mabadiliko yanayopendekezwa hapa ni kufuta Kijifungu cha 3 na kuweka kipya kama kinavyosomeka kwenye Ibara ya 4 ukurasa wa nne wa Muswada huu. Mapendekezo ya mabadiliko haya yanafafanua masharti ya kulipwa fidia kwa wageni waliomilikishwa ardhi kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999. Muswada unatoa ufafanuzi wa sheria ilivyo ambapo wageni watastahili kulipwa fidia ya maendeleo waliyoyafanya katika ardhi hiyo na sio kwa thamani ya ardhi tupu. Wakati wageni hao wanamilikishwa ardhi hiyo walimilikishwa kwa kupewa *granted right of occupancy* na bila malipo yoyote ya fidia ya ardhi kwa wale waliokuwa wanamiliki ardhi hiyo na kwa hiyo hawatakuwa na haki ya kudai fidia ya ardhi isiyoendelezwa endapo Hati Miliki itabatilishwa au kutwaliwa kwa mujibu wa sheria.

Kifungu cha 37, msingi wa mfumo wa umilikaji ardhi nchini ni kuhakikisha ardhi inaendelezwa na kutumiwa kwa manufaa ya Watanzania. Kwa raia kumilikishwa ardhi na kukaa nayo bila kuitumia kwa ustawi wake hakumsaidii Mtanzania. Kwa hiyo, lengo la mapendekezo ya Muswada ni kuhakikisha ardhi inatumika kuleta ustawi na maendeleo ya Watanzania. Kwa lengo hili, pamoja na mambo mengine Muswada unapendekeza raia asiyeweza kuiendeleza ardhi aliyomilikishwa aihamishe miliki yake kwa raia mwenzake anayeweza kuiendeleza vinginevyo mwananchi huyo anapewa fursa ya kutohamisha miliki yake moja kwa moja bali kuingia ubia na mtu mwingine ili aweze kuiendeleza na kuitumia (*partial transfer of interest*)

Mheshimiwa Spika, ili kuweka mazingira mazuri yatakayoweza kuwepo shughuli mbadala kwa wananchi watakaomua kuuza ardhi yao, mapendekezo ya Muswada huu yanazingatia sera na mikakati mingine ya Serikali inayolenga kumwezesha Mtanzania kuondokana na umaskini. Sera na mikakati hiyo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi (*National Economic Empowerment Policy*) na Mikakati ya Kuondoa Umaskini (*Poverty Alleviation Strategy*). Mabadiliko yanayopendekezwa hapa ni kufuta vijifungu vya 8 na 9 na badala yake kuweka vijifungu vipya kama vinavyosomeka katika Ibara ya 5 ya Muswada huu. Mabadiliko haya yanalenga kuruhusu uhamishaji wa Hati Miliki isiyoendelezwa kwa kuruhusu uzaji kwa masharti ya miliki husika. Sharti la msingi ni kwamba uhamishaji wa Hati Miliki ya aina hiyo ufanyike kati ya raia na raia na siyo kwa wageni kwa madhumuni yaliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili la mabadiliko linahusu Sehemu ya Kumi (*Part Ten*) ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 iyohusuyo kuweka rehani ardhi kama dhamana ya mkopo. Mabadiliko yanayopendekezwa katika eneo hili ni kufuta Sehemu ya Kumi ya sasa inayohusu rehani na badala yake kuweka Sehemu mpya ya Kumi. Sehemu hii ina vifungu kuanzia 111 hadi 142. Baadhi ya vifungu vimependekezwa kufanyiwa marekebisha, kufutwa na vingine kutobadilika. Sehemu hiyo imeandikwa upya ili kumrahisishia msomaji au mtumiaji wa sheria hii kuisoma na kuitumia katika mtiririko ambao ni rahisi kueleweka.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yanayopendekezwa katika Sehemu hii ya Kumi yanalenga kurahisisha, kuharakisha na kutenda haki kwa wakopeshaji na wakopeshwaji. Tunapozungumzia ardhi inayostahili kuwekwa rehani tunamaanisha aina mbili za ardhi zenye sifa hizo. Kwanza ni ardhi yenye Hati Miliki inayotolewa na Serikali (*Granted Right of Occupancy*) kwa kipindi maalum hususani yenye asili ya upangishwaji (*Lease Hold*). Pili ni ardhi yenye Hati Miliki ya Kimila (*Custom Right of Occupancy*) ambayo sasa inatolewa au kuthibitishwa na Serikali ya Kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 na haina ukomo wa kumiliki. Hati Miliki za aina mbili zote zina hadhi sawa na zinapaswa kutambuliwa na taasisi za fedha kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu pendekezo la kufuta Kifungu kinachohusu wakopeshaji wadogo (*small mortgages*). Baadhi ya wadau wamelalamikia eneo hili na napenda kutoa ufafanuzi. Katika Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 chini ya Kifungu cha 115 ipo dhana ya kuwalinda wadaiwa wadogo kwa kuwawekea kinga kubwa kuliko wadaiwa wengine lakini katika utekelezaji wa dhana hii imekuwa vigumu kutambua kiwango stahili cha mikopo midogo kinachopaswa kulindwa.

Kwa mujibu wa taasisi za kutoa mikopo na Mabenki tafsiri ya rehani ndogo ni tofauti kabisa na tafsiri iliyomo katika sheria. Ili kuepuka utata huo, inapendekezwa mkazo uwekwe katika matumizi ya ardhi kuliko kiwango cha mkopo ambapo kinga imependekezwa iwekwe katika ardhi ya makazi inayokaliwa na mkopaji au ya kilimo, ufugaji inayotumiwa na mkopaji kwa ajili ya kipato chake. Ulinzi wa mkopaji ulenge katika matumizi ya ardhi yake na sio kiwango cha mkopo kutoka katika Mabenki. Kwa msingi huo, mabadiliko yanayopendekezwa ni kufuta Kifungu cha 115 cha Sheria kinachozungumzia wakopaji wadogo. Ulinzi wa mkopaji umezingatiwa katika Kifungu cha 130(5) cha Muswada huu. Aidha, kutokana na mapendekezo hayo, imelazimu kufanya marekebisho madogo katika vifungu ambavyo vimezungumzia wakopaji wadogo ambavyo ni vifungu vya 117, 119, 125, 127, 128, 138.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa nipitie vifungu kama vinavyopendekezwa chini ya Ibara ya 6 ya Muswada huu. Kifungu cha 111, inapendekezwa kufanywa mabadiliko kwa kuondoa neno "*before*" katika Kijifungu cha 1 ambalo linahusisha mikataba iliyofanyika kabla ya Sheria Mama na mabadiliko haya kuanza kutekelezwa. Kwa Muswada huu, inapendekezwa Sheria Mama na mabadiliko haya yasihusishe mikataba yote iliyofanyika awali.

Kifungu cha 112, mabadiliko yanayopendekezwa na nyongeza ya kifungu kitakachotoa tafsiri ya maneno yafuatayo katika Kijifungu cha pili kwanza ni *matrimonial home*, tafsiri ya nyumba ya ndoa iliyotumika kwenye Muswada huu ni ile ile iliyomo kwenye Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Endapo tafsiri hiyo haieleweki vizuri basi wakati muafaka wa kufanya marejeo ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 hilo litazingatiwa lakini sio kupitia Muswada huu. Neno *mortgager* yaani mkopaji na neno lingine ni *mortgagee* yaani mkopeshaji na neno lingine ni *third party mortgage* yaani mkopo wa dhamana ya ardhi inayotolewa na mtu ambaye si mkopaji. Ufafanuzi huu unatolewa kwa maneno haya kwa sababu maneno haya yanatumika tu katika Sehemu hii ya Kumi ya Sheria hii. Kwa hiyo, ni muhimu tueleze maana yake ili yaweze kueleweka. Kifungu cha 113, kifungu hiki kinatoa utaratibu wa mmilikaji ardhi kuweka rehani maslahi yake katika ardhi ili kudhamini deni hii ni pamoja na udhamini wa mkopaji asiye kuwa na ardhi yaani *third party mortgage* kama ulivyofafanuliwa katika kifungu cha 112.

Kifungu cha 114, kifungu hiki kinatambua ndoa za mitala, narudia, kifungu hiki kinatambua ndoa za mitala. Aidha, Kifungu 114(2) hakianzishi aina mpya ya ndoa bali kinalinda haki za wanandoa wenye ndoa zilizosajiliwa au ambazo hazikusajiliwa kama zinavyotambuliwa katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Kifungu hiki kinaeleza utaratibu wa kuweka dhamana ya nyumba ya wanandoa dhamana hiyo haina budi kupata idhini ya mwanandoa au wanandoa wa mkopaji wanaoishi katika nyumba hiyo ya ndoa. Pia kinafafanua kuwa mweza/wenza wa ndoa wa mkopaji wanaotambuliwa ni yule/wale walioandikishwa kwenye Daftari la Usajili wa Ndoa linalohifadhiwa na Ofisi ya Msajili wa Ndoa au yule/wale ambao wanatambuliwa kisheria kuwa ni mweza/wenza wa ndoa.

Mapendekezo hayo yanatoa jukumu kwa Mabenki na taasisi za fedha kuchukua hatua za kujihakikishia kuwa kama nyumba inayokusudiwa kuwekwa rehani ni ya makazi ya wanandoa, wanandoa wote wanaoishi katika nyumba hiyo wanaridhia. Vifungu vya 115-119, mapendekezo kwenye vifungu hivi ni kuhuisa maneno mapya yanayopendekezwa kwenye Muswada huu bila kuathiri maudhui yaliyokuwemo awali.

Kifungu cha 120, kifungu hiki kinazungumzia mabadiliko ya riba ya rehani. Viwango vya riba vinaweza kubadilika na kama ikitokea hivyo basi ni lazima mkopaji apewe taarifa na mkopeshaji na kuanza kutumika pale mkopaji atakapokuwa amepokea taarifa hiyo. Katika hali halisi imeonekana kwamba sio rahisi kutoa taarifa ya mwezi mmoja kabla ya mabadiliko ya riba ambayo inabadilika mara kwa mara.

Hivyo inapendekezwa kuwepo utaratibu kwa mkopeshaji kutoa taarifa ya mabadiliko ya riba zinapobadilika mara kwa mara bila ya kuweka muda maalum.

Kifungu cha 121, sheria ya Ardhi imeweka masharti kwa mkopeshaji kuruhusiwa kulipa mkopo wote au kuikomboa mapema ardhi iliyowekwa rehani. Imedhihirika kwamba masharti haya ni kikwazo kwa mkopaji na mkopeshaji kwa kuwa kuna gharama zinazohusika. Inapendekezwa pawepo na utaratibu wa mkopaji kuruhusiwa kulipa mkopo wote wakati wowote au kuikomboa ardhi iliyowekwa rehani. Pia inapendekezwa kwamba pale ambapo mkopaji anaamua kulipa mkopo mapema kabla ya muda wake itakuwa marufuku kwa mkopeshaji kuweka masharti yenye lengo la kukwamisha azma hiyo ya mkopaji. Atakachotakiwa kufanya mkopaji ni kulipa deni lote analodaiwa na mkopeshaji pamoja na riba ya mwezi mmoja tu.

Vifungu vya 122-125, mapendekezo kwenye vifungu hivi ni kuhuisha maneno mapya yaliyopendekezwa kwenye Muswada huu bila kuathiri maudhui ya awali. Hata hivyo, napenda kutoa ufafanuzi kuhusu Kifungu cha 124(j). Nia ya kijifungu hiki ni kuhakikisha kuwa mkopaji anatimiza wajibu wake kisheria kupitia kwa mkopeshaji kwa mfano kulipa kodi, ada au bima. Pia kuitunza ardhi au mali iliyowekwa rehani isiharibike. Matumizi ya fedha kwa ajili ya malengo hayo ni yale yaliyo ya lazima endapo patatokea ubishani kuhusu matumizi yaliyo ya lazima inategemewa kwamba Mahakama itakuwa na jukumu la kutoa tasfiri hiyo.

Kifungu cha 126, katika Muswada huu zinapendekezwa hatua zinazoweza kuchukuliwa na mkopeshaji inapotokea mkopaji ameshindwa kutimiza masharti ya mkopo. Hatua hizo ni kwanza kuteua Msimamizi wa mapato yanayotokana na ardhi iliyowekwa rehani. Pili, kukodisha ardhi iliyowekwa rehani. Tatu, kuichukua na kuitumia ardhi iliyowekwa rehani na nne kuiuza ardhi iliyowekwa rehani na kama ardhi ni ya kimila masharti ya Kifungu cha 30 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 yatatumika. Hatua hizo zimefafanuliwa katika vifungu vya 127,128,129.

Kifungu cha 127, Muswada huu unapendekeza utaratibu wa kutoa ilani kwa mkopaji aliyeshindwa kutekeleza masharti ya mkopo. Ikumbukwe kwamba jukumu la kulipa mkopo linaanza tokea siku ya kuingia mkataba wa kukopa hivyo ilani inayotolewa ni hatua ya kumkumbusha mkopaji wajibu wake anaoujua tangu awali. Katika hali hiyo, inapendekezwa hatua ya kuuza ardhi iliyowekwa rehani ichukuliwa baada ya kutolewa ilani ya siku 30 ambazo zitaanza kuhesabiwa baada ya mkopaji kupokea ilani. Utaratibu unaopendekezwa unazingatia mazingira magumu ya mawasiliano hasa kwa wananchi waishi vijijini ambao pia wamepewa fursa sawa ya kuanza kuhesabu siku 30 za ilani tangu siku ya kupokea ilani.

Baada ya kumalizika muda baada ya kupokea ilani Kifungu cha 140 cha Muswada kinampa mkopaji fursa ya kuiomba Mahakama muda wa kutimiza masharti ya mkopo muda ambao Mahakama itaona inafaa. Pamoja na utaratibu unaopendekezwa ardhi hiyo haitauzwa bila kibali cha Mahakama. Aidha Waziri anapewa uwezo wa kutunga kanuni zitakazoelekeza utoaji wa ilani.

Mheshimiwa Spika, yako mazingira ya kuzingatia endapo mkopaji akifariki kabla ya kulipa au kutimiza masharti ya mkopo. Kwa kuzingatia ukweli huo, mapendekezo ya Muswada huu yatatekelezwa sambamba na sheria za mirathi. Kwa hiyo, mkopeshaji anapokufa ardhi iliyowekwa rehani ni sehemu ya mali ya marehemu zinazolazimika kuwekwa chini ya Msimamizi au mrithi ambaye atachukua nafasi ya mkopaji kwa lengo la kulipa deni. Hivyo hatua yoyote kuhusu mali ya marehemu itachukuliwa baada ya Msimamizi wa mirathi au mrithi kuteuliwa. Kifungu cha 128, mapendekezo chini ya kifungu hiki ni kuweka taratibu za uteuzi, wajibu na mamlaka ya usimamizi yatokanayo na ardhi iliyowekwa rehani. Taratibu hizo zinazingatia ilani chini ya Kifungu cha 127.

Kifungu cha 129, chini ya kifungu hiki inapendekezwa marekebisho yanayozingatia mapendekezo yaliyofanyika katika kifungu cha 127(2) kilichofanya marekebisho ya masharti ya utoaji ilani. Kwa msingi huo, kifungu hicho kinampa mkopeshaji madaraka ya kupangisha ardhi iliyowekwa rehani kwa nia ya kulipa deni, atakuwa na uwezo wa kufanya hivyo pale tu atakapokamilisha taratibu za kutoa ilani zilizoolezwa katika Kifungu cha 127 au kwa amri ya Mahakama.

Aidha, inapendekezwa kuongeza kifungu kidogo cha 129(5) kinachozingatia kifungu cha 130(5)(a), (b) na (c) ili ardhi ya makazi, kilimo na ufugaji isipangishwe isipokuwa kwa amri ya Mahakama.

Kifungu cha 130, pendekezo chini ya kifungu hiki ni kumpa uwezo mkopeshaji kuchukua na kuitumia na kusimamia ardhi iliyowekwa rehani baada ya mkopaji kushindwa kutimiza masharti ya mkopo baada ya muda wa ilani kuisha. Pale ambapo utwaji utahusu ardhi ya makazi, kilimo, ufugaji na ardhi ambayo haiwezi kuchukuliwa kwa amani ni sharti amri ya Mahakama ipatikane kwanza.

Kifungu cha 131, kifungu hiki kinapendekeza misingi na taratibu za mkopeshaji kuiachia ardhi iliyochukuliwa kwa lengo la kuitumia na kuisimamia ardhi iliyowekwa rehani. Kifungu cha 132, chini ya kifungu hiki inapendekezwa mkopeshaji awe na uwezo wa kuiiza ardhi iliyowekwa rehani, mamlaka haya yatatekelezwa baada ya mkopaji kupokea ilani chini ya kifungu cha 127 na kupata kibali cha Mahakama chini ya Kifungu cha 130.

Kifungu cha 133-138, mapendekezo kwenye vifungu hivi ni kuhisha maneno mapya yanayopendekezwa kwenye Muswada huu bila kuathiri maudhui yaliyokuwepo awali. Hata hivyo, yapo maeneo machache yanayohitaji ufafanuzi. Kifungu cha 135(3) kinalenga kulinda na kuendelea soko la ardhi inayonunuliwa kufuatia amri ya Mahakama pia kumpa mnunuzi wa ardhi uhakika wa kuimiliki ardhi aliyoinunua.

Vifungu vya 139-141, chini ya vifungu hivi zinapendekezwa taratibu zitakazofuatwa na Mahakama katika kushughulikia masuala yanayohusu ardhi iliyowekwa rehani. Taratibu hizo ni pamoja na kwanza kutafakari na kumzuia kwa muda mdai kutwaa ardhi iliyowekwa rehani ambayo mdaiwa anaishi au anaitumia kwa kilimo au ufugaji kwa kipato chake ili mdaiwa aweze kutimiza masharti ya mkopo. Pili, kutumia taratibu za kesi za madai ya dharura (summary proceeding) kwa mujibu wa sheria ya kanuni za mwenendo wa kesi za madai. Nia ni kuharakisha maamuzi katika mashauri haya. Tatu, kuangalia upya masharti ya mkopo au urejeshwaji wa rehani endapo itagunduliwa kuwa mkataba wa mkopo ulitokana na udanganyifu au ulaghai.

Kifungu cha 142, katika kifungu hiki ambacho ni cha mwisho, inapendekezwa Mahakama ipewe uwezo wa kutekeleza mamlaka iliyonayo chini ya Kifungu cha 141. Aidha, Mahakama imepewa uwezo wa kutamka kuwa masharti yaliyowekwa katika rehani ni batili au yaendeleo kutekelezwa kwa kufuata marekebisho yaliyofanywa na Mahakama.

Ili mabadiliko yote haya yaweze kufanyika bila kuathiri taratibu zilizopo kwenye Sheria Mama wakati huu, italazimu kufanya marekebisho kwenye maeneo kadhaa ya uendeshaji kama vile taratibu za kuendesha mashauri ya dharura na kanuni zilizotayarishwa na Waziri kuhusu taratibu za uwekaji rehani wa nyumba au ardhi isiyohamishika. Baadhi za hoja zilizotolewa na wadau zitazingatiwa katika zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yanayopendekezwa katika Muswada huu na Sheria za Ardhi kwa jumla yanazingatia maelekezo yaliyomo katika Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010 hususan mkakati wa uwezeshaji kwa wananchi kiuchumi kwa kuunda mazingira muafaka yatakayowapatia fursa ya kumiliki ardhi na kupata mitaji ya kuwekeza katika shughuli za kiuchumi. Dhamira ya mabadiliko haya ni pamoja na kuigeuza rasilimali ardhi iliyokufa na kuwa rasilimali hai inayoweza kuwa chanzo cha mitaji na kupanua shughuli za uchumi kwa wananchi walio wengi.

Kwa maana nyingine mabadiliko haya yanalenga changamoto kwetu wote ya kujishughulisha kupata mitaji ya fedha kwa kutumia rasilimali yetu ardhi kwa ajili ya kuwekeza katika shughuli za kiuchumi. Ardhi ipo na fedha zipo katika Mabenki. Mabadiliko haya yanalenga kurahisisha na kuharakisha matumizi bora ya rasilimali zetu hizi ardhi na fedha ambazo zipo hazitumiki kwa ukamilifu. Ni mabadiliko ya uwezeshwaji kiuchumi kwa Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa Sheria Mama ya Ardhi, mabadiliko haya yanahitaji wananchi waelimishwe vya kutosha, hiyo ndio dhamira yetu tumekwishaanza na tutaendelea. Katika sheria yenyewe pamoja na maelekezo ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa 2000 Aya ya 33 yapo maelekezo ya kutafsiri Sheria hizi za Ardhi katika lugha ya Kiswahili na kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria hizo.



Tutatilia mkazo kuwaelimisha wananchi faida zitokanazo na mabadiliko haya na papo hapo kuwatahadharisha athari zinazoweza kutokea kwa kutozingatia masharti yatakayowekwa katika kuweka ardhi rehani kwa taasisi za fedha zinazotoa mikopo. Kama nilivyokwisha sema kazi hiyo tumekwishaanza na tutaendelea ili kuwafikia walengwa mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya hayabadili mfumo wa umilikaji ardhi nchini, ardhi itaendelea kuwa mali ya umma na Rais mdhamini kwa niaba ya raia wote wa Tanzania, umilikaji utaendelea kuwa wa kupangishwa au kukodisha (*lease hold*) kwa muda maalum na kwa lengo la kuendeleza ardhi husika, atakayeshindwa kuiendeleza ardhi aliyopewa kwa mfumo huu atanyang'anywa na kupewa raia mwingine aliyetayari kuiendeleza, aidha.

Raia wa jinsia zote wenye umri wa miaka zaidi ya 18 wana haki sawa ya kuomba, kupata, kutumia ardhi kwa mfumo huu uliokubalika mijini na vijijini na kwamba ardhi ina thamani. Masuala haya ya msingi yataendelea kuzingatiwa katika sheria hii na mabadiliko haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili mabadiliko haya ya sheria yaweze kutekelezwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa itakuwa lazima kufanya mabadiliko katika sheria nyingine mathalani Mfumo wa Mwenendo wa Mashauri ya Madai *Civil Procedure Code*. Kabla ya kuanza kutekeleza mabadiliko haya tutahakikisha mabadiliko katika sheria hizo husika yamefanyika pia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu na kuipitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati yangu, naomba kwanza nikushukuru kwa nafasi uliyonipa na pili niwasilishe maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu hoja iliyotolewa hivi punde.

Kwa mujibu wa Kanuni 68(1), Kamati ililetwa Muswada huo ili iweze kuupitia na kuukamilisha. Kwa hiyo, kazi imefanyika na kwa mujibu wa kanuni ya 70(2), naomba kutoa maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada kabla sijafanya hivyo, naomba niwatambue wajumbe ambao walishiriki katika kuuchambua Muswada huu ili kuweka kumbukumbu sahihi. Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah; Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Salama Islam, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Robert Mashala na Mheshimiwa Abdilhi Omar Namkulala.

Wengine ni Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Dr. Suleiman Omar, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Masoud Salim, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Ali Salim, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Paul Makolo na mimi mwenyewe Mwalimu Eliachim Simpasa na Katibu wetu Aggrey Nzowa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hiyo kwa jinsi walivyoshiriki kwa njia moja au nyingine kutuwezesha kuuchambua Muswada kadri walivyowasilisha kwetu.

Vile vile niwapongeze na kuwashukuru sana wadau mbalimbali ambao walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Sisi kama wajumbe wa Kamati pia tulishirikishwa kwanza mwezi Novemba, mjini Dodoma.

Wajumbe wa Kamati walialikwa pia kule *Hotel ya Golden Tulip* tarehe 19 Januari, 2004. Kamati kwa upande wake iliwakaribisha wadau katika kikao chake cha tarehe 26 Januari, 2004 ili kupata mawazo yao.

Mheshimiwa Spika, wadau walioalikwa na Kamati na kufika kutoa mawazo yao ni kama hawa ifuatavyo:-

- (1) *Tanganyika Lawyers Society;*
- (2) *Women Legal Aid Centre;*
- (3) *Legal and Human Rights Centre;*
- (4) *Women Advancement Society;*
- (5) *Tanzania Ecumenial Dialog Group;*
- (6) *Landnet (East Africa Tanzania) Chapter;*
- (7) *Tanzania Gender Networking Programme;*
- (8) *Land Rights Research and Resources Institute* au wanajiita Hakiardhi;
- (9) *Tanzania Bankers Association;*
- (10) *National Bank of Commerce 1997 Limited;*
- (11) *Azania Bancorp.*

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri hapa kuwa maoni yetu haya ni maboresho ambayo pia yanatokana na michango ya wadau mbalimbali walioalikwa na wale waliofika kwenye Kamati na katika vikao kama nilivyotaja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, wadau wengi waliipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu katika jitihada za kuwawezesha wananchi kukopa na kutumia raslimali hii ya ardhi. Wadau wachache walionyesha wasiwasi wao katika maeneo fulani fulani kama ifuatavyo:-

- (a) Wakasema, wananchi hawajaelimishwa kiasi cha kutosha kuhusu faida au hasara za sheria hii.
- (b) Wananchi watanyang'anywa ardhi yao kwa kushindwa kurejesha mikopo yao.
- (c) Muda wa siku 30 wa taarifa ya nia ya kumnyang'anya ardhi aliyeshindwa kulipa deni lake ni mfupi mno ambapo haumpi mwenye ardhi fursa ya kujiandaa.
- (d) Mwanandoa atambuliwe kulingana na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na ithibitike kuwa ameshiriki kuizalisha mali hiyo.
- (e) Walisema kwa sheria hii Watanzania watapambanishwa na nguvu za soko huria bila kuwekewa mazingira madhubuti ya kiseru na mikakati itakayowawezesha kupambana na soko huria. Kwa misingi hiyo wananchi watapoteza ardhi wanayomiliki kwa kuwauzia wenye kipato kikubwa na hata kukosa uhakika wa chakula chao.
- (f) Muswada huu unamwondolea mkopeshaji wajibu wa kuwaelimisha wakopaji wadogo wadogo haki na wajibu wao kabla ya kusaini Mkataba wa rehani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kamati baada ya kushiriki kwenye vikao vyote hivi vilivyotajwa hapo juu Kamati ilipata fursa ya kuupitia Muswada huo kwa makini sana na huku ikizingatia maoni ya washiriki na wadau.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada ni kuwaondolea wananchi wa Tanzania umaskini ili waweze kuitumia ardhi yao kupata mkopo kwa maendeleo yao na pia kumruhusu mwananchi mwenye ardhi ambaye hawezi kuendeleza uwezo wa kuhamisha miliki ya ardhi yake kwa mtu mwingine raia kwa

kumwuzia na hivyo kupata fedha kwa ajili ya maendeleo yake. Kwa msingi huo Kamati iliona kwamba Muswada huu umeletwa na Serikali kwa wakati muafaka au umechelewa kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa vile ardhi ni mali kwa mujibu wa Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995 ambayo tumeipitisha hapa Bungeni na kwa Muswada huu mkopaji makini anaweza kufaidika. Sivyo tu, kwa sheria tunayoirekebisha leo, mabenki yalikuwa yanasita kutoa mikopo kwa vile sheria ilionekana kuwalinda sana wakopeshwaji.

Mheshimiwa Spika, si mara moja humu Bungeni bali ni mara kadhaa Waheshimiwa wamekuwa wakilalamika kuwa watu wetu wanashindwa kupata mikopo kutokana na masharti magumu yanayowekwa na benki kwa mikopo hiyo na kwa maana hiyo suala la kuondoa umaskini limekuwa gumu miongoni mwa wananchi. Kamati iliona kuwa sasa jibu la tatizo hilo limepatikana. Sheria hii ikitekelezwa kwa makini, uaminifu na uadilifu mkubwa kati ya pande mbili, mkopaji na mkopeshaji, labda tatizo hili litakuwa limepungua.

Mheshimiwa Spika, katika vikao vyote tulivyoshiriki baadhi ya wajumbe pamoja na baadhi ya wadau tulionyesha wasiwasi fulani kuwa sasa wananchi wetu watanyang'anywa ardhi kama nilivyosema awali lakini ukweli ulibakia pale pale kwamba mali ambayo Mtanzania wa kawaida anaweza kuweka rehani ni ardhi.

Ni vema elimu itolewe kuhusu kujenga dhana ya kukopa na kurudisha. Watanzania tubadilike, Kamati ilisisitiza. Mikopo ina Mikataba yake, ile tabia ya kukopa na kupotea lazima iachwe kabisa. Wananchi wakope kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao siyo kwa matumizi mengine. Siyo mtu anakopa leo badala ya kwenda kufanyia ile shughuli anakwenda kuoa au kufanya mambo mengine ambayo siyo lengo la mkopo. Wakifanya hivyo ni dhahiri wataweza kurejesha fedha walizokopa kwa mujibu wa makubaliano. Zaidi ya yote si kazi ya mabenki na taasisi za kifedha kuhodhi ardhi. Kamati iliridhika na sehemu ya Muswada ambayo inaelezea kuwepo kwa mawasiliano kati ya mkopaji na mkopeshaji.

Mheshimiwa Spika, tumehakikishiwa pia kuwa iwapo mkopeshaji anataka kushika ardhi na ikionyesha dhahiri kuwa mkopaji ameathirika pengine kwa mazao yake ambayo ndiyo mapato yake anayotarajia kulipa lile deni, basi Mahakama itatumia busara yake ili maamuzi yake yahusishe na kuharibika kwa mazao ya mkopaji. Kamati iliipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa sababu wananchi wakiwa makini na wakielimishwa watafaidika na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu kuhusu dhana hii mpya ni la msingi. Ni wajibu wetu sote na sisi Wabunge kuwa tayari kuelimisha wananchi wetu juu ya sheria hii. Kamati imeshauri Wizara ichapishe pia sheria hii kwa lugha ya Kiswahili ili wananchi wengi waweze kuisoma na kuelewa vizuri. Elimu ni mchachato na hivyo tuendelee kuelimishana ili tutumie fursa hii vizuri na wananchi wetu waondokane na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika ingawa katika sheria za awali ilikatazwa kuhamisha miliki ya ardhi tupu wala kuiuza kwa mtu mwingine. Jambo hili kwa ukweli limekuwa likifanyika kwa kificho, watu wamekuwa wakiuziana ardhi tupu kwa visingizio vya kuuza msingi au shamba au bustani. Mficho huo umekuwa ukiikosesha Serikali mapato. Hata hivyo kwenye Muswada huu uhamisho wa haki ya miliki ardhi hautakwenda kwa zaidi ya wamiliki watatu kabla haujaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyopo kwenye Muswada huu sasa unayawezesha mabenki ambayo yana fedha nyingi za amana za wananchi kuzikopesha fedha hizo bila kuwa na wasiwasi wa kuzipoteza. Sheria ya Ardhi ipo tangu mwaka 1999 lakini haijatekelezeka kwa vile ilionekana kushindwa kumlinda mkopeshaji na kumlinda zaidi mkopaji na hivyo ikabaki haina maana yoyote kwa walengwa. Mkopaji (mwananchi) na mkopeshaji (mabenki) na pia ubutu wa sera ya ardhi nao ukajionyesha. Ni imani ya Kamati kuwa baada ya kuitunga sheria hii basi ile sera ya ardhi tuliyoipokea humu Bungeni na kuishangilia sana itatekelezwa na *Inshallah* tutaona mabadiliko katika maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake kuhusu hati miliki. Waheshimiwa Wabunge walionyesha wasiwasi wao kuhusu mchachato wa kupata hati miliki kwa

mtu wa kawaida aliyeko Kijijini kwa mfano kule kwangu Msangano au Kapee. Tumefurahi kuambiwa kuwa sasa na huko Vijijini kutakuwa na hati zitakazotolewa na Serikali za Vijiji kwa ardhi inayomilikiwa kimila na ambazo nakala zake zitatumizwa kwenye masjala ya ardhi ya Kijiji na hizo nazo zitatumizwa kisheria kuwa ni hati halali na hivyo mwananchi anaweza kuitumia kwa kuomba mkopo benki. Tulielezwa kuwa masjala hizo za majaribio moja ipo Wilaya ya Mbozi na nyingine ipo Mkoa wa Iringa. Kamati inashauri kwamba pamoja na kuwa zoezi hili litakuwa na gharama kubwa watendaji wa Wizara wahakikishe kuwa wanajiweka muda maalum wa kutathmini mwenendo na utekelezaji wa sheria hii ili iwe na faida kwa watu wengi. Zoezi hili liende sambamba na kuhakikisha kuwa mchachato wa upimaji wa ardhi za Vijiji kwa nchi nzima linaendelea na kukamilika.

Kamati imezingatia ukweli kwamba riba za ukopaji kwenye mabanki yetu ni kubwa, ni matumaini yetu kuwa riba itaendelea kupungua kutokana na mabanki mengi na taasisi za kifedha kujiingiza kwenye biashara hii. Ni wito wa Kamati hii pia kuziomba taasisi za kifedha na mabanki kufikiria upya riba hizo ili kuchangia katika kupiga vita umaskini kwa wananchi wetu. Serikali inashauriwa pia kuweka utaratibu utakaoziwezesha taasisi hizo kufanya jukumu hilo la kupunguza riba ili kuchangia maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo kwa manufaa ya sheria hii na wadau hasa walengwa:-

- (a) Wakopeshaji (mabanki) yawe na wataalam ambao wanaweza kuandikia miradi au *write-ups* wateja wao kwa ajili ya mradi mmoja na hata miradi ambayo imeandikwa ili wakopaji wasianzishe miradi isiyokuwa na faida.
- (b) Halmashauri zetu za Wilaya na Miji ziwe na wataalam wa kuandika miradi ili kuwasaidia wananchi walio kwenye maeneo yao kufaidika na miradi wanayoiwaza wao wenyewe wananchi.
- (c) Inabidi Serikali iunde au iimarisha chombo cha usuluhishi wa migogoro ya ardhi kwa vile baada ya watu kuona kuwa wanaweza kupata mikopo kwa kutumia kipande cha ardhi tabia ya kunyang'anyana itaweza kuzuka.
- (d) Ni vema mabanki yetu yakishakubali kukopesha basi yasitoe fedha zote kwa mkupuo bali watoe hatua kwa hatua kutokana na mahitaji na mwenendo wa mradi huo na kwa maana hiyo mabanki yatatambua mapema ni kwa nini mteja fulani ameshindwa kulipa deni lake kwa wakati na kuweza kumshauri ipasavyo.
- (e) Kwa vile sheria hii vile vile inahusisha wananchi ni vema na kwa haraka sana sheria hii na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1975 zitafsihiwa kwa lugha ya Kiswahili.
- (f) Ufanisi wa sheria hii hautaonekana iwapo sheria zingine kama vile Sheria za Mwenendo wa Mashauri ya Madai ya Mwaka 1966 (*Civil Procedure Code Act, 1966*) pamoja na *Temporary Injunctions* hazitafanyiwa marekebisho.
- (g) Kabla sheria hii kuanza kutumika itolewe elimu ya kutosha juu ya dhana hii mpya. Serikali ihakikishe kwamba kila mwananchi anapata hati miliki ya eneo lake ili kuondoa migogoro ya ardhi lakini pia hati miliki ndiyo itakayomwezesha mtu kupata mkopo, bila hati miliki ni vigumu benki kutoa mkopo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kukushukuru tena wewe mwenyewe binafsi, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wadau wote walioshiriki katika kuuboresha Muswada wetu huu. Nawashukuru wajumbe wa Kamati yangu wote kwa jinsi walivyoshiriki katika suala zima la kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa niaba ya Kamati nzima na naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MHE. ALI SAID SALIM - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii

kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa uwezo wake katujalia wote kufika asubuhi hii tukiwa katika hali ya afya njema.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na kukupongeza pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kumaliza vizuri mwaka wa 2003 na kuingia kwa nguvu mpya kwenye mwaka huu wa 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi nzima ya Upinzani na wananchi wote wa Tanzania tuliona mapungufu makubwa kwenye marekebisho ya Muswada huu wa Ardhi. Naomba kuainisha mapungufu hayo kama tulivyobaini.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 37(4) mpaka (5) kuhusiana na uuzaji wa ardhi tupu au isiyoendelezwa. Kwanza, kwa hali ya kawaida katika nchi yetu hakuna ardhi tupu, kama ilivyoitwa katika sheria hii. Kwa kuwa nchi yetu ni ya wakulima na wafugaji na kwa makabila makubwa ya wafugaji ni watu wa kuhamahama pamoja na mifugo yao. Sasa hiyo ardhi wanayoiita tupu isiyoendelezwa ikiuzwa malisho ya wafugaji yatakuwa wapi?

Mheshimiwa Spika, naona sasa nchi yetu inataka kuingizwa kwenye janga la vita mbaya kati ya wafugaji na yeyote yule atakayechukua ardhi kwa kisingizio cha ardhi isiyoendelezwa. Nadhani Waheshimiwa Wabunge bado tuna kumbukumbu ya mauaji yaliyotokea Kilosa. Kwa hili namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kulifikiria na kuliona, yatakayotokea yeye na sisi tunaopitisha sheria hizi ndiyo tutakaolaumiwa na ulimwengu mzima pamoja na Watanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 112 cha nyongeza tafsiri ya neno *matrimonial home* na tafsiri yake iwe kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Ndoa Namba 5 ya Mwaka 1971. Hili nashukuru Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake aliweza kuifafanua. Kwa tafsiri hii tunaona bado watafiti wamesahau kuwa kuna neno linaitwa *Polygamous marriages* na kwa njia hii mwanamke yule tu ambaye kwa muda huo atakuwa karibu na mume wake ndiye atakayetambulika na mkopeshaji lakini wote wengine wanaweza kuwa hawana taarifa na chochote kuhusu mume wao pamoja na mke mdogo kuweka rehani ardhi ya familia. Hivyo basi sheria hii kama itapita itakuwa imewanyima haki ya umiliki wa ardhi nao kama wake halali ndani ya Sheria Na. 5 ya Mwaka 1971. Madhara yanayoweza kutokea yataikumba familia nzima yaani wake zake wote hata kama ni kumi kwani ndoa za kijadi na kimila hazina idadi ni wake wangapi wawe mwisho kwa mwanaume mmoja. Lakini cha msingi ni wanandoa wote kuridhia wakati wanatambua kuwa familia imeweka rehani ardhi au sehemu ya ardhi yao na wote wawe tayari kwa lolote litakalotokea kwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24(1) cha Muswada huu kinachosema kuwa kama mkopaji atashindwa kuiendeleza ardhi hiyo au atashindwa kulipia baadhi ya kodi kama ilivyotakiwa basi mkopeshaji bila kutoa taarifa kwa mkopaji atalipia gharama zote kama sheria zingine zinavyoelekeza na baadaye kuongeza gharama zote alizotumia bila kumweleza au kumtaarifa mkopaji thamani halisi ya mkopo kwa njia hiyo kuongeza deni analodai.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hii mkopeshaji kwa kutambua ubora wa thamani ya ardhi, ni rahisi kwake kumnyang'anya mwananchi ardhi yake kwa njia hii ya kupandisha thamani ya mkopo bila kushauriana na mkopaji. Hivyo Kambi ya Upinzani inashauri kifungu hiki cha sheria kiangaliwe upya kwani kinaweza kuchukua haki za wale wote wenye uwezo mdogo kiuchumi na kumpa mkopeshaji haki zao.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 127(2c) kinachohusu utoaji wa ilani kipindi cha siku 30 kama ilivyoonyeshwa kwenye Muswada huu kwa mkopaji kulipa deni au kuuzwa kwa ardhi yake ni kifupi mno kwa kuzingatia mazingira na hali halisi ya mawasiliano ya kutuma na kupokea barua katika nchi yetu. Kwa kuangalia mantiki hii tu, Waheshimiwa Wabunge nadhani Muswada huu ni maalum kwa watu wachache wenye uwezo na sio wale Watanzania wengi wanaoishi katika Wilaya ambazo hata baada ya kipindi cha zaidi ya miaka 40 ya Uhuru wa Tanzania bado hazina hata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa wayaangalie vizuri haya yaliyomo ndani ya Muswada huu. Kambi ya Upinzani na wadau husika tunaona kipindi cha miezi mitatu kinaweza kuwa muafaka katika utoaji na upokeaji wa ilani kwa pande husika. Hivyo tunaomba kipengele hicho kirekebishwe ili kuondoa ugomvi na dhuluma inayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 128 kinachompa mkopeshaji kutumia ardhi iliyowekwa rehani kwa nia ya kulipa deni ikiwa atakuwa amekamilisha taratibu za kutoa ilani au kwa amri ya Mahakama, Kambi ya Upinzani inaona na kuishauri Wizara husika kwamba mkopeshaji hatakiwi kujichukulia au kuwa na uwezo wa kuitwaa ardhi licha ya ilani, Mahakama ya Ardhi ndiyo inatakiwa kuwa chombo pekee kinachoweza kutoa haki baina ya pande zote husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 130(1e) kinachompa uwezo mkopeshaji kuchukua umiliki wa ardhi iliyowekwa rehani na mkopaji, kwa mantiki hiyo basi mkopeshaji ana uwezo wa kuiweka rehani ardhi hiyo kwa mtu au chombo chochote bila kufikiria kuwa ardhi aliyoipora ilikuwa imeshafikia thamani gani kwani *land always appreciates not depreciates* yaani siku zote ardhi inapanda thamani na haishuki thamani. Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo kwa *valuers* wa Serikali ili kuangalia thamani halisi ya ardhi kabla na baada ili kama mkopaji atashindwa kulipa, mkopeshaji achukue kile ambacho ni haki yake tu kulingana na muda husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona ni mapema mno kuipitisha sheria hii kama wadau wengi walivyopendekeza. Kwanza, elimu itolewe kwa wananchi wote ili waelewe vizuri athari zinazoweza kuwapata kutokana na kushindwa kurejesha mikopo waliyochukua kwenye mabanki. Kwa njia hii wananchi wasifikiri kuwa ni fedha za Serikali kama ilivyokwishatokea huko nyuma mfano kufilisika kwa Benki ya Nyumba (*Tanzania Housing Bank - THB*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza siku hii ya leo lakini pia nitumie nafasi hii ya kumpongeza mwenzetu Ndugu Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuingia katika Bunge letu hili. Lakini pia niwapongeze wenzetu waliochaguliwa katika Bunge la Afrika kwa sababu tuna imani watatuwakilisha vizuri sana huko mbele ya safari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ambayo imejadili kwa undani Muswada huu. Nadhani amesema mengi ambayo mengine nitaongezea tu ili kuweka uzito katika masuala ambayo amezungumza Mheshimiwa Simpasa. Napenda niwashukuru wamefanya kazi nzuri kwa niaba ya sisi Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nizungumze masuala matatu ambayo mengine ni ushauri tu. Kwanza, napenda nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Ardhi, kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa katika kutuletea Muswada huu ambao ni muhimu katika maendeleo hasa ya wakulima wetu Vijijini. Nalisema hilo kwa sababu ardhi ni msingi wa maendeleo ya watu wetu, tunaanzia hapo. Karne hii ya ishirini na moja ni karne ya ushindani na itatawaliwa na wenye uwezo na ustadi wa namna ya kuweza kutafuta maendeleo yao wao wenyewe. Hapa ndipo nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba wataandaa utaratibu mzima wa kuanza kuwafundisha wakulima wetu wajue utaratibu wa kupata mikopo. Wajue namna ya kuandaa mipango ya miradi ya mikopo, lakini pia kuwapa mbinu ambazo wajanja wanaweza kuzitumia kunyang'anya ardhi yao na wakaitumia hiyo ardhi kwa faida yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, hili nalisema kwa sababu dira ya maendeleo ya mwaka 2025 inatamka wazi ya kwamba Taifa letu tukitaka liendelee lazima tuandae namna ya kuwasaidia wakulima Vijijini ili waondokane na umaskini uliokithiri katika maeneo yao na ardhi kwa sababu ndiyo msingi wenyewe. Hivyo Serikali lazima iandae utaratibu wa kuhakikisha kwamba ardhi kweli inakuwa na manufaa kwa maendeleo yao. Mimi napenda kushukuru kwa sababu bila kuwaandalia utaratibu huu ambao Mheshimiwa Waziri ameusema tutapata matatizo makubwa sana. Lakini sera yetu ambayo tuliipitisha mwaka 1995

wote ni mashahidi ilizungumzia yafuatayo: “Nia ya Sera ilikuwa ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila raia awe na haki sawa ya kupata ardhi”.

Mheshimiwa Spika, nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu walinifurahisha wenzetu wa *Gender Land Task Force* walioleta makabrasha, wote mlifahamu, nadhani wengi tulipewa, wamejaribu kutoa ushauri na maoni yao. Mimi napenda kuwapongeza kwa sababu utaratibu huu lazima tuimarisha uendelee na wenyewe wawe ni chachu ya kuleta ushauri ndani ya Bunge hili na kila Mtanzania mahali popote kwa kweli kama ana kitu chochote, ni vizuri akatumia utaratibu wa aina yoyote ili kuhakikisha Waheshimiwa Wabunge wanaelewa nini kero ya wananchi na wananchi wanalalamika nini. Huu utaratibu nadhani ukiendelea utatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri amejaribu kufafanua, tunalotakiwa pale ni kufafanua baadhi ya maeneo ambayo tunadhani wanataka yaeleweke. Mimi nalisema hilo kwa sababu bila kuelewa tutaendelea na matatizo ya kutojua tunafanya nini.

Mheshimiwa Spika, sasa sera inahakikisha kuwa miliki ya ardhi za kimila pia zitatambulika na kuhakikisha kwamba zinalindwa kisheria, lakini sera pia imeweka kikomo cha eneo la ardhi linaloweza kumilikiwa na mtu mmoja ili kuepusha watu kujilimbikizia ardhi au kuwa na ardhi kubwa kuliko uwezo wa kuiendeleza ardhi hiyo. Nalisema hilo kwa sababu mtindo ambao tunadhani unaanza kujitokeza hivi sasa ni wale wajanja wachache baada ya kujua sasa wanaweza kutumia ardhi kupata mikopo mikubwa watakimbia kwenda kung’ang’ania na kuchukua maeneo makubwa sana ya ardhi na wachukue mikopo na mikopo hiyo bahati mbaya inaweza kutumika kwa mambo mengine.

Kwa mfano, kuna baadhi ya watu ambao nawafahamu wamekwenda kuvamia baadhi ya maeneo, wamechukua ekari 2,000, 3,000 mpaka 6,000 na baadhi yao wamepata mikopo ya benki lakini hata senti tano haikuingia kwenye shamba. Wamefanyia kazi nyingine, wametumia ardhi kwa kupata mikopo lakini kazi iliyofanyika si kwa ajili ya shamba. Sasa Mheshimiwa Waziri ni vizuri tukawa waangalifu kwa sababu wapo wajanja ndani ya nchi hii wataendelea kutumia utaratibu huo na wenzetu wanaotoa mikopo wakati mwingine wanakuwa na matatizo ya rushwa. Tatizo la rushwa tusipoliangalia wataendelea kutumia fedha hizi ambazo zingesaidia kuinua hali ya uchumi wa wananchi wetu Vijijini wakaendelea kutumia kwa kazi nyingine ambayo ni tofauti na ilivyokusudiwa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia suala la thamani ya ardhi liangaliwe upya kwa sababu ardhi usipoiwekea thamani ambayo inajulikana basi wajanja ambao watakuwa wanatoa mikopo wanaweza kutumia hesabu yoyote wanayotaka wao wenyewe. Hii biashara itakuwa sasa ni nani anayejulikana na huyo anayekwenda kufanya hiyo kazi, kama mnaelewana au mnapeana chochote ataoa thamani kubwa kwenye ardhi yako tofauti na mwenzako. Sasa wakati mwingine ni vizuri tukawa waangalifu tuwe na utaratibu na mtandao utakaokuwa wazi kabisa kila mmoja ajue ya kwamba ardhi inapotolewa thamani isiwe ya upendeleo. Fulani thamani yake ni kubwa kuliko mtu fulani. Ndiyo maana wakati mwingine wananchi wanalalamika kwamba mimi wamethaminisha ardhi yangu kwa hela ndogo ukilinganisha na fulani. Labda mwenzetu alitoa chochote ndiyo akapewa thamani kubwa. Sasa ni vizuri hilo likaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika hilo najua tutakuwa na matatizo kwa sababu ya upungufu wa baadhi ya watumishi wa Wizara yako. Hawatakuwa na uwezo kukidhi mahitaji haya ambayo sasa yataanza kufumuka kila kona ya nchi hii na wapimaji binafsi gharama zao tunazifahamu, ni kubwa sana. Wana bei kubwa sana kiasi kwamba mkulima wa kawaida hawezi kumudu kuwachukua wapimaji binafsi.

Sasa nilikuwa nashauri tuandae kautaratibu katakaowasaidia kwa kushirikiana wapimaji binafsi na wa Serikali ili kuhakikisha kwamba kuna haki inatendeka. Pia utaratibu ambao huwawezesha hata wenzetu ambao uwezo wao ni mdogo wakaweza kupimiwa maeneo yao na wakapata haki ya kupata mikopo kama utaratibu utakavyokuwa umeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, pia ningeshauri Wizara kuanzia sasa kama inawezekana, ione umuhimu wa kuendelea kuwafundisha watumishi wengi zaidi. Watumishi hao tunahitaji watusaidie kwa sababu wimbi hili ambalo tunalisema la wapimaji na wimbi hili la watu watakaokuwa wanasaidia kutoa thamani ya

maeneo ni vizuri likawa na ushirikiano wa pande zote mbili na pande zote mbili zinaweza kuwa ni *fair* kwa sababu watumishi wa Wizara watakuwa na miongozo ambayo itakuwa inasimamia utaratibu mzima.

Sasa ni vizuri wakiwa karibu sana na hawa watu binafsi ambao watakuwa wanaanza kujitokeza kufanya hiyo kazi. Najua Wizara ina matatizo ya fedha lakini pia najua Wizara inaweza kuandaa *program* maalum ya kuhakikisha kwamba hao watu wanaandaliwa bila kuwa na gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tumeweka vigezo vya kuthamini ardhi. Vigezo vya kuthamini ardhi ni vizuri vikawa wazi kwa kila mtu akajua isiwe ni siri ya Wizara au ni siri ya watu binafsi ambao watakuwa wanafanya kazi hiyo.

Vigezo vinajulikana wakati mwingine vinaweza kuwa ni kutokana na ubora wa eneo fulani na jinsi watu wanavyokimbilia eneo hilo, ndiyo vigezo viweze kutumika. Lakini wakati mwingine mimi nadhani tuangalie pia haya maeneo ambayo watu watakuwa wanakimbilia yanakuwa na faida gani kwa Taifa. Je, yataingiza kiasi gani cha faida ukilinganisha na maeneo mengine? Vigezo hivi lazima viwe wazi kila mmoja avijue na kama inawezekana visambazwe na sisi Waheshimiwa Wabunge tupewe nakala ya vigezo vitakavyotumika katika kuthamini maeneo mbalimbali. Ili na sisi tukasaidie kuwaeleza wananchi katika maeneo yetu ili wajue utaratibu utakaokuwa unatumika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuomba kwamba sheria yoyote inapotungwa huwa inatungwa kwa manufaa ya wananchi wenyewe, na manufaa yenyewe hayo yatajulikana tu, iwapo sasa wananchi watapata nafasi ya kuelezwa kwa undani shabaha, madhumuni na faida ya sheria hiyo ambayo itakuwa imetungwa. Nina imani kwamba utaratibu huu ambao Mheshimiwa Waziri amesema atatoa elimu sehemu mbalimbali, utakuwa ndiyo chimbuko la wananchi kuhakikisha haki inatendeka na wao wanashirikishwa kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono kwa dhati Muswada huu, na ninamwomba Mheshimiwa Waziri simamie kwa undani ili tuweze kufanikiwa katika kazi yetu. (*Makofi*)

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kueleza machache niliyonayo.

Mheshimiwa Spika, napenda awali kabisa niunge mkono Muswada huu. Na nina machache nitakayoyasema ambayo yanania tu wasiwasi inawezekana pengine haupo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri, lakini haujatatia tatizo tulilionalo hapa nchini. Tuna wafugaji, inasemekana eneo la mfugaji pengine linaweza likawekwa rehani. Lakini sasa ardhi na hati miliki tuliyonayo hii ambayo bado *transparency* haijachukua hatua yake ya kuwezesha watu waogope kuingilia maeneo ya watu itatuletea matatizo. Ni vizuri elimu ipite watu wajue kwamba eneo lililo na hati miliki mwenzio, wewe huna nafasi ya kuingilia, watu walijue hilo kabisa. Lakini kwa tabia ya watu wetu hili litatuchukulia muda sana ili waweze kulikubali. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri afanye hilo kwa kueneza elimu kwa wananchi hawa wakulima wa vijijini waelewa hilo ili waweze kulitii na kulizingatia.

Vilevile ni vizuri wafugaji wakajua haki ya ardhi yao. Kule Shinyanga wana ngitili. Sasa ngitili ingekuwa ina sheria yake ya kudhibiti maana hata ukitenga eneo lako la kufugia unaweza kuwa na hati, lakini kama huwezi ukapanda majani ya kisasa, huwezi ukalimiliki kama unavyotarajia lina matatizo, nimeishi huko nimeona. Ukishaweka ngitili basi kila mtu mwenye mifugo wakati wa shida ya nyasi ni kupeleka katika sehemu ile. Hili litatuletea ardhi hii ya ufugaji kutupa matatizo makubwa kabisa. Ni vizuri tukaliangalia ili kupunguza kelele na vurugu inayoweza ikatutokea.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tatizo tulilionalo wakulima wana maeneo yao na wafugaji katika maeneo mengi hasa kule kwetu Mbozi ambako maeneo ya ufugaji si makubwa kwa kweli wafugaji hawana maeneo, wanabaki tu kuswaga ng'ombe karibu na mashamba na kulindalinda. Sasa kwa kuwa tuna tabia hii italetu matatizo kwa mtu kulitunza eneo lake likaweza kuwa na msingi wa kukua kibiashara na kuuzika.



Mheshimiwa Spika, suala lingine kuna wenzetu waliobahatisha wameshika mashamba makubwa sasa hawa tunawafanyaje? Ni vizuri tukakaa wale walioshika mashamba makubwa na wana hati na hawayatumii kwa kweli turekebishe. Turekebishe haya mashamba wasiyaweke kwa nia ya kuyauza. Hili ni vizuri tuliangalie lisije likatuletea matatizo.

Lingine hati hii inazungumza juu ya ardhi ambayo pengine mtu amejenga nyumba au shamba. Lakini tunasema wanandoa tumeona matatizo ya vijijini, watoto wana matatizo sana wale wenye umri wa kulelewa na wengine wanapokuwa shuleni tu wanaondolewa kwa sababu ardhi baba kauza, kanywea pombe, kaa mke wa pili na wa tatu, watoto hawana cha kutumia wala hawana sehemu ya kuzalisha na haya ndiyo matatizo ambayo kwa kweli sasa hivi kama sheria hii haitafuatiwa kwa upesi kuangalia namna ya Mahakama zetu ili ziweze kufuata utaratibu tutapata matatizo. Kuna watoto baba yao akifariki wanafukuzwa kwenye eneo hilo na hili nadhani kama mtu anataka auze eneo au aliweke rehani, ni vizuri hata familia yote ya watoto pale wakubali na walielewe hilo kuliko kuliuzwa tu hivi hivi bila utaratibu hatutaweza kufanikisha ardhi hii na bado tutaleta makelele na matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika, hili la kuweka tabia ya sheria 71 ile inatambua mke hata bila kuoana kikamilifu mradi mmeishi tu miaka 2 au 3 ni mke. Sasa hii imekuwa ni tabia ya miaka mingi tuliyonayo. Sasa hii itatuletea matatizo nadhani ni vizuri tuiangalie tena hapa. Nyingi sana ya ndoa hizi tunaziendesha kwa kuficha ficha. Sasa na bahati nzuri sheria ile haikuangaliwa zaidi kwamba hata mama naye anaweza kushika ungoni kwa mama ambaye si halali hajatambulika. Labda ni vizuri tuweke utaratibu ueleweke, mama mwanandoa kwa sheria ile kwa kweli tulichunguze vizuri litatuletea shida na maneno mengi na matatizo mengi zaidi tuliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kusema kwamba benki ikopeshe mtu aliye na ardhi aweke rehani. Mimi nadhani tungekuwa na msisitizo kwamba ardhi isiuzwe hivi hivi mpaka mtu awe ameandika *write up* ambayo inaonyesha atatumia kwa kitu gani huo mkopo na benki iwe na wajibu wa kufuatilia kuona kweli zile fedha alizokopa zinaendelea ile ardhi. Kama hana *write up* tutapata matatizo. Niliona wakati ule niko kule Kahama kama Mkuu wa Wilaya, sasa wengi walikuwa ndugu zangu hawa Wasukuma wanakopa fedha ya pamba anakaa, baada ya kuza pamba anahamia Kibondo. Sasa na hii tunayoruhusu watu waende popote tu, nikishaona matatizo hapa nauza hapa nakwenda Mtwara nitapata ardhi nyingine. Maana hakuna utaratibu na uzito unaoonyeshwa hapa. Nitakaa kule nikichoka nauza nakuja sasa Rufiji naingia kwenye umwagiliaji na watu wanabadili majina. Kwa hiyo hili nalo litatuletea matatizo. Ni vizuri kuwe na ufuatiliaji wa ndani kabisa na wa kuona kuwa watu hawavurugi utaratibu ambao tumeutengeneza.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa ninaomba hasa kule kwetu Mbozi kuna watu wamefanya kazi hii ya kuweka rehani, na kuna maneno wanasema kukata vichwa kahawa wamechukua mashamba ya watu na hawajayaendelea kwa kudanganya danganya hivi hivi, na tusipoangalia sasa hii itakuwa ndiyo msingi wa watu kufanya hivyo. Wajanja watajipatia ardhi. Sasa tukubaliane kila mtu aonyeshe ardhi yake na madaraka haya tuwape vijiji vihakikishe kila mtu ana eneo analolima kwanza kwa chakula chake na kwa biashara yake. Lakini hii ya kutazamana hivi kusema sijui biashara, Wamachinga hawa hatwendi mbali hata kidogo. Lazima tushikane kwa nguvu zote, nadhani sasa ndiyo wakati ule wa sheria ile ya nguvukazi kama ingeingizwa hapa nayo ingetusaidia kusukuma utunzaji wa ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tuweke utaratibu kwamba ardhi aliyopewa mtu aitunze akionekana haitunzwi anyang'anywe kuwe na ufuatiliaji. Watu wengine ardhi wanaikwangua tu, wanaichoma moto na wanaifyeka. Sasa ardhi ya namna hii haitakuwa ardhi na tutafilisi na tumeona maeneo mengine. Nimeona hata sehemu nyingi kama kule Kibaigwa maeneo yale kwa kweli yamekwishafilisika na hali ya uzalishaji mzuri, na ndiyo watu wanaikwangua tu na wanaichoma moto, wanachimba mashimo watumbukiza mbegu basi, hakuna rutuba hata kidogo katika maeneo yale. Sasa nchi hii tunaiua namna hiyo. Atakayepewa eneo alitunze na alime mazingira ya eneo hilo na vilevile ahakikishe anatomia mbolea na kuwe na ukaguzi wa mazingira haya. Nadhani itatusaidia na tunaweza kuwa na maendeleo ya kilimo chetu na ardhi yetu ikatunzika kama tunavyotegemea. (*Makofi?Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache ya kushauri. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo ndiyo tunafikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha kikao cha leo.

### **MATOKEO YA UCHAGUZI WA SADC PARLIAMENTARY FORUM**

Nimeshakupata matokeo ya kura zilizopigwa asubuhi hii na sasa ningependa kuyatangaza. Idadi ya wapiga kura waliokuwemo ndani ya ukumbi wa Bunge kipindi hicho ni 229 hakuna kura hata moja iliyoharibika. Hatua ya kwanza ni kutangaza kila mgombea amepata kura ngapi. Halafu ya pili, ndiyo kutangaza mshindi. Kama mtakavyokumbuka kulikuwa na wagombea wawili.

Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya amepata kura 39. Mheshimiwa Sophia Simba amepata kura 190. Kwa hiyo, namtangaza Mheshimiwa Sophia Simba, kwamba amechaguliwa kwenda kutuwakilisha kwenye *SADC Parliamentary Forum*. Ngoja tumalize shughuli za Bunge kwanza. Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.45 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi napenda nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pamoja na wataalamu wake wote kwa kuweza kuleta Muswada huu wa nyongeza katika Muswada mkubwa wa ardhi ambao tuliupitisha.

Ninachotaka kusema katika Muswada huu kwa kweli kwa upande mmoja ni ukombozi katika nchi yetu. Ni ukombozi kabisa kwa sababu kwa muda mrefu sana ardhi yetu haikuwa na thamani. Sasa tunapoingia katika soko huria na soko la ushindani na kuthaminisha ardhi yetu kuwa na thamani kwa watu wetu sasa ndio tumepata mtaji mkubwa sana. Tunashukuru sana Wizara pamoja na Serikali kwa kuweza kuthaminisha ardhi ambayo kwa muda mrefu tuliona kwamba ni kitu ambacho hakina maana wala hakina thamani ya haina yoyote.

Kwa hiyo, Muswada huu ukipitishwa na kuwa sheria na tukiitumia vizuri itatusaidia sana watu wanyonge ambao wako vijijini na madaraka ambayo tunawapa kutegemeana na ardhi ambayo tumegawanya itawasaidia sana.

Lakini jambo moja ambalo naliomba sana Serikali katika hizi hati ambazo zinatolewa bado kabisa wananchi wetu hawajaelewa watapataje hati hizo. Kwa hiyo, kutojua Muswada uko mbele zaidi na watakatutumia hati hizi ni watu ambao ni waelewa kuliko wanavijiji na ardhi kubwa imemilikiwa na wanavijiji.

Kwa hiyo, kwa Muswada huu sasa wajanja wanaweza wakaitumia nafasi yao kuweza kuwagandamiza wanyonge. Hiyo ndiyo hofu yangu niliyonayo mimi kwamba kama unaweza ukapata hati ukaweka rehani, ukapata mikopo na wanavijiji wetu bado hawajaelewa suala hili vizuri itakuwa ni lazima kabisa zifanyike jitihada za makusudi ili kuweza kuelimisha wananchi waweze kuelewa Muswada huu vizuri sana. Vinginevyo Muswada huu utageuka kuwa janga la wanyonge. Naogopa kabisa.

Kwa hiyo, katika kutoa hati ni lazima sasa tukubali kabisa kwamba vyombo ambavyo madaraka ya kutoa hati kama hati hizi za *customary* au *certificate* ambazo vijiji kama kijiji au taasisi inaweza ikatoa cheti kabisa cha ardhi yake ikathaminiwa na Benki pale pale kwa kweli tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana kwa sababu ndiyo chombo kilichopo karibu na wananchi.

Kwa hiyo, naomba sana ikiishia katika hali hiyo na vile vile kupata hati kwa nini isiwe kabisa ni sawa sawa kama mlivyopima vile viwanja 25,000. Unakwenda mara moja umekaa masaa mawili au matatu unapata hati yako, kuliko huu mlolongo kabisa ambao uondoke uende Wilayani, unaondoka unatoka

Wilayani unakwenda Mkoani yaani unahangaika. Kwa hiyo, tengenezeni utaratibu wa namna ya kupata hizi hati isiwe ni usumbufu mkubwa kwa wanakijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hofu yangu kubwa na ndiyo iliyonifanya niombe nafasi katika Muswada huu. La kwanza ardhi yetu hii tumeigawanya gawanya. Kuna mahali ambapo umesema. Sisi kwetu sehemu za wafugaji ardhi yote sasa hivi imejaa. Maana yake unaweza ukaona mbuga ukafiri kwamba hiyo ardhi haina watu. Ndiyo tatizo moja maana yake mpaka uone shamba ndio useme kwamba ardhi hii ina watu.

Katika maeneo ya wafugaji ukiona vichaka au misitu ni maeneo ya ufugaji ya malisho. Kwa sababu ninyi mnasema ardhi hiyo ni tupu kwa kweli katika maeneo ya wafugaji ardhi hiyo ukiigusa ni matatizo kabisa. Maana yake kuna watu wanafikiri kwamba wakija Kiteto wakiangalia, wakiondoka kutoka Kibaya kwenda Orkesmet anafikiri kwamba anakata mbuga, hamna kitu chochote mpaka Orkesmet na Profesa Mark Mwandosya, anafahamu amepita yeye na wengine pia. Anafikiri kwamba ni msitu kumbe ni maeneo kabisa ya ufugaji na ndiyo malisho ya mifugo yetu.

Wengine wanafikia kusema kwamba hapa sasa tunajaribu kwenda pale kujaribu kupata mashamba. Lakini sio hivyo tu katika maeneo ya wakulima vile vile Morogoro mpaka sehemu za Usukumani huu Muswada unaweza ukawafanya wasifuge. Ardhi hiyo sasa nao wataikatakata wataiuza bila kujali mifugo wataweka wapi.

Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali iangalie kwa makini katika suala hili kwanza tupate matumizi bora ya ardhi, tupange mpango wetu wa ardhi mifugo ipate sehemu yake, wakulima wapate sehemu yao na wakatekate. (*Makofi*)

Vile vile la mwisho suala la kuuza ni rahisi sana. Sasa tunasema kwamba unaweza ukauza ardhi lakini kuwe na kianzio basi. Maana yake mkulima sasa hivi na mtu yoyote ambaye yuko namna hii watu wanaweza wakanunua ardhi ovyo ovyo bila wananchi kufaidika angalau katika sehemu ukitaka kuuza ardhi eka moja ijulikane kabisa Kitaifa kwamba sio chini ya thamani hii ili kila mwananchi aelewe hata kama atapandisha inategemea ardhi hiyo iko mahali gani. Lakini lazima sasa tuweke ardhi yetu katika *grade. Off course* kwa kweli ardhi iliyoko karibu na barabara ina gharama kubwa au iko juu zaidi kwa sababu ya usafirishaji kuliko ardhi ambayo iko ndani ya pori itabidi ukate barabara na kadhalika inategemea. Ardhi ambayo ina rutuba labda kule kwa Profesa Mark Mwandosya ambayo ina milima milima na thamani zaidi kuliko karibu na ardhi ambayo ni ya jangwa ya Kiteto au pale Arusha na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima kuwepo mkatekate ardhi kwamba hii ardhi ina thamani kiasi gani na inategemea itakavyokuwepo. Hatujui suala la chini kwa almasi kwa Wasukuma kwa sababu nao ni ardhi lakini ukishaingia nusu nchi ambayo sio yako tena inabaki ni ya kwetu. Kwa hiyo, hii ya juu juu tuielewe.

Mimi nilitaka niseme kwamba ardhi ya wafugaji na niseme hivyo na wengi watachangia kwamba iwekwe kabisa bayana isije ikaingilia katika masuala ya kuuza ardhi, wapewe wafugaji ardhi yao kama wako Morogoro, kama wako Kiteto, kama wako Chunya na sehemu popote pale kabla hamjaanza mauzo ya ardhi mfugaji kabisa ameshawekwa pembeni kabisa, la sivyo mkiingilia pale mtazua majanga mengine ambayo ninyi wenyewe mmeyatafuta. Nasema hivyo kwa sababu ninaiona hali itakavyokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nazidi kuwashukuru sana Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa jitihada zao hasa pamoja na hayo yote kwa kumalizia na hivi viwanja ambavyo mmevipima kupanua miji yetu kwa kweli imeleta matumaini makubwa kwamba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi sasa inataka kupima sehemu za makazi ili miji isioteote ovyo, kwa kweli itakuwa imetusaidia sana. Lakini waende katika miji mingine kwa kupima viwanja pamoja na vijiji. Kwa sababu sasa hivi vijiji vinaweza kuunganika yaani tunatengeneza vijiji, vinaunganika maili mbili au tatu wakifuata barabara tu mpaka mwisho ndiyo tatizo tulilionalo sasa. Ukienda katika kijiji kimoja inaunganika kwenye barabara nyingine hakuna mtu anayetaka kujenga nyumba nyuma ya mwenzake, ni barabarani tu.

Kwa hiyo, tunaomba hii kazi ambayo mmeanza muifanye kwa makini na tunashukuru sana kwamba huu ndio mwanzo wa kutajirika kwa Watanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii leo mchana na mimi nichangie machache kuhusiana na Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa hiyo, nimeshiriki pamoja na wenzangu kwa kipindi chote kuupitia Muswada huu kuutafakari na kuuchambua pamoja na wadau mbalimbali tangu mwanzo mpaka hivi leo tunauzungumzia. Kwa hiyo, yangu niliyonayo ni machache sana na kwa sehemu kubwa nia ni kuunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na kusema kwamba hivi sasa ninavyozungumza kama wenzangu wengi walivyowahi kusema ni kwamba nchi yetu kwa kweli ina njaa na mimi kule katika jimbo langu wananchi wale wana njaa. Wiki mbili karibu na nusu nimetoka kule hali ilikuwa mbaya. Debe la mahindi ukilipata ni kati ya shilingi 5,000/= na 6,000/=. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuangalia kwa pande zote za nchi yetu kwa sababu tulizoea kwamba kuna maeneo ambayo ni makame mara kwa mara yanakumbwa na njaa lakini safari hii hata yale maeneo ambayo pia hayapatipati shida ya chakula safari hii tumepata matatizo hayo. Kwa hiyo, ningeiomba kwanza ujumbe huo ufike na kule kwangu wakati ukifika wa kusaidia wananchi wale kwa chakula basi wapate msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na wenzangu wote waliozungumzia Muswada huu hasa katika maeneo machache ambayo pia hata mtoa hoja aliweza kuyafafanua. Nakubaliana sana na eneo la kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wetu ili waweze kuelewa Muswada huu hasa maeneo muhimu maeneo ya ukopaji na kuweka rehani ardhi yao, elimu iendelee. Nakubaliana pia kwamba ni vizuri tutakapoipitisha sheria hii na itakapokubaliwa mara moja iweze kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo wananchi walio wengi wanaielewa ili waendelea kujielimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo taarifa kwamba ziko sheria nyingi kadhaa ambazo kama hazikuangalia upya basi zinaweza kuingilia sheria hii na madhumuni ya sheria hii yasiweze yakafanikiwa. Ninaomba zile sheria ambazo zinazuia ufanisi wa sheria hii basi pia ziangaliwe upya haraka iwezekanavyo ili sheria hii iweze kufanya kazi. Kukopa au kukopeshwa ni hiari ya mtu. Muswada huu kwa kweli umeletwa ili utusaidie kwa wananchi wetu kupambana na umaskini kwa ujumla. Ni muda mrefu katika nyumba hii Waheshimiwa Wabunge wote tumezungumzia matatizo ya watu tunaowakilisha, umaskini, umaskini. Wale ambao wanajua biashara na maendeleo ya nyanja mbalimbali wanakuambia kwamba hakuna mtu anayepiga hatua nzuri ya maendeleo katika kilimo na hata katika biashara bila kukopa.

Kwa hiyo, njia hii imeletwa, ni nafuu na mbadala ili wananchi waweze kukopa na walichonacho hasa ni ardhi kwa hiyo utaratibu uliowekwa utawasaidia naamini ukisimamiwa walio wengi ili wakope na waweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu hasa baada ya kukiri kwamba madhumuni ni kuunga mkono, nina eneo moja la kuchangia na eneo hili naomba kwa kweli ufafanuzi wa kina na pengine sio wa Waziri anayehusika tu lakini wa Serikali nzima. Tunajua kwamba nchi yetu ni kubwa na mimi kama Mbunge wa jimbo la Mlalo ni Mbunge wa watu ambao kusema kweli wanakaa vijijini na vijijini mbali kabisa na mji hata ule Mji Mkuu wa Wilaya. Wasi wasi wangu na lile ambalo ningependa nifafanuliwe pamoja na Bunge lako Tukufu na Wabunge wenzangu wanaishi katika maeneo kama haya ya vijijini ambapo ndipo walipo wapiga kura wengi kwamba hivi Muswada huu tukiupitisha na naamini tutaupitisha wale watu walionileta mimi hapa wa Jimbo la Mlalo watafaidikaje na Muswada huu hasa katika eneo la kukopa.

Natoa mashaka yangu hayo kwa sababu Mabenki mengi yanayotoa masharti haya na utaratibu huu wa mikopo yako mijini na yako miji mikubwa. Nakumbuka siku za nyuma wakati wa Benki yetu ile ya NBC tulikuwa na matawi mpaka kule Mlalo. Lakini sera zimebadilika matawi yale yakafa. Pale Wilayani kwetu tulikuwa na Benki chungu nzima. Tulikuwa na Benki ya Maendeleo Vijijini, Benki ya Nyumba sasa hivi hizi Benki hazipo zote zimekimbilia mijini na nyingine hata katika mji wetu mkuu wa Tanga hazipo zipo Dar es Salaam pengine na Arusha.

Je, hivi watu wale ninaowawakilisha wakitaka mkopo huo pamoja na utaratibu wa hati hizo za kimila na hati tunazozijua, hivi wanawezawezaje kupata mkopo kutoka Dar es Salaam au Tanga mjini zaidi ya kilomita 300 kutoka pale walipo, watafaidikaje na sheria hii?

Naomba Serikali itoe ufafanuzi juu ya jambo hili maana nina hakika nikirudi maswali yatakuwa ni hayo kwamba sheria hii tunayoitengeneza inamsaidia nani? Watu wale walionituma mimi hapa watafaidikaje, watapataje msaada?

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisitiza hilo kwa sababu maeneo ambayo Mabenki yalipo sasa hivi ni mbali. Mtu wa kijijini akikopa hela pamoja na hati aliyonayo ya ardhi, shilingi milioni moja au milioni moja na nusu wataalamu wa Benki watoke Dar es Salaam waende mpaka kule walipo pengine hata nusu ya huo mkopo utakuwa umekwisha. Maana yake ni kwamba wale watu ninaowawakilisha wanaishi vijijini kabisa hawatafaidika na sheria hii. Serikali inawaambiaje Watanzania walio wengi wanaoishi vijijini?

Ushauri wangu kama kweli Serikali ina nia ya kuwasaidia wananchi wote wanaopenda kuendelea kwa sheria hii tulisikia nadhani wakati ule wa Bajeti, hivi kweli Serikali ina nia ya kuunda Benki nyingine, Benki ya Wakulima, Benki ya Wafugaji, Benki ambayo itakwenda mpaka kule Wilayani ili iwe rahisi wananchi hawa waweze kukopa wanaotaka au inategemea Mabenki haya ya biashara ya kigeni yaliyoko mijini ndiyo yafanye hiyo kazi.

Ninaamini Mabenki haya hayawezi kufanya hiyo kazi kwa sababu kwanza itakuwa kazi ngumu halafu haitakuwa na faida sana kwao itakuwa na hasara. Mabenki haya yanakimbilia ardhi iliyoko karibuni na wateja wao walioko karibuni ili waweze kupata faida kwa haraka. Naomba Serikali itujibu hayo ili tuweze kupata majibu ya kusema wakati tukiulizwa. Hilo ni jambo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulisema hilo naomba wenzangu wote tusiwe na wasi wasi. Ninajua suala la ardhi ni suala nyeti na ndiyo maana pamoja na vikao vingi na wadau, pamoja na mazungumzo ya mara kwa mara bado wako watu ambao hawajatosheka wanaosema bado Muswada huu uendelee kuahirishwa. Lakini kusema kweli nafikiri tukiendelea kuuahirisha Muswada huu tunaendelea kuahirisha matatizo, hatuendelei kuahirisha utaratibu wa makusudi wa kusaidia watu wetu kutatua matatizo yao. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tukubaliane Muswada huu upite tuanze na nina hakika tukianza matatizo yataweza kujitokeza. Lakini matatizo yakijitokeza basi tutayashughulikia jinsi tunavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niseme tena kwamba nia yangu ni kuunga mkono hoja hii kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati. Tumezungumza sana na tumechambua sana Muswada huu lakini kubwa zaidi nilitaka nipewe majibu ya hilo nililolizungumzia kwamba watu wale wa vijijini watafaidikaje na utaratibu huu na ni Mabenki gani yatakubali kwenda kule pembezoni kabisa mwa nchi yetu ambapo watu wana umaskini mkubwa lakini wana nia ya kupambana na umaskini huo. Pengine Serikali isije ikatubalia kwamba ni vizuri wananchi wajiunge tuanzishe kitu kinachoitwa *Community Bank*.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua watu ambao wameweza kuanza, Dar es Salaam wamefanya, kule Mufindi nasikia wamefanya lakini sio Watanzania wote katika maeneo yote wana uwezo wa kuanzisha Benki hizi. Si Watanzania wote, wengi hawana uwezo wa kufanya hivyo na wengine hata utaalamu wenyewe wa kuanzisha hizi Benki ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Serikali isije ikatupa majibu hayo ambayo tunayafahamu ila itupe majibu kweli ya matumaini ya kwamba Watanzania wote watakaotaka kuitumia sheria hii ikipita basi watakuwa kwenye nafasi ya kuweza kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi naomba wenzangu Waheshimiwa Wabunge wote tukubali kupitisha Muswada huu.

Kwanza Muswada huu tayari imekuwa ni sheria ni maeneo fulani fulani tu ambayo yamechaguliwa ili kuwasaidia wananchi wa Tanzania maskini waweze kushirikiana na watu wa Benki ili kupata mikopo waweze hatimaye kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana tena kwa kunipa nafasi ya leo mchana. Ahsante sana.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote nawatakia kheri ya mwaka mpya wa 2004. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naona leo amebadilisha *position* yake inaelekea sheria hii ina mambo. (*Makofi/Kicheko*)

Nawapongeza sana kwa juhudi ambazo mmezifanya pamoja na wasaidizi wenu wote kwa maandalizi ya Muswada huu ulioko mbele yetu na kwa kusikiliza kilio cha wananchi na kilio cha wenye Mabenki nchini kuhusu mahitajio ya marekebisho ya sheria yetu ya ardhi ya mwaka 1999.

Ndugu zangu hii ndiyo hali halisi ya dunia ya utandawazi kwamba lazima sasa tutoke tulikokuwa kwa sababu ardhi lazima ipewe thamani na iingie katika soko na ili haya yawezekana basi Muswada kama huu unaohusu uuzaji wa hatimiliki ya ardhi na hasa katika eneo hili la maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa kweli ni muhimu.

Pongezi zangu ziko katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza kuhusu msisitizo uliopo humu ndani wa kukataza wageni kumiliki ardhi hiyo peke yao. Lazima kuwe na ubia wa aina fulani na Mtanzania na masharti fulani fulani ya upangishwaji na umilikaji wa ardhi hiyo, hilo ni jambo zuri sana. Lngine zuri katika Muswada huu ni kuhusu mnunuzi kutaka kuiendeleza ardhi ile aliyoigharamia.

Kwa hiyo, inatuhakikishia kwamba haitatoka mkono mmoja kwenda mkono wa pili ikaendelea kutokuendelezwa. Kwa hiyo, kiuchumi tutakuwa tumefaidika kwa namna moja au nyingine kwa maana ya kodi au mapato mengine na uzalishaji wa chakula na mazao mengine au uwekezaji wa aina nyingine yoyote. Lakini pia fursa hii iliyopatikana ya kuwawezesha Watanzania sasa kuuza sehemu ya ardhi yao ambayo haijaendelezwa itawawezesha au itawawezesha Watanzania kupata kipato ambacho kinaweza kutumika katika kuwekeza katika maeneo mengine.

Lakini pili linalofuatia hapo ni umuhimu uliowekwa ndani ya sheria ambao unalinda haki ya wanafamilia kushiriki katika mikataba inayohamisha mali kutoka upande mmoja kwenda upande wa pili. Hii imelindwa vizuri sana ndani ya sheria na ni jambo ambalo ni zuri sana Serikali ingeliangalia mapema.

Mheshimiwa Benedict Losurutia, jirani yangu amezungumzia hapa kwamba unaweza ukatembea katika maeneo ya Kiteto kuelekea Simanjiro kule ukakuta mapori makubwa sana ukadhani zile ni *empty spaces* tu.

Mimi nipitie hapo hapo kwa kweli kuwa si kila maeneo ambayo tunayopita barabarani tunadhani ni machaka tu au ni ardhi zisizoendelezwa. Nyingine ziko pale, nyingine ziko *occupied* na vijiji au na watu wa maeneo yale kwa kufuata *customary law* ile ile ambayo tunaitambua katika sheria hii. Kwa hiyo, tuwe makini sana katika maeneo ya aina hiyo.

Sasa kwa kuwa dhumuni kuu la marekebisho haya ni kuwezesha Mabenki na taasisi nyingine za fedha kutoa mikopo kwa wananchi kwa urahisi na ufanisi kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri. Uzoefu tulionao hapa nchini kwetu kuhusiana na mikopo ya Mabenki ni uzoefu ambao umejaa matatizo mengi kwa sababu ya masharti ya kikiritimba kiasi kwamba ni Watanzania wachache sana ambao watafaidika na fursa ambazo zinalengwa na sheria hii.

Kwa hiyo, nilikuwa natoa wito kwa Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla kuangalia taratibu za Mabenki za masuala ya ukopeshaji na masharti ambayo yanaambatanishwa nayo japo tunasema katika biashara huria hatuwezi kuwaingilia sana lakini tuangalie namna bora ambayo tunaweza tukayabana Mabenki haya yakaweza kutoa mikopo hii ili kutekeleza nia iliyopo ndani ya sheria hii. Vinginevyo itakuwa tumepitisha sheria hii kwa ajili ya wageni wa nje lakini Watanzania watakaofaidika na sheria hii wapo lakini wachache sana na jimboni kwangu sijui kama wanaweza kufika wawili watatu.

Lakini pia sheria hii pamoja na uzuri wake wote niliokwishausema imemlinda sana mkopeshaji katika maeneo kadhaa mpaka inafikia kumruhusu mkopeshaji kujiuzia ardhi japo kwa ruhusa ya Mahakama baada ya mkopaji kushindwa kutimiza masharti fulani fulani. Hili ni eneo ambalo nina wasi wasi nalo kidogo.

Lakini eneo lingine ni lile ambalo Mheshimiwa Waziri umelizungumzia ni kifungu cha 127(c) kuhusiana na mkopeshaji kutoa notisi ya siku 30 na yule mkopaji kama hakuweza kutekeleza basi ardhi ile inaweza ikahama bila ridhaa yake kwenda katika mikono mingine. Tulikuwa tunadhani siku 30 kwa kweli ni kidogo sana tungelirudi kwenye siku 90 tulizozioea kidogo tusingekuwa na wasi wasi sana. Tunazungumzia habari ya ardhi na msisitizo mkubwa katika sheria hii ni suala la hatimiliki.

Mheshimiwa Edson Halinga, asubuhi alitaja maeneo yanayotumiwa kidogo si vizuri sana katika Jimbo langu. Ni kweli. Lakini sababu kubwa ni ile ile kwamba mtu hana hatimiliki na ardhi kipande kile alichokiacha.

Kwa hiyo, uendelezaji wake kwa maana ya kupanda miti, kuboresha virutubisho vya ardhi na kwa maana nyingine namna hiyo inakuwa uangalizi wake si mkubwa sana na sehemu nyingi wanakodishana wanavijiji kwa wanavijiji. Kila mwaka anamkodisha huyu eka kwa elfu mbili, elfu tatu, sasa yule anayekodi analima mazao ambayo ni ya mwaka huo huo tu kama ni mahindi na kadhalika havezi kupanda muhogo au zao la kudumu lingine la miaka miwili, mitatu, minne kwa sababu amekodisha kwa mwaka mmoja tu. Kwa hiyo, inakuwa ni ardhi ambayo haitumiki vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maskini wengi hawataguswa na suala hili kwa sababu ya kipengele hiki cha hakimiliki, kwa sababu ardhi ambayo inakuwa *mortgaged* hapa kwa sheria hii ni lazima tayari iwe inamilikiwa kisheria. Ingawaje wamesema hata *Customary Law* inakubalika, lakini hii sasa ina-vary kabila kwa kabila na mahali na mahali. Ni kitu ambacho kina matatizo mengi sana, inabidi mtuelimishe kweli katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa maoni yangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, ule utaratibu wa utoaji hakimiliki ya ardhi uliopo sasa ambao ukiritimba wake ni lazima tu shughuli hizi zifanyike Dar es Salaam kwa nchi nzima, inabidi ikiwezekana tu-*decentralize* ili wananchi wengi Mikoani sasa waweze ku-*process* hakimiliki ya ardhi na kuipata katika muda mfupi na kwa gharama nafuu, vinginevyo malengo ya Muswada huu yanaweza yasitimizwe kama nilivyokuwa nimesema mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia inahitajika sana kuhakikisha kuwa ina wataalam wa kutosha watakaoshughulika na masuala haya ya upimaji. Iwe ni wale walioajiriwa na Wizara, iwe ni wapima binafsi, lakini ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba watu hawa wanapatikana maeneo mengi na gharama zao zisiwe kubwa sana kupita kiasi ili masuala ya kupima ardhi kwa maana ya mashamba, liwe ni jambo la kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yote haya ni lazima yaendane na kutoa elimu kwa wananchi. Ni rahisi sana wananchi kuweza kupotoshwa na watu wasiotutakia mema kwamba sasa ardhi inauzwa. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iangalie sana suala hili, ikiwezekana sheria kama hizi zitafsiriwe Kiswahili na wananchi wapewe elimu ya namna ambavyo wanaweza kuingia katika fursa hizi wakafaidika badala ya kukaa kulalamika tu kwamba nchi inauzwa, kitu ambacho si kweli hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa hii ilikuwa ikisubiriwa sana na Watanzania wengi ili waweze kuingia katika ubia na Watanzania wenzao wenye mitaji na wageni wenye mitaji, wao mtaji wao ukiwa ni ile ardhi katika shughuli nzima ambayo inatakiwa kufanyika.

Kwa hiyo, ombi langu kubwa lililonifanya nisimame hapa kwa kweli ni kuitaka Wizara kuangalia kwa undani kabisa suala la ukiritimba wa upimaji wa ardhi ili majukumu haya yaende Mikoani na ili wananchi wengi waweze kufaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naomba kukushukuru sana na nasema kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru Wizara kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika maandalizi ya kurekebisha Sheria hii ya Ardhi ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ambayo imejadili Muswada huu toka awali na napenda niipongeze Wizara kwa maandalizi mazuri wakati wa matayarisho na majadiliano na kwa jinsi walivyowahusisha wadau ambao wamehusika kujadili Muswada huu kwa kina. Sisi kama wanakamati tulijifunza na kufaidi na tulielewa ni vipi wadau wanafikiria Muswada huu utakuwa ama wa matatizo ama wa manufaa kwa wananchi wetu na ninawapongeza wadau wote ambao wameshiriki kikamilifu katika kujadili Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu tunaoujadili siyo mpya. Hapa tunajadili tu marekebisho ya sheria ambayo tayari Bunge hili lilikwishapitisha (Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999). Kwa hiyo, yako maeneo machache sana ambayo yanajadiliwa katika mabadiliko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kwamba, chimbuko la mabadiliko haya kwa kweli ni sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mabenki.

Kwanza, sisi kama Wabunge muda mwingi tulikuwa tukilalamika kwamba wananchi wetu hawapati mikopo, mikopo haiwafikii na kwa namna hiyo ilikuwa inaangaliwa ni jinsi gani wanaweza wakapata mikopo hii. Lakini kwa upande mwingine wenzetu wa Benki waliona kwamba sheria hii ambayo ilipitishwa mwaka 1999 iliegemea sana kumsaidia mkopaji badala ya kusaidia wote wawili. Katika sheria ile ya mwaka 1999 ilikuwa inaonekana kwamba mkopaji angelindwa sana yaani hata kama yapo matatizo yametokea ameshindwa kulipa mkopo hakuna uwezekano rahisi wa kuuza ardhi ambayo ameweka dhamana. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo marekebisho haya ya sheria sasa yanaangalia pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tuseme kwamba, hata kabla ya sheria hii kufanyiwa marekebisho watu walikuwa wanaweka dhamana ya ardhi, lakini tofauti ni kuwa walikuwa wanaweka dhamana ya ardhi ambayo imeendelezwa, ardhi ambayo thamani yake ilikuwa ni kwa *investment* ambayo imefanywa katika eneo hilo. Lakini tofauti na sasa ni kwamba, hata ardhi ambayo haikuendelezwa inaweza kuwa dhamana kwa ajili ya mikopo. Nadhani hili ndiyo badiliko kubwa ambalo sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa tulielewe, tulione na kwamba badiliko hili ni kwa msaada wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri yote haya, bado yapo matatizo katika sheria hii. Matatizo yaliyopo makubwa ni kwamba, katika kuuza ardhi tupu lipo tatizo la kuthamini ardhi yenyewe. Wakulima wetu wengi walioko Vijijini maeneo yao ya ardhi ni madogo sana, wana eka moja, nusu eka na kule maeneo ya milimani kama Korogwe, Lushoto, Kilimanjaro na hata kule Same maeneo waliyonayo ni madogo mno, labda mtu ana nusu eka ndio eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikiria kwamba eneo la nusu eka linaweza likapata thamani kubwa na kuweza kusimama badala ya mkopo kwa kweli si jambo rahisi. Ina maana kwamba kwa sheria hii hilo ni tatizo moja kubwa yaani wananchi walio wengi hawataweza kupata thamani kubwa ya kuweza kukopa. Kwa hiyo, kama ni mikopo itakuwa ni midogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado lipo tatizo la kuwafikia wananchi hawa ambao wapo maeneo ya Vijijini, tatizo kubwa ni mtandao wa Benki zenyewe. Kama alivyozungumzia Mheshimiwa Charles Kagonji, suala hili na wengine kwamba hata kama umeamua kuwa inawezekana kukopesha kupitia *mortgage* ya ardhi, lakini kama huwezi kuwafikia wananchi walio wengi, kama huna mtandao wa kuweza kuwafikia, basi bado sheria hii itakuwa si ya manufaa makubwa kwa wananchi walio wengi, itakuwa ni ya manufaa zaidi kwa wananchi ambao wana uwezo, wako karibu na maeneo ambayo Benki hizi zipo. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, upo wasiwasi uliojengeka baina yetu kwamba sasa wananchi watapoteza ardhi yao. Napenda kusema kuwa, hata hivi sasa tunapozungumza hapa ndani wapo wananchi wanauza ardhi zao kwa sababu wananchi huwa wanauza ardhi Vijijini, leo, kesho, siku zote wanaendelea kuuza kwa ajili ya kupata manufaa yanayowahusu wao binafsi wala si kwa ajili ya kuwekeza. Inawezekana ni kwa ajili ya kusaidia watoto kwenda shule na kusaidia mambo mengine na hata wengine wanauza tu kwa sababu ya kujiona ni wazee na hawana mtu wa kurithisha ardhi hiyo. Kwa hiyo, ardhi itaendelea kuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wasiwasi huu kwamba tukiuzwa ardhi watu hawatakuwa na ardhi, nadhani si wasiwasi mkubwa katika sheria hii kwa ajili ya mikopo kwa sababu hata watakaokuwa na uwezo wa kukopa siyo watu wengi.

Kwanza ili uweze kukopa ni lazima uwe umeandika mradi, ni lazima uwe umeandika mtiririko wa fedha, ni lazima mradi wako huo bidhaa zake ziwe na soko, ni lazima mradi huo uwe unaweza kurudisha mkopo. Wananchi wenye uwezo wa kuandika mradi mpaka uonekane mradi huu kweli unakopesheka siyo wengi hapa nchini kwetu. Inawezekana bado tunazungumzia Muswada ambao matumizi yake kwa sasa ni madogo, lakini zaidi tunaweza tukasema kwamba Muswada huu unaweka mazingira ya kumfanya mwenye uwezo wa kukopa aweze kuwa na dhamana ya ardhi na hasa ile ambayo haijaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, binafsi nimekuwa kwenye Kamati hii na mambo mengi yaliyojadiliwa na mimi nimeshiriki. Nisingependa nichangie kwa muda mrefu kwa mambo yale ambayo tayari yamezungumzwa, ila nina mambo matatu madogo tu ya kupitia kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wananchi waweze kufaidika na mikopo hii na ili ule woga wa kwamba wananchi watapoteza ardhi uondoke jambo la kwanza ni kwamba, Benki zetu zinazokopesha zinapooa mwananchi anaomba mkopo ni vizuri zimsaidie kuona kwamba anao mradi mzuri, inapowezekana waweze kumsaidia kuutayarisha vizuri kusudi mradi wenyewe uwe unakopesheka na unaweza kurudisha mkopo wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni juu ya upimaji wa ardhi yenyewe. Kama tulivyoambiwa katika eneo hili la sheria kwamba ardhi iliyo tupu itakuwa ni dhamana na kwamba ardhi inatakiwa iwe imepimwa ama kwa sheria ya kawaida ambayo inampa mtu kuwa na hatimiliki au kwa njia ya kimila, nafikiri njia hii ya kupima viwanja au kupima ardhi kwa kawaida, kwanza ni njia yenye gharama kubwa halafu pili, inahitaji tuwe na idadi ya wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukilinganisha gharama na idadi ya wataalam unaweza ukaona kwamba kazi hii itakuwa haina kasi kubwa hivyo itachukua muda mrefu mpaka kufanikisha azma ile ambayo inategemewa katika Muswada huu. Ili iwe na manufaa, pengine ingekuwa vizuri ile ardhi ambayo inamilikishwa kimila ikafanyiwa mpango wa haraka ili wananchi ambao wana maeneo waweze kurithishwa maeneo hayo bila matatizo yoyote, kwa sababu hivi sasa Vijiji kwa kweli havina uwezo mkubwa wa kuweza kupima maeneo na kuwagawia wananchi na kumilikisha maeneo waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kazi hii haitafanywa kwa haraka itakuwa haina manufaa makubwa, ni vizuri Serikali ikapunguza urasimu katika upimaji, ikaangalia ni jinsi gani rahisi ambayo inawezekana Wananchi kupatiwa maeneo na kumilikishwa bila urasimu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni elimu, kwamba wananchi wetu wanahitaji kuwa na uelewa mkubwa. Uelewa huu si lazima ufanywe na Serikali peke yake, uelewa huu unaweza ukafanywa hata na Mabenki yenyewe kwa kutoa elimu wakati wanapata maombi ya wakopaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, sheria hii kama nilivyosema inaweka mazingira kwa wananchi kukopa, lakini kama mtandao wetu wa Mabenki utaendelea kubaki ulivyo yaani hautasambaa vya kutosha, hatutaweza kuanzisha Benki zinazomgusa mwananchi zaidi katika maeneo ya kilimo na katika maeneo ya mifugo. Wananchi wetu hawana uwezo mkubwa wa kuwa na miradi zaidi ya miradi ya mifugo na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nilisimama hapa kuunga hoja hii mkono na ninaiunga mkono. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na kuingia katika Bunge hili. Ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Pili, nami naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa kutuletea Muswada ambao unagusa maisha ya Watanzania. Ninampongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara hii kwa kutuletea Muswada huu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa sababu kwa kweli imeleta Muswada ambao wameufanyia kazi sana. Kama walivyosema wenzangu, nami pia ni Mjumbe wa Kamati hii, lakini kwa kweli wenzetu wamefanya kazi ya ziada, wameuchambua Muswada na watu mbalimbali wameshirikishwa katika kufanikisha suala hili. Lakini kubwa ambalo naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja ni kwa sababu umelenga kumtazama Mtanzania kwamba hana kitu chochote kile ambacho katika maisha yake angeweza kupata mtaji isipokuwa ni ardhi anayoitegemea yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wetu wengi na wanavijiji wetu wengi hawana fedha, lakini kwa sasa kwa mtaji huu na kwa Muswada huu kwa kweli ardhi sasa itakuwa ni raslimali ambayo wanaitegemea, ndiyo raslimali pekee Mtanzania wa Kijijini anayoitegemea. Kwa hiyo, ninawapongeza sana kwa kuleta Muswada huu katika kipindi muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linanifanya niunge mkono Muswada huu ni kwamba, ni miaka zaidi ya 40 sasa tumejitawala na bado tu maskini, hivyo tukiukataa Muswada huu maana yake ni kwamba tuendele kuwa maskini. Sasa hatuwezi kukubali kuendelea kuwa maskini na kama hutaki kukopa hutaendelea katika maisha, huwezi! Hakuna binadamu yeyote ambaye anaweza kuendelea katika nchi yoyote, mahali popote bila kukopa. Kwa hiyo, suala hili kwa kweli litatuwezesha kuona kwamba wananchi wetu sasa wana mahali pa kuweza kukopa, kitu ambacho kwa kweli binafsi kimenipa nguvu ya kuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naunga mkono kwa sababu Muswada huu unazungumzia Sera ya Ardhi, kwamba ardhi ni mali ya umma, ardhi ina thamani na ni mali na inapaswa kuendelezwa na siyo kuhodhiwa. Hili ni suala la msingi sana ambalo lipo katika sera na ndiyo maana nimeona niunge mkono kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nisingependa nirudie wenzangu waliyoyazungumza. Nina mchango katika eneo moja tu ambalo litaleta utata, naomba Serikali yote kwa ujumla wao walione. Kuna watu wengine wana ardhi kubwa, wengine hawana ardhi kabisa, hili ni lazima Serikali ilione. Lipo eneo ambalo naomba nilizungumze na nitazungumzia eneo hilo tu, ni migogoro ya ardhi. Hii ni lazima iondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi tusipoitoa kuna baadhi ya watu na baadhi ya wananchi wetu Muswada huu kwao hautakuwa na faida yoyote kwa sababu hawana ardhi. Sasa kama Serikali haitaji-*address seriously* katika suala hilo tutakuwa na hali ngumu sana.

Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba si wewe peke yako ambaye unaweza kulitatua hili, lakini naomba Serikali nzima iji-*address* katika kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza hivyo kutokana na *experience* na nitatoa na mifano. Kuna wananchi katika baadhi ya maeneo ambao wapo katika eneo ambalo labda ni sehemu ndogo tu, lakini utakuta mtu hawezi kuiendeleza, hawezi kuilima na hata huko kukopa kwenyewe tunakokuzungumzia hataweza kukopa. Ni wale wananchi ambao wanakaa kwenye maeneo ambayo baadhi ya wawekezaji

wamechukua mashamba makubwa na wameshindwa kuyaendeleza. Naomba sana hili Serikali ilipe kipaumbele katika kuondoa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue mfano ambao ni hai na ni mfano ambao huwa nauzungumza katika Bunge hili na nitaendelea kuzungumza katika maisha yangu yote ya Bunge. Mkoa wa Tanga ni Mkoa ambao umebahatika kuwa na mashamba ya Mkonge kwa miaka mingi na ni zao la biashara ambalo tunalitegemea katika nchi yetu. Lakini ni vizuri mkaelewa kwamba, katika mashamba hayo kuna maeneo wananchi sasa hivi baada ya mashamba haya kutokuendelezwa na sera inasema: “Wale waliohodhi mashamba...” wananchi hawa hawana maeneo ya kuweza na wao kujiendeleza.

Nikizungumzia hapa kwa mfano katika Jimbo langu la Korogwe Mashariki, robo tatu ya wananchi wangu wanaishi kando kando ya Mkonge na Mkonge umekufa. Sasa katika sheria hii tunasema wale ambao wamehodhi mashamba na hawayaendelezi, wamehodhi ardhi, wanyang’anywe na wapewe ambao wana uwezo wa kuendeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni *serious*, tulifanyie kazi. Sisemi mashamba ya Mkonge yasiwepo, binafsi napenda Mkonge uwepo kwa sababu ni zao la uchumi na ninalipigia debe sana kama Mbunge wa eneo hilo, lakini wale wenye mapori sasa Muswada huu ufanye kazi. Mapori yale wapewe watu ambao wanaweza kuendeleza, siyo yakae pale watu waone kuna ardhi kumbe hakuna! Hili ni tatizo nyeti na ni tatizo ambalo kwa kweli Serikali inatakiwa ilifanyie kazi ya ziada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano hai. Kuna shamba moja la *Magunga Estate*, lina karibu hekta 4,000, lakini hekta zinazolimwa na wawekezaji ni 300! Pia, kuna Mgombezi, Mandela, Mswaha, Hale na Mnyuzi. Hayo ni mashamba yapo. Watu wakipita barabarani wataona kuna Mkonge kumbe hakuna! Kuna maili na maili huko hakuna maendeleo ya aina yoyote, yamehodhiwa. Wananchi wanaokaa kandokando ya maeneo hayo hawana uwezo na wala hawana ubavu wa kuchukua mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii ipo kwa muda mrefu katika mashamba ya *Mohammed Enterprises*, katika mashamba ya Chavda, katika mashamba ya *Tungi Estate* na katika mashamba ya *Katani Limited*. Serikali imekumbatia kwa mfano mgogoro wa *Katani Limited*, huu sijui ni mwaka wa ngapi! Imewekwa mpaka *arbitration* suala hili haliishi, litakwisha lini? (*Makofi*)

Muswada huu unakuja sasa kunufaisha watu. Sasa wapeni basi hati kama mnaona kwamba wanaweza kuendeleza. Wapeni hati waendeleze Mkonge kuliko kukaa muda mrefu bila kutatua tatizo ambalo haliishi. Nategemea Serikali hasa kutokana na Muswada huu ilimalize tatizo hili ili wananchi wale wajue namna gani watakvayopata ardhi yao kwa sababu hawana ardhi. Hao wenzetu pia waliopata mashamba sasa wachukue *hectors* ambazo wana uwezo wa kuziendeleza nyingine waachie. Waachie ili wananchi wapewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Korogwe hasa katika Kijiji cha Hale-Mwakinyumbi kumshukuru Mheshimiwa Charles Keenja. Alipokuja juzi alikabidhi ardhi kwa wananchi wa Hale-Mwakinyumbi hekta 4,000.

Sisi tunampongeza sana, hiki ni kilio toka nimeingia ndani ya Bunge hili kwa miaka mingi sana, kuiomba Serikali itoe eneo kwa ajili ya wananchi ili walime, leo tumepatiwa hekta 4,000 sasa mwananchi huyo atapata naye angalau eka zake 10, 20 au 30 atakwenda kukopa fedha au akajiendeleze. Hayo ndiyo tunayotaka, lakini kung’ang’ania mashamba na hamyawezi mnang’ang’ania ya nini na mkonge hauliwi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimefarijika sana na hawa wenzetu (Wawekezaji), ili waendane na Muswada huu wasiwafanye wananchi wa maeneo yale kwamba hawaelewi. Sasa hivi upo mtindo wa kusema *smallholder* apewe eka 10 alime Mkonge, hilo silikatai, nakubaliana nalo, lakini nani mwenye mali? Ni *Mohammed Enterprise* ambaye amekupa uwe *smallholder* una *sublease* humo ndani? Ni nani ambaye Serikali itampa hati? Naomba kama kuna ku-*sublease*, yule mwananchi anayepewa hekta 20, hekta 10 apewe hati yake, siyo atumiwe tu kama *rubberstamp*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mtu anapewa hati ya 2,000 *hectors* halafu wewe unam-*sublease* unamchomeka humo unamwambia lima Mkonge, lakini shamba siyo mali yake, si sahihi ni uonevu. Sasa tuwape wale wananchi maeneo yao, kama ni eka 10 apewe haki yake aendeleze shamba lake na alime mkonge, hiyo sawa, lakini siyo mnasema shamba hili sisi ndiyo tunachukua hati, yatakuwa yale aliyozungumzia ndugu yangu Mheshimiwa Charles Kagonji na Waheshimiwa wengine hapa. Watu wanachukua hati wanakwenda kukopa hela sisi tunaendelea kuwa maskini, hatutakubali. Huo ni utumwa ndani ya nchi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo haya ambayo leo nimeyazungumzia, naomba leo iwe mwisho. Kwa Muswada huu sasa Serikali ifikie muafaka, pia wale wananchi walioshindwa kuendeleza mashamba hayo waondolewe, wafukuzwe ili wapewe watu wenye uwezo na wananchi wamegewe maeneo, wapewe hatimiliki na wawe na maeneo ambayo wanaweza kuyamudu wenyewe na kuendeleza mkonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kulirudia hili kwa sababu ninapozungumza hivi nashikwa na jazba kwa sababu linaniuma, linanikera sana kwa sababu ni suala ambalo kwa muda mrefu halijapatiwa ufumbuzi. Tunaambiwa kuna *arbitration*, Mheshimiwa Warioba ndiyo amepewa hiyo nafasi ya kuwa *mediator* kati ya Serikali na watu wengine, lakini mpaka leo ufumbuzi haujapatikana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla mfikie mwisho wa suala hili ili Mkonge uendelee na wananchi wa Mkoa wa Tanga nao wafaidike. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze na kutoa pongezi kwa mwenzetu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, ambaye ameteuliwa kuungana nasi humu ndani. *(Makofi)*

Pili, pongezi zangu ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote ambao tangu juzi tumewapa dhamana ya kuwapitisha kwa kura nyingi tu kutuwakilisha sehemu nyingi na tunategemea kwamba watatuwakilisha kama ambavyo tumewapa dhamana hiyo. *(Makofi)*

Tatu, ningependa kutoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Gideon Cheyo, wataalam wake na watendaji kwa kutuandalia marekebisho haya ya Muswada ambao tulikwishaupitisha mwaka 1999, lakini kama Serikali waliona marekebisho yanapaswa kuwepo kwa sababu sheria zetu zinapaswa kwenda na wakati hasa wakati huu wa utandawazi ila tu tunapaswa kuwa na tahadhari kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sitakuwa na mengi sana ya kuzungumza, lakini ningependa ndani ya Muswada huu licha ya jumla mengi ambayo wenzangu walionitangulia wameyasema na kwa kweli ninakubaliana nao kwa sababu mpaka hivi tunavyozungumza baadhi ya wananchi bado wana ile hali ya kufikiri kwamba Wabunge ndiyo wamekwenda kuuza ardhi huko kwa kupitisha Muswada huu.

Kwa hiyo, yote yaliyoshauriwa na wenzangu ninayaafiki, la msingi likiwa lile la elimu kwa sababu wakati mwingine mtu unaweza ukalalamikia kitu kwa kulalamika tu, lakini hujui undani wa jambo lenyewe. Kwa hiyo, suala la elimu ni la msingi sana kabla ya Muswada huu kupita kuwa sheria na kuanza kuutumia wote wakopaji, wakopeshaji na wananchi tujue undani wa marekebisho haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo napenda kuzungumzia ni katika ukurasa wa 6 kuhusu haya maneno ya *matrimonial home*. Kwenye Muswada tumeambiwa tuangalie Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Ninashauri kwamba badala ya kungoja *reference* na wengine hata hiyo Sheria ya Ndoa huenda hawana mikononi mwao kuelewa kwamba kipengele hiki kilisema nini, basi kiandikwe hapa hapa ndani ya Muswada huu huu, maana hiyo itolewe hapa hapa kuliko tena kwamba turudi 1971 ambapo wengine hata hiyo sheria hatujawahi kuiona. Si mimi, lakini walio wengi ninaamini haya yatakuwa ni matatizo kwao. Kwa hiyo, tuwarahisishie kazi kwa kutoa tafsiri hapa hapa ili mtu aweze kuelewa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 7 nimefurahishwa sana na Muswada huu kwa sababu umetilika maanani hali halisi ya jamii zetu kwamba tuna ndoa za mitala, ndoa zinazothibitishwa na dini na ndoa za mila na desturi.

Kwa hiyo, Muswada huu ume-*take into account* hali halisi hiyo, kwamba hizo ndoa zipo na ndiyo maana imeruhusu kwamba mume kabla hajakopa basi akae na wale wake wote sita alionao, awaeleze na wale waridhie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nilivyoelwa ni kwamba, wote sita watatia *signature* kwenye huo mkataba, kwamba mmoja akifariki kati ya sita, angalau watano watajua mume wao alifanya nini.

Kwa hiyo, hili kwa kweli nimelifurahia kwa sababu hata mwanamke amepewa hadhi na nafasi yake hapa kwamba na yeye ni mmiliki mmojawapo na ni lazima ajue nini kinaendelea ndani ya nyumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie ndani ya Muswada huu ni kwamba ukurasa wa 17, Ibara kadhaa pale zimeeleza kwamba mkopaji atapewa siku 30 za kukamilisha mkopo kwa *notice* hiyo, atakayopewa baada ya siku 30 ardhi hiyo, inaweza ikauzwa, inaweza ikafanyiwa chochote na mkopeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu tunazungumza wananchi walio wengi na wengi hawana hizo fedha za haraka haraka. Mimi nilikuwa naomba hizi siku 30 ambazo ni mabadiliko ya sheria 1999 ilisema siku 90 hapa tumerudi siku 30 mimi naona *speed* ya kurudi imekuwa kali mno, kiasi kwamba siku 30 ni chache mno za *notice* hiyo. Kama haturudi kwenye siku 90 ambayo ni miezi mitatu, basi nashauri iwe angalau miezi miwili mtu aambiwe kwamba ahaa! Bwana usipojiweza ardhi inakwenda. Vinginevyo kwa watu wengi sheria hii kwa suala hili watasema basi ndiyo njia ya kutunyang'anya kimacho macho. Hili naomba Serikali ilifikirie sana, siku 30 kwa wengi ni chache ziongezwe ili mtu aweze kuzitafuta hata kama ni kukopa kwa ndugu na jamaa ili ardhi hiyo, basi isiwe kama ameipoteza burebure tu pamoja na kwamba alikopa na maafikiano.

Nafahamu kwamba lengo ni kujaribu kuhamasisha mkopaji alipe haraka haraka. Lakini uharaka huu umezidi kwa sababu wengi watahindwa. Kama ilivyotokea viwanja vya Dar es Salaam, mara wiki tatu rudisheni, tulihangaika pamoja na kwamba wengine wameweza kuvilipia lakini tufikirie walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya mimi kwa ujumla Muswada huu nimeuelewa, baada ya wenzangu kutuelimisha kwamba ardhi sasa itapata thamani, lakini kama wengine walivyosisitiza tuwe na tahadhari sana wajanja hapa ndiyo watachukua nafasi ya kuteka nyara wengi ambao hawaelewi. Kwa hiyo, elimu ni ya msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kushauri hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi na la pili, nimpongeze Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kuleta marekebisho haya na la tatu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba nafasi zake kumi za kuteua Wabunge, sasa amekamilisha.

Kwa kweli Mheshimiwa Rais ameonyesha kwamba anaweza akafuata Katiba ipasavyo na amemaliza hasa kwa kumteua rafiki yangu Bwana Charles Makongoro Nyerere ambaye naye aliwahi kuonja zulia hili jekundu. Kwa hiyo, ni vizuri tu kwamba sasa yuko nasi tena, naye nampongeza. Nadhani wengine sasa nafasi haipo imekwisha kwa hiyo, waliokuwa wanatarajia tena basi tena. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba Muswada kwa sehemu kubwa marekebisho yanagusa kuweka rehani ardhi na uuzaji wa ardhi tupu. Sasa ili sheria yoyote itekelezwe vizuri kwa maoni yangu nadhani kuna mambo kama manne kama yafuatayo:-

Moja, ni lazima sheria hiyo, ieleweke vizuri, ni jinsi inavyoeleweka kwa wananchi, lazima sheria iwe na *Public Understanding*. Sheria isipoeleweka kwa wananchi kutatokea uhasama kati ya Serikali na wananchi, utekelezaji wake utakuwa duni na vile vile watu wanaweza wakachukua sheria mkononi. Hilo la kwanza ili sheria itekelezwe vizuri, lazima kwanza watu waelewe vizuri.

Lakini la pili, lazima sheria iungwe mkono na wananchi ili itekelezwe vizuri. Sheria yoyote ambayo haiungwi mkono na wananchi haiwezi ikatekelezwa vizuri. Itakosa ushirikiano kwa mfano ukiitunga sheria ukasema mwizi afungwe kifungo cha nje au jambazi afungwe kifungo cha nje. Sheria ya namna hiyo, haiwezi ikaungwa mkono na wananchi. Kwa hiyo, sheria lazima iungwe mkono na wananchi. *(Makofi)*

Lakini la tatu, ni kuona kwamba sheria inaweza ikatekelezwa vizuri iwapo wananchi watafikia mahali pa kutaka mabadiliko ya sheria yenyewe kulingana na wakati. Kwa mfano, katika sheria hii sasa wananchi wanataka mikopo kwa kutaka ardhi nayo iwe sehemu ya kuwekwa rehani, ili aweze kupata mtaji kwa njia iliyo rahisi na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la nne, ni kwamba ni jinsi ambavyo watendaji wanavyotekeleza sheria, kama watendaji hawatatekeleza sheria vizuri basi ujue sheria hiyo haiwezi ikatekelezeka. Nitoe mfano mdogo sheria hii ambayo sasa ambayo tumeitunga tangu mwaka 1999, tulikubaliana kwamba ardhi tupu ni lazima nayo iwe na thamani na ni lazima ifidiwe. Unapochukua ardhi lazima ithamanishwe na ifidiwe. Ardhi watekelezaji wasiipofanya inavyotakiwa au wakifanya vinginevyo basi ni kwamba sheria hiyo watu hawataipenda na haitekelezeki, kwa hiyo, kutakuwa kunakukwama kwa utekelezaji. Wananchi wanaweza wakaichukua Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe mfano wa Babati. Babati ni Mji unaokua na ambapo sasa viwanja vinagawiwa. Wananchi ambao walikuwa na ardhi katika eneo la mji wa Babati kwa muda wa miaka mingi maisha yao wameyatategemea pale kwa miaka mingi sana. Sasa mipango miji inapokuja ile ardhi inachukuliwa ili ipimwe viwanja, kama hakuna utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba, kwanza yule ambaye ardhi inachukuliwa anapewa kiwanja basi kutakuwa na matatizo makubwa sana. Kama sehemu ya ardhi yake kwa mfano ana eka mbili inaweza ikatoa labda viwanja labda vinne, sita au nane kulingana na mahitaji ya vipimo vya viwanja kama viwanja hivyo haviwezi kufidiwa basi tayari unatengeneza mgogoro mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi tatizo hilo lipo Babati na ni Mji ambao sasa unakua jambo hili halitekelezwi vizuri, yako malalamiko mengi sana juu ya utekelezaji wa sheria ya ardhi ambayo kwa kweli inamtaka mtu aliyekutwa katika eneo naye apewe kiwanja na vile vingine lazima awe mtu wa kwanza kupewa na vile vingine vipate fidia hapo ndipo kwa kweli unaweza ukakubaliana kwamba ardhi inaweza ikawa sasa sehemu ya raslimali. Kwa sababu unapochukua ardhi ya mtu kwa sababu ya kupanua mji, halafu ardhi ile unampa mtu anajenga ghorofa, anajenga jumba kubwa la biashara, yule uliyemchukulia hukumpa hata *plot* hivyo unadhani kweli hilo ghorofa huyu mtu si atakuwa alia kwamba afadhali lianguke hilo ghorofa? Kwa sababu hukumpa hata yeye ardhi kwenye eneo ambalo yeye zamani alikaa pale. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuangalia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye vifungu vichache vya Muswada ukurasa wa nne kifungu cha 5 (9) ambayo inaeleza mazingira ya uuzaji wa anayeuzua inaonekana kwamba habanwi sana na mazingira ya uuzaji. Mimi nilidhani kwamba badala ya kuruhusu tu watu kuuza ardhi holela au hata kwa utaratibu huu la kwanza lingekuwa tuwasaidie wananchi hawa waendeleze hiyo ardhi hata kwa kupanda miti tunashindwa kuwaambia? Waiendeleze ipate thamani vizuri zaidi halafu ndiyo wauze. *(Makofi)*

Vifungu hivi nikiangalia (a) mpaka (f) sawa inasema ardhi tupu isiuzwe kwa tofauti zaidi ya mara tatu bila kuendelezwa. Mnunuzi vile vile asifanye makubaliana yasiyokuwa na ahadi ya kuiendeleza ardhi iliyonunuliwa bila maendeleo. Kwa mtazamo wangu nilikuwa naona kwamba ukishasema ardhi tupu isiuzwe kwa watu tofauti zaidi ya mara tatu, ina maana unamruhusu auze mara ya kwanza na ya pili bila kuendelezwa. Sasa hapa tunatengeneza mwanya wa utapeli, mwanya wa ulaghali, udanganyifu na utajiri wa haraka haraka. Mwanya huu ni lazima Serikali iuangalie kabisa. Mtu anapouza kwa mara ya kwanza

labda ni kwa matatizo, kwanza aulizwe kuwe na eneo la kuulizwa mtu kwa nini unauza unataka kufanyia nini? Iwekwe bayana.

Halafu pili ikishauzwa ile yule ambaye ameuziwa mara ya pili anapotaka kuiuza kwa mtu mwingine ni lazima pamoja na masharti yale kwamba inakubadilika kwamba ataweka ahadi, ahadi tu haitoshi, sioni kama kuna adhabu yoyote inayopendekezwa kwamba asipotimiza hayo kuna lipi litafanyika hakuna. Kwa hiyo, tusitoe mwanya ambao utawata-peli watu.

Kwa mfano mtu wa kwanza anaweza akauza kwa laki tano kwa sababu ya shida zake, lakini yule aliyenunua kwa laki tano kwa sababu anajua kwamba eneo lile ni eneo muhimu akauza kwa muda mfupi ikiwa vile vile tupu kwa milioni mbili. Yule tena kwa muda mfupi akamuuzia mtu wa tatu kwa shilingi milioni tano.

Sasa huyu wa shilingi laki tano na yule wa shilingi milioni tano kwa kipindi kifupi tunatoa mwanya ambao kwa kweli nilikuwa nadhani kwamba kunahitaji sana tuangalie sana jambo hili ili kuondoa udanganyifu na mwanya wa utapeli na ulaghali na huo utajiri wa haraka haraka. Lazima sheria nayo ionyeshe kwamba watu wa namna hii tunawafanya nini. Sasa sijaona sheria katika marekebisho haya, lakini sijui pengine iko kwenye sheria ile kubwa, lakini nadhani marekebisho yoyote lazima yaendane na sheria na adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 127(c) ardhi ya rehani ili iuzwe zimetajwa pale siku 60. Nakubaliana na wale waliosema kwamba ni lazima tutoe nafasi na mimi nilidhani nafasi ingepelekwa mpaka siku 90 ili kuturuhusu mawasiliano, masharti ya mkataba na sheria zingine ziangaliwe kama alivyosema Mheshimiwa Margareth Mkanga, kuna mambo mengine pale ya mirathi na ndoa nao kuwe na muda wa kutosha. Hii haraka tunayotoa kwenye sheria inatusaidia nini na tunakimbilia wapi? Tutoe nafasi ya kutosha ili ardhi kwa kweli iangaliwe kama raslimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukumbuke hivi mantiki ya wakati wa *operation* vijiji kugawa ekari tatu, tano ni nini ilikuwa? Kama siyo kumsaidia Mtanzania apate walau chakula chake kwenye eka tatu? Leo tunapokubali kirahisi rahisi na kugawa na kusema kwamba basi sasa inaweza ikauzwa baada ya muda mfupi iliwekwa rehani tumesahau zile sababu ambazo tulisema kwamba ili tuendelee tunahitaji karibu manne ambayo ni ardhi, watu, siasa safi, uongozi bora na Rais sasa ameongezea amesema na mtaji. Kwa nini tunataka kusahau hayo mambo?

Tukumbuke kwamba ardhi ya eka tatu tatu iligawanywa kwa sababu hiyo kuwasaidia wananchi wadogo wapate mahitaji yao kwanza ya chakula, hii ndiyo mantiki yake nadhani. Kwa hiyo, tusifanye haraka sana katika sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ufafanuzi wa vifungu vya 135 na 136 ni muhimu katika kuweka uwiano mzuri kati ya mkopaji na mkopeshwaji, ufafanuzi unahitajika ili watu waelewe vizuri vifungu hivyo. Lakini vile vile tunao wageni wasio raia ni muhimu katika sheria hii, maafisa uhamiaji washirikishwe kikamilifu wakati wa uuzaji wa kubadilisha hati miliki wa kukodisha hii ni muhimu sana kwa sababu watu wengine wasio raia ni wajanja sana na wanaweza kughushi hata vitambulisho, hata hati. Hili jambo lazima liangaliwe vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme la mwisho kwamba tayari sasa kanuni zimekwishatungwa kwa sheria hii hasa katika mabaraza ya ardhi, *The Land District Court Act 2002, regulations* zake zimeshatoka, sasa nilikuwa najuliza sasa ni nani anaunda haya mabaraza kule Wilayani? Ni Mkuu wa Wilaya, ni Mkurugenzi?

Ni nani sasa anahakikishwa kwamba kwenye vijiji tunakuwa sasa na mabaraza katika kila kijiji yanayoshughulikia ardhi? Yale ya vijiji na Kata. Kwa sababu zoezi hili linaonekana kwamba sasa linasuasua. Bunge limeshamaliza kazi ya kutunga sheria, sheria imeshatungwa kwa kiswahili, vitabu viko kule vijijini, viko kule Wilayani, sasa nani anaunda haya mabaraza haya? Ni muhimu sana mabaraza haya ya ardhi katika ngazi ya kijiji yaundwe haraka iwezekanavyo ili kuondoa hii migogoro kuanzia kijiji kata mpaka Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, basi mimi niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa sheria hii. Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba utendaji ndiyo jambo la msingi katika kutekeleza sheria. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kushiriki kutoa mchango wangu katika hoja hii. Lakini pia kwa sababu nimeupitia vizuri sana Muswada huu nimeusoma nikauelewa vizuri nitajitahidi sana kutoa mchango ambao utasaidia kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia mengine, niseme tu kwamba naunga mkono Muswada na upite uwe sheria, lakini maboresho yanayoelezwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kwa kweli yawe ndiyo nguzo ya kuujenga huu Muswada, ili uwe sheria nzuri zaidi. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wametangulia wametoa mchango yao inachangia kutoa utaratibu ambao utazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubali lakini nijaribu kutoa maelezo ya kukumbusha Serikali mambo machache hapa. Jambo la kwanza nasema Katiba ndiyo inayozaa sheria, lakini pia sheria huzaa Kanuni, lakini pia kanuni nazo huzaa utaratibu, lakini utaratibu nao unazaa utekelezaji, lakini utekelezaji unazaa athari. Sasa hapo unaweza athari nzuri ama athari mbaya. Kwa hiyo, naomba basi hatma ya Muswada huu uzae athari nzuri kwa maana kanuni zitakazokuwa zimetungwa baada ya sheria hii kupita uzingatie athari nzuri. Hicho ni Kiswahili barabara, kuna athari nzuri, athari mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba Serikali izingatie basi yafuatayo ili lengo la kuboresha Muswada uweze kufanikiwa. Yapo mambo saba yafuatayo:-

Kwanza, katika Miswada ya kurekebisha sheria mbalimbali zihusuzo ardhi, tutumie mkakati wa Taifa wa kusimamia utekelezaji wa sera za kuondoa umaskini nchini. Sheria zote zitakazoletwa lazima tuzingatie kwa sababu tumejiwekea taratibu za kuondoa umaskini katika nchi yetu. Tutaondoa umaskini kupitia ardhi, hilo moja.

Pili, kwa kuwa wananchi zaidi ya asilimia 80 huishi vijijini na ndiyo maskini zaidi, naomba Serikali ilione hilo ili wasionewe, wasipuuzwe na wajanja wachache kupitia sheria hii. Kwa sababu watu watakwenda vijijini watavamia ardhi halafu wananchi hao wanyonge, maskini watabaki kuwa vibarua wa hao.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali lazima izingatie sana katika kutengeneza kanuni zitakazo walinde hawa wananchi wachache maskini ambao wanatumia ardhi yetu hii kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Tatu, kuna watu wanaopenda ndoa za mitala kwa mfano watani zetu sisi ni Wahehe, Wahehe wanapenda sana kuoa wake wawili, watatu na kuendelea, lakini pia hata katika Uislam tunaruhusiwa zaidi ya mke mmoja, lakini wasizidi wanne, wakizidi basi utakuwa umevunja sheria. Sasa hao wanawake na watoto walindwe ili sheria hii iweze kufanya kazi vizuri.

Nne, kwa kuwa sheria hii inaweza kuzalisha matajiri hata makabaila wa ardhi kule vijijini naomba sheria hii iweke kanuni za kulinda wachungaji wetu wanaochunga mifugo na malisho yao. Tusije tukafika mahali malisho yote yakamalizwa halafu wachungaji wetu wakashindwa mahali pa kufugia mifugo yao. Ni muhimu sana. *(Makofi)*

Zingatia la tano, tafadhali sana sheria hii isiwe na jaribio la kujenga tabaka kubwa la wanaomiliki ardhi halafu wananchi wanyonge wawe vibarua katika maeneo yale. Hilo naomba sana. Kwa hiyo, katika kanuni zile zikinge, ziwalinde hawa wafugaji. Tunaweza tukafikiri tunajenga uchumi halafu baadaye kumbe tunaporomoshwa uchumi. *(Makofi)*

Sita, kwa kuwa umaskini uliopo nchini umejikita sana kwa Watanzania takribani asilimia 36 ndiyo maskini sana, sheria na kanuni zilenge kuwakomboa hawa wananchi na katika kulenga kuwakomboa ndiyo



maana hata Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia wanasema kile kipindi cha *notice* kiwe siku 90 siyo 30, siku 30 haitoshi. Wananchi wa kawaida maskini wataporwa mashamba kwa sababu siku 30 ni chache ziwe 90. Nafikiri Waziri na Serikali inasikia. (*Makofi*)

Saba, ndiyo ya mwisho eneo la vita dhidi ya umaskini hapa nchini ni ardhi na watu wake. Hivyo ardhi ndiyo mtaji rahisi kabisa wa watu wetu maskini. Upungufu wa ajira kwa vijana wetu nchini upo kwa kiwango cha asilimia 35. Sasa sheria hii na kanuni zake zichochee basi kuondoa hali hiyo, kwa maana kwamba sheria hii iwe chanzo cha kuibua ajira miongoni mwa vijana. Tutoe nafasi ili vijana wetu wapate ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa na hayo machache, lakini naendelea kuisisitiza kwamba ni muhimu sana, Serikali ikatumia ardhi ili wananchi wetu maskini waweze kulindwa, waweze kuondoa umaskini. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wamezungumza humu ndani. Ninataka nianze kwanza kwa kukubali kwamba mimi Muswada huu ninaunga mkono, halafu baadaye nitaeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachozungumzwa hapa ni mahusiano ya uzalishaji mali. Tunazungumza habari ya *The Political Economy of Capitalism* na *The Political Economy of Socialism*. Mahusiano ya uzalishaji mali ya Kibepari ama kwa mtindo wenyewe au *by orientation, history* haikuweza kuonyesha kwamba hatimaye wanaomiliki ardhi watakuwa ni walio wengi hata kidogo. Hakuna mahali popote, tumesomasoma *epochs* zote, soma *Slavery*, soma *Feudalism*, soma *Capitalism* hakuna mahali popote panaposema mahusiano ya uzalishaji mali yakiwa na mwelekeo huo yatakuzalishia watu wengi kumiliki ardhi hakuna kitu cha namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokwenda kwenye *The Political on Economy of Socialism* katika maana ya mfumo wa kijamaa, hapa kwetu hatuna mfumo wa kijamaa tuna mwelekeo wa kijamaa, njia kuu za uchumi ikiwemo ardhi inakuwa mikononi mwa umma, ndivyo *history* inavyotonyesha.

Mimi nataka kujenga *premises* hiyo ili tukifika mahali tusije tukaanza kulaumiana tuonekana kwamba tunakuwa *irresponsible*. Haya matatizo mengi kabisa, *Europe* ukisoma walikuwa na kitu kinachoitwa *primitive accumulation*, wakileta kitu kinachoitwa *enclosure system* na wakajenga sheria wakasema hizi sheria hizi zinawazuia walio wengi wanatoka nje na sheria zinaweka pale unawaweka viboko ukiwakuta mitaani hakuna kuingia katika lile eneo wanaweka uzio ndiyo tunayozungumza. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni vizuri hata wale wanaotusikiliza wajue kwamba hawa wamepitisha sheria, lakini walijua kwamba sheria hii ina madhara haya na haya na haya. Mheshimiwa Gideon Cheyo, usije ukawa na wasiwasi, mimi hapa nitafika mahali nitaonyesha kwamba ni kwa nini *at this particular moment* Serikali inafikiri kwamba ifanye hivi inavyofanya.

Lakini mimi nafikiri na ninaamini kwamba ukifanya hivyo unavyofanya, ukasema kwamba hatimaye walio wengi watailiki ardhi (*is not true*) si kweli.

Kwanza kwangu mimi Kilimanjaro kwa maana ya Siha, wakinisikiliza watakumbia iko wapi hiyo ardhi unayozungumzia. Kinachozungumzwa hapa Waheshimiwa Wabunge, kama naelewa ni kwamba ardhi, huku nyuma kote tulikopita ilikuwa na kitu kinachoitwa (*use value*), *value* ya matumizi na tulikuwa tunasema ardhi ni mali ya Taifa na watu walikuwa wanafanya ujanja ukitaka kuuza ardhi ulikuwa huuzi ardhi unasema mimi nina mihogo yangu mle ndani, nina mahindi mle ndani, mna kahawa mle ndani nina nyumba kule kwa hiyo ninachouza ni mihogo, ni nyumba ulikuwa huuzi ardhi. Kwa sababu isije ikatumika kama *exit* tunafika mahali Watanzania tunakuja kuzalisha tatizo, sasa wameanza kuiona Zambabwe

inaingia hapa hatutaki twende huko, tuondoke tuwe waangalifu, tunataka tujue kwamba tunakwenda wapi, tunataka kujua kwamba ni nini maana yake hiki kinachozungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa Tanzania kama nilitaka kumiliki ardhi nilikuwa nakwenda Wizara ya Ardhi wakati ule walikuwa Wakuu wa Wilaya ndiyo walikuwa Wenyeviti wa wa kamati ya ardhi inayogawa ardhi. Nilikuwa silipi kitu chochote, nilikuwa nakwenda pale nasema jamani mimi nataka kumiliki hii ardhi hapa, nataka kuitumia kwa ajili ya biashara, nataka kujenga nyumba, nataka kulima na vitu vinginevyo, ninaandikiwa mimi hati pale napewa masharti sana sana ilikuwa na shilingi 35,000/= shilingi 60,000/=.

Leo unazungumza habari ya kwamba mwananchi mmoja atatakiwa anunue ardhi ile kwa shilingi 500,000/= mwananchi yupi? Hiyo ni *on your marks, get set go* watatimka pale wenye nguvu na ubavu ndiyo watakaokamata watachukua hiyo ardhi ndiyo watawakamata. (Makofi)

Ni lazima tuanze hiyo tuanze na *premise* lazima tukubaliana kwamba hapa ninachotaka kusisitiza hapa wananchi Watanzania, Wabunge, wenzangu lazima tuwe *very traditional and very conservative* kuhusu suala la ardhi. Ardhi iendeleo kubaki ni mali ya umma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awe na kauli nayo. Ukishaweka hiyo, una hakika na unachofanya. Aje mtu hapa aitumie ardhi kwa maana ya matumizi akifika mahali amehodhi ardhi haitumii kama alivyotuambia ataitumia, unamwambia bwana wewe ondoka unairudisha ardhi. Ardhi pale kijijini ibaki kuwa mali ya kijiji. Baba wa Taifa ndicho alichotuachia kama urithi. (Makofi)

Sasa mimi najua watu wengine watasema huyu *very conservative* na haya maneno unayosema najua siyo muafaka sana! Lakini kwa nini Serikali inafika mahali inasema kwamba sasa tufike mahali tuifanye ardhi iwe na thamani ya kubadilisha yaani badala ya kuwa na thamani ya matumizi unataka iwe na kitu kinachoitwa *exchange value* ni kwa sababu *you have to start with a full acceptance of the fact* kwamba huna kitu kinachoitwa mtaji. Kama huna mtaji sasa wananchi hawa unawapelekaje? (Makofi)

Sasa hivi hapa tumebadilisha mahusiano ya uzalishaji mali, tumekwenda kwenye mwelekeo wa kibepari, zinakuja benki hapa kutoka nje zinakuja haziwezi kutoa hela mfukoni hivi zikatoa hivi zikatupa hapa zikakumbia chukua. Tunachoambiwa leo hii ni kwamba tuende tukawaambia wananchi wetu ule mchezo wa zamani ulikuwa unachukua pesa unakwenda zako, lazima kuweco na nidhani ya hali ya juu katika kuchukua mikopo ndiyo ujumbe tunaoletewa hapa.

Wewe una watoto watano na mke wako wewe unachukua hela pale unakwenda kulewa pombe halafu unasema unajua bwana nchi hii ni nchi ya kijamaa, mimi nimeshangaa nimekwenda benki nikaenda nikachukua mkopo sasa wanakuja wanauza shamba langu litakwenda, kama ni nyumba itauzwa ndivyo inavyokwenda. Hii inaita *a cut throat competition*, ndiyo itakayokuja hapa. Hakuna tena. Watu walikuja hapa wakasema tutaendeleza viwandani, waliviendeleza? Mashamba pale *West Kilimanjaro* watu walisema kuwa wataendeleza mashamba pale wameendeleza, wamekaa pale wameanza kuwakodishia wananchi wale wale wanakuwa wanakodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba lazima tufike mahali tuainishe tuseme kwamba tunasema nini katika jambo hili. Mimi 50% ya *voters* wangu ni wafugaji, ni Wamasai, mimi ni Kiongozi wa Wamasai Mheshimiwa Edward Lowassa, anafhamu habari hii. (Makofi)

Leo nikitoka hapa nikienda kule nyumbani nikawaambia wananchi kwamba ardhi kutoka sasa ni itauzwa, lazima sheria hii iniambie kwamba wafugaji, wale wachungaji wangu kule Lekimuni, walioko Karani, Magadini, Makiwaru, Otkolin, Donyomorok, hao nakwenda kuwaambia nini kuhusu hii sheria mpya? Usije ukakuta pori limekaa pale halafu unawaambia nafunga hivi, nafunga hivi halafu tumeliuza hili na tumekaa hapa kwa ajili ya kwenda kuchukua mkopo wa Benki, *problem!* (Makofi)

Lile eneo kuna kitu kinachoitwa *land use plan*. Lazima uli-*demarcate* useme hapa hawezi kujenga mtu, hawezi kulima mtu, hapa ni kwa ajili ya kuchungia ng'ombe, lazima itamkwe hivyo. Mimi najua Mheshimiwa Edward Lowassa huko aliko anafurahi sana na maneno haya. Huwezi ukaambiwa kwa sababu sasa ng'ombe wale watakwenda kuchungwa wapi? Hilo moja.

Pili, mashamba kwa mfano katika Jimbo langu la Siha, mashamba yako chini ya *NAFCO, NARCO* katika maana ya mifugo, sina *problem* nayo najua tutapewa utaratibu. Mashamba yako katika Vyama vya Msingi na mashamba yako katika *KNCU*. Wako watu wameingia kule. Katika *Siha Kyeyo Cooperative Society* kwa mfano, lipo eneo pale linachukuliwa kila wakati wanabadilishana pale, wanakuja pale, wanaitwa *strategic investors* ili utishike uogope, unafikiri anasema kitu cha ajabu sana. Unajua, sasa unashangaa wewe unasema maneno haya, tumempata *strategic investor*, wewe utaogopa eh, *strategic investor*, unaogopa. (*Kicheko/Makofi*)

Wale wanakuja pale siku mbili, tatu, badala ya kuendeleza zao la Kahawa pale unakuta wanakodishia watu mashamba. Hatuna *problem* na hiyo, lakini wananchi wanaozunguka maeneo hayo walioko katika eneo la Jimbo la Siha pale, kila siku wanapiga kelele hapa. Juzi nimeuliza swali hapa kuhusu *West Kilimanjaro* itakuwaje? Nikaambiwa kwamba watauziwa. Nani? Hawa waliokuwepo Kilimanjaro ndugu zangu hawa ni Wanyakyusa, Wafipa, hao wote walioko *West Kilimanjaro*, waliokwenda kule kihistoria. Leo uniambie watakwenda kutoa laki tano, milioni moja, watazipata wapi? Wale ni vibarua tu mzee wangu walioko pale.

Chonde chonde Mzee Gideon Cheyo, nakuomba kule *West Kilimanjaro* kwanza kawagawie yale mashamba mapema kabla ya mwaka 2005, la sivyo sirudi huku. Nitapata matatizo. Wataniambia wewe umekwenda kule unapitisha sheria ya ajabu ajabu pale, tulikuwa na mpango hapa tulijua kwamba kila mtu atapata heka mbili, heka tatu! Pale ninao ma-*squatter* wamekaa pale kwenye maboksi, leo mimi sheria inapita hapa halafu waniambia nenda kawaambie walipe hela, watoe wapi? Wamekaa pale wanasubiri wanajua kwamba wanakwenda. Chonde chonde, nawaombeni. Mimi jamani mniangalie. Kule kwangu mkienda kwa mtindo huu tunaokwenda nao, humu sirudi. (*Kicheko/Makofi*)

Ninachosema hapa, tufike mahali tuainishe. Kusema kwamba mtu atakwenda kufanya valuation ya ardhi, ardhi value yake inatokana na *activities* zinazofanyika mahali. Kama uko Dar es Salaam, robo heka, nusu heka bei yake, value yake itakuwa juu kuliko mtu aliyeko Dodoma, maeneo ya Kijijini kwa robo heka ile ile inayozungumzwa hapa. Unasema kwamba mimi nitakwenda kufanya *valuation*. Wala huna haja ya kwenda kufanya *valuation*! Kama tumekuta kuna almasi pale, kama tumekuta kuna dhahabu pale, *automatically* utaona value ya ardhi ile itapanda pale.

Kwa hiyo, kutakuwa na watu wanaitwa *Land Speculators*, anakaa pale anajua kwamba hapa huu Mji unavyokua hapa unavyokwenda mimi naweza nikachukua heka zangu 20, 30 nikabana nazo ili kesho nikabadilisha nikapeleka kule badala ya ku-*invest* kwenye Benki mimi nita-*invest* kwenye ardhi. Sheria hii inatuambia nini kuhusu *Land Speculators*? Wako watakaokuwa wanangoja ardhi tu wanakuwa na maeneo makubwa makubwa.

Pili, sheria hii inatuambia nini kuhusu wakulima wadogo wadogo ambao wamerithi maeneo? Najua kwamba hapa utaratibu huu wa kumiliki ardhi kimila unazungumzwa, lakini kinachosemwa hapa ni kwamba huyu mtu atatakiwa a-*develop* lile eneo. *Contradiction* iliyoko katika nchi za kwetu changa hizi ni kati ya vitendea kazi na *labour*. Hakuna *mechanized agriculture*. Wewe unasema kwamba lazima a-*develop* lile eneo, huyu anakwenda kulima kwa jembe la mkono halafu unasema eti aende akali-*develop* lile eneo, asipoweza kufanya namna hiyo mtampa mtu mwingine. Sheria hii, utaratibu huu unatuambia nini kwa maana ya *the level of the productive forces*? Kwa sababu usiseme tu kwamba lazima aendeleze lile eneo, wale wanalima kwa jembe la mkono tena la kuketi hapo chini na sehemu yote anasikiliza redio. Wewe unasema kwamba leo tutakwenda tu hivi, lisipoendelezwa linachukuliwa. Sio *enclosure system* hiyo? Sio ndiyo tunakwenda hivyo? (*Makofi*)

Mzee wangu Naibu Spika, hii sauti nilishakwambia, mama juzi alisema watu wanapiga kelele huko, sijui hata kama napiga kelele, *I want to argue my case* hapa.

Mimi watu wananisubiri huko nje wananisikiliza. Naomba mtusaidie mashamba ya Serikali yaliyoko *West Kilimanjaro*, yaliyoko chini ya Vyama vya Ushirika, yaende yafike mahali tuone kwamba wananchi wa kawaida wanaweza na wao wakapewa maeneo ambayo watamiliki, wakishamiliki ndio waanze sasa hii shughuli halafu kila mtu atajaza huko mbele ya safari atajua itakavyokwenda. (*Makofi*)

Napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba sitaki kuji-*contradict*. Mimi ninaiona *logic* ya Serikali. Kama sisi hatuna mtaji, lazima tufike mahali tukae, hakuna mtu atakayekupa mkopo hapa. Kwa msingi huo na ndilo ninalozungumza hapa, ukisoma yote hii, Mheshimiwa Gideon Cheyo anazungumza humu ndani, anasema hivi katika maana ya kwamba tumefika mahali hatuwezi kuwa tunaikalia ardhi hivi hivi, lazima ufike mahali uibadilishe kama unavyobadilisha ng'ombe upate pesa halafu ujenge uelimishe watoto na vitu vingine.

Kwa msingi huu, mimi hii naiunga mkono. *It is very unfortunate* ndio tumefika hapo, lakini kwa msingi huo *at least* hakuna mtu atakayenipa shilingi zake milioni tano hivi tu naweka mfukoni, umekuwa *Parish worker*, umekuwa unafanya kazi Msikitini au wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Semindu Pawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatus Magayane na Mheshimiwa Ruth Msafiri, pia ajiandae.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu.

Nilishapongeza tayari na nilishatoa kheri ya mwaka mpya, kilichobakia tu ni kwamba niliona kwamba rafiki yangu Mheshimiwa Gideon Cheyo, anatoa Muswada huu wa Sheria itabidi na mimi niunge mkono kwa sababu sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ambayo tuliipitisha hii ni ya Kijiji ambayo tulipata nakala Waheshimiwa Wabunge na ilianza mwaka 2001. Nilikuwa namtania pale tu kwamba hivi Mheshimiwa Gideon Cheyo kuwa hii sheria kweli mwaka 2001 imeshaanza kutekelezwa? Akaniambia ndiyo imeshatekelezwa na ni kweli huu ni utaratibu wa ardhi, ugawaji, usimamizi na hatua zinachukuliwa, Kamati zinazoundwa, mambo ya usuluhishi na masuala mengine. Kwa hiyo, yote imeeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika kinachokuja hapa ni kwamba pamoja na Sheria, ardhi ya jumla si ya ardhi kwamba wanaongezea kipengele kimoja mle ndani na kufanya marekebicho kadhaa ili kuifanya ardhi sasa iwe na thamani. Sio mali, kwa sababu ukisema ardhi ni mali, basi itakuwa ni *commodity*, kwa hiyo, inakuwa *judged* kwa kitu ambacho price kutokana na thamani yake kwa mtu inanunuliwa ovyo ovyo. Tumewaambia Watanzania pamoja na dunia kwa ujumla kwamba muwe makini kweli kweli katika raslimali zenu. Raslimali moja ambayo mtakuwa nayo makini ni ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja wa ka nchi kamoja kanaitwa Tuaru. Tuaru nikiitaja mtacheka lakini ni nchi. Ina *square mile* kumi ambayo *square kilometer 21* yenye watu 8,239 na ina Serikali. Hii taarifa ya mwaka 1998. Mtaniuliza kwa nini nimetaja mwaka?

Nimetaja mwaka huo kwa sababu idadi sasa hivi ya Tuaru kwa mujibu wa *internet* ni watu 15,413. Nitawasomea *internet* niliyopata kwa upande wa [www/population.com](http://www/population.com) ambayo nitawatajia lakini inaonesha dhahiri kwamba kumbe watu huongezeka, lakini Tuaru nikauliza je, eneo lenu limeongezeka mara ngapi? Wakaniambia iko vile vile *square mile 10* na vile vile kwenye nchi haipandwi wala haikuzwi, ni raslimali ambayo inataka ilindwe kweli kweli. Ndiyo maana Serikali katika sera na Mheshimiwa Gideon Cheyo alirudia, naomba ninukuu hapa nadhani naruhusiwa kusoma kwa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri wa Ardhi, ukurasa wa 35 ibara ya 67, mbwembwe zile nimeziacha nimeanzia kwenye sera, Sera ya Taifa ya Ardhi haijabadilika. Ardhi ya Tanzania ni mali ya raia wote wa Tanzania. Ardhi ya Tanzania haiuzwi kwa wasio raia wa Tanzania, ardhi itatambuliwa kuwa na thamani na inatarajiwa kutumika kama dhamana kwa mikopo ya vyombo vya fedha.

Nilidhani Mheshimiwa Gideon Cheyo ni Sheikh Yahya ambaye anatabiri mambo yanayokuja. Haya niliyasema wakati akisoma hotuba yake ya mwaka 2003/2004, sasa leo yametokea. Nimeamini kweli kweli leo ni vitendo, kesho ndoto jana ni historia. (*Kicheko/Makofi*)

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni mwongozo ambao tunatekeleza, sasa hivi nafikiria ni *two step* katika ukurasa wa 32 ibara ya 33. Kwa kutambua kwamba ardhi ni raslimali kuu kuliko zote, hapo nime-underline katika uchumi wa nchi yetu Chama cha Mapinduzi kwa kupitia Serikali Kuu na Serikali za Mitaa itaendeleza juhudi zinazokwisha, hili ni neno la Kiswahili jipya, katika kipindi kilichopita cha kuwahakikishia kuwa wananchi wataelimishwa ili watambue umuhimu wa kuendeleza ardhi kwa kumiliki raslimali ya kuwaondolea umasikini kuwaletea maendeleo.

Ya tatu, anasema ngazi zote za uongozi wa Chama cha Mapinduzi zitahamasisha Vijiji kuchangia gharama za upimaji. Sasa inakuja namba nne, inasema: “Utaratibu wa kuthaminisha ardhi kwa maslahi ya wananchi wetu unahimizwa na utaendelezwa kufuatwa katika maeneo husika.” Mwisho wa kunukuu.

Kwa hiyo, hapo unatekeleza Ilani ya Uchaguzi, lakini kwenye utekelezaji sasa, nimesema kwamba utekelezaji mara nyingi unaleta matatizo. Nakupa kitu kimoja tu, kwamba mara nyingi hivi tunaanzia mwisho lakini unianza mapema ili muweze kuelewa. Hotelini wako watumishi wengi wote wamevaa *uniform* wanafanya kazi moja ya kuuza bidhaa ndani ya Hoteli. Sasa watu wanne wanaagiza vitu, mmoja anaagiza maziwa. Sasa yule mmoja anatumia *style* yake anayojua yeye mwenyewe. Maziwa akaandika ‘M,’ yeye mwenyewe anajua kabisa ‘M’ ni maziwa. Mwingine akasema anataka andazi, akaandika ‘A’ likatokea “MA,” mwingine akasema nipatie wali, akaandika ‘W’, ikatokea “MAW,” mwingine akasema matunda yapo? Akasema ndizi hakuna, zipo embe. Akasema nipatie embe, akaandika ‘E’. Ikatokea MAWE. (Kicheko)

Sasa baada ya hapo akaitwa kuna mgeni wake, yule jamaa aliyeagizwa kuna mgeni akaacha hela pamoja na yale maandishi kwenye meza nyingine akaondoka. Wateja wamekaa baada ya nusu saa wakamwita mwingine wakamwambia ninyi watu wa Hoteli hii sio wastaarabu, muda wa saa nzima tuko hapo kwa kashfa na nini chukua mali zetu utuletee. Kwenda akakuta hela na neno MAWE. Akachukua mawe akaleta. Nani alaumiwe? Mtekelezaji au aliyeandika? Wote hawana makosa kwa sababu aliyeandika, kwa utaratibu aliyeagiza yule wa kwanza angeleta maziwa, andazi, wali na embe. Lakini kwa kuwa hakuna mawasiliano sahihi kati ya huyo wa kwanza na wa pili, kaleta mawe. Hapo tusilaumiane. (Kicheko)

Kwa hiyo, katika kanuni ambazo utaziweka, weka taratibu ambazo zitaelimisha kwamba zisigongane na sheria yenyewe ambayo inatajwa katika vifungu hivi. Najua hii sio sheria mpya, bali unathaminisha ardhi. Sheria ile mama ya ardhi ipo pale pale. Sasa haya mabanki yanayotajwa kwenye sera, yale yaliyoambiwa *Barclays Bank* au *Stanbic* au *NBC Limited*, nadhani sio hayo tu. Tutaunda Benki yenye mfumo wa kuangalia wakulima, sio Benki hii. Hizi najua kwa vyovyote zitakuwa tukiwapa hizi tu ndiyo wale tulikataza wageni kule wasinunue ardhi, halafu Benki za wageni zinakopesha watu.

Kwa hiyo, wana *feature* ile ya *style* ambayo siyo *indirect feature* tena, watapitia hata hivyo kwamba wale ni Benki za kigeni zipewe masharti kwa sababu wana sheria zao za kibenki. Nimeona katika ibara ya 141 mpaka 142 katika Muswada huu inaeleza ni *financial institution* na utaratibu wa kukopa tu. Kwa hiyo, huo utaratibu, jinsi gani mtu unapata ardhi kwa sababu tayari imekuwa *accommodated* kwenye ile sheria iliyopita.

Kwa hiyo, kuna *regulations* nyingi zimekuja safari hii, *Intrusion Act*, kuna Chama cha Wanamabanki, sasa kuna aina za mabanki, kuna *Commercial Bank*, kuna *Savings Bank*, kuna *Credit Bank*, kuna Benki nyingine Benki Kuu, kwa hiyo, unakuta kwamba hizi Benki kwa mwongozo wa *BOT* kwenye Benki hiyo itambulike kwamba inaweka *collateral* yake inaweka ardhi. Wakati huo nadhani na *financial institution* nao wataleta *Financial Institution Act* katika kubadilisha vipengele kwamba *collateral*, ili wazikubali kwa sababu mkopeshaji na mkopwaji sasa wanakutana mahali pamoja wasije wakagongana kama wale makengeza wawili wakagongana halafu wakaanza kulaumiana badala ya kutafuta njia ya kwenda pamoja. Kengeza mmoja akamwambia kwa nini huendi unakoangalia? Mwenzake akamwambia na wewe kwa nini huangalii unakokwenda? Hawaku-solve problem pale. (Kicheko)

Muswada mzuri lakini utekelezaji wake. Naomba nirudie, wanasema kwamba makengeza wawili waligongana. Sasa walipogongana badala ya kutafuta *solution* wasigongane waende bega kwa bega badala ya kuja ana kwa ana, mmoja akamlaumu mwenzie kwa nini huangalii unakokwenda na mwenzie

akamwambia na wewe kwa nini huendi unakoangalia? Kwa hiyo, ngoma ikawa *draw*. Kwa hiyo, hawaku-*solve* tatizo walikuwa wanalaumiana tu. Kwa hiyo, lawama hazisaidii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu ndio maana hatuajiri Majaji makengeza vile vile. *Judges* mara nyingi anatakiwa awe *straight*. Jaji mmoja alikuwa makengeza alikuwa anaangalia washitakiwa watatu, akamwuliza wa kwanza. Kumbema wakati anamwanguka wa kwanza macho yake yalikuwa yanamwanguka kama anamwona wa pili yule, sasa wa pili akaona anakaziwa macho, akamwuliza wewe mshitakiwa jina lako nani? Akajibu wa pili, ninaitwa Joel. Alikasirika, akasema mimi nimemwuliza mtu wa kwanza anajibu wa pili. Akamwuliza wa pili, sikukwambia wewe, kwani nimekuuliza wewe? Wa tatu, akasema mimi sijasema kitu Jaji. Kwa hiyo, macho alivyomwanguka wa pili akamwanguka mtu wa tatu. Kwa hiyo, hapo akaamua afute kesi, akaona hawa watu ni wendawazimu, kumbema ni kwa sababu ya macho yake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu basi, neno *mortgage* lilitumika katika Na.121 ukurasa wa 142, sasa nimekuta kuna kitu kinaitwa kama *housing*. Sasa hapa tunasema Sheria ya Ardhi, neno nyumba mbona limeingia ghafla pale? Tumelikuta neno *housing* limeingia kwenye Muswada huu wakati tumesema tuna ardhi. Sasa ukitaja nyumba ni kitu ambacho ni *asset*.

Vile vile kuna maneno fulani fulani nilitaka niyaangalie, kwa mfano kuna neno moja limetumika neno *court*. *Technician* ya *court* haipo, ni *court* ya aina gani? Halafu vile vile muda ule, tulikubaliana kwamba Waziri umeandika siku 30, lakini wenzako wanakwambia siku 40, sasa kwa nini usiseme 50? Kaa katikati basi. Usikubali 90 lakini acha thelathini, sema hamsini basi tukubaliane. Tusibishane kama mabata.

Mara nyingi kuku wanasikilizana, sijawahi kuona bata anamsikiliza mwenzie. Mwenzie akisema kha na yeye kha, sijui wanasikilizana saa ngapi! Kwa hiyo, tuwe na utaratibu wa kusikilizana. Kwa hiyo, kama imekataliwa hizi siku 90 na sisi hatutaki 30, sema 50 basi. (*Kicheko*)

Mwisho, nampongeza Waziri kuhusu elimu kwa umma. Ameanza tayari, ameshapeleka vitabu Vijijini karibu 7,853 na vile vile Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Semina ilishafanyika ngazi ya *radio*, *television*, sheria tunazona na kwamba zilielezwa, vitabu vya sheria za Vijiji ambavyo tumepata Wabunge na vile vile vitabu nadhani katika taarifa yako umetoa vitabu 3,464, kanuni 2,681.

Nadhani hizi ni kanuni za ardhi, sio kanuni za hii. Kanuni za hii nazo vile vile utugawiwe iwe tafsiri kwa Kiswahili maana wakati mwingine kuna matatizo ya tafsiri ya maelezo na afadhali kutokuelewa kitu kuliko kuelewa vibaya. Kwa sababu usipoelewa kitu hutekelezi, lakini ukielewa vibaya unatekeleza. Yupo mtu alileta athari baada ya kuelewa vibaya kitu. Alifuata tahadhari kadhaa ambazo ziliwahi kutokea kwa kutokuelewa kwa kutekeleza.

Aliambiwa hivi, alikuwa anamtuma mkewe kila siku kwamba twanga, pika, fanya hivi, siku moja kazi karibu sabini. Sasa walimshauri wakamwambia usimue mkeo kwa kazi ngumu, acha umeme ufanye kazi hiyo. Sasa neno hiyo, alitafsiri akadhani basi kazi hiyo ni ya kumuua mkewe badala ya kuuwawa na kazi ngumu. (*Kicheko*)

Lingine vile vile alitafsiri vibaya. Walimwambia kwamba mtoto wako kila ukimpa maziwa mabichi hapendi, wakamwambia *if your child did not sleep on fresh milk boil it*. Walimwambia kama mtoto wako hapendi maziwa mabichi, chemsha. Kwa hiyo, uchemshe nini, mtoto au maziwa? (*Kicheko*)

La msingi ni kuangalia kabisa kwamba katika sheria hii kuna neno *court* limetumika katika ibara ya 140 mpaka 141 neno *court* liwe na ufafanuzi. *Civil Procedures* ambayo ilielezwa katika *Act* Na.66. Nadhani 66 ile sio *Act* ni *Bill*. Bado *Act* au *Bill*. Lingine limeeleza kuhusu maneno kama neno *house* katika upande wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika la msingi katika utekelezaji wa Muswada huu twende pamoja mbele moja tu. Ninaposema twende mbele Watanzania, sio kila mtu mbele kwake. Kwa hiyo, tukisema twende mbele, wewe ukija mbele kwako na wao wakija mbele kwao tutakwaana. Twende mbele kwa taratibu za

viongozi wa Ilani ya Uchaguzi, tunajielekeza na utaratibu wa sera zetu. Kwa hiyo, mbele ya Tanzania ni mbele kote kwetu wote.

Hivyo basi, kabla Muswada huu haujatekelezwa, tungeomba kwamba mipaka ya Vijiji iangaliwe kwa sababu yapo matatizo. Sasa hivi yalitokea matatizo ya mipaka kati ya Wilaya fulani na Kondo. Kuna mipaka ya Wilaya na Wilaya, kuna mipaka ya Vijiji na Vijiji. Kama kwangu kule kwa mfano Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, yako matatizo ya mipaka katika maeneo kama vile Kiloka kwenda Kiziwa, Mkuyuni kwenda Mwalazi, Kibukwe na Lukange, Changa hadi Ludewa, Lung'ala hadi Burugi, Kalundu na Kibwaya, Kibwaya na Mfumbwe, Logo na Uponda, kwa hiyo vyote hivyo Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mifuru, Hewe, Bagiro, Nyamigadu, Mkololo, Kumba, Amili, Ludewa, maeneo yote yale mpaka Mkulazi, Chanyumbu, unakuta wanatakiwa sheria hii waielewe na vile vile watekelezewe mipaka yao na kupewa ardhi kuwa thamani. *(Kicheko)*

Watanania kwa ujumla ardhi ina thamani lakini haiuzwi kwa bei hivi hivi, inapewa thamani ili ukopee kama *collateral*. Ahsante, nitawaelimisha Watanania kwa ujumla. Ni wakati wetu wa kuwaelimisha Watanania kabla ya uchaguzi ili kusudi muwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni goli la nne. Goli la kwanza lilifungwa Kitaifa la kifundi na Rais wetu kwa utawala bora kutambulika Tanzania, tukafunga goli la kwanza katika miaka ya nyuma. Goli hilo lilikuwa lile ambalo lilitufanya kufutiwa madeni kwa mpango wa *HIPC*. Hilo goli la kwanza, hamshangilii Wabunge?! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika goli la pili lilifungwa kwa kisigino kwa kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni, ambalo Waziri wa Elimu alifunga kwa kisigino kwa kufuta michango yote ya Shule za Msingi. Hilo lilikuwa goli la pili. *(Makofi)*

Goli la tatu, lilifungwa na Waziri wa Fedha, tulipofuta zile kodi zote za sitini na kufuta kodi ya Maendeleo kwa Watanania. Hilo ni goli la kiufundi. *(Makofi)*

Goli la nne, ni hili la leo ambalo Waziri wa TAMISEMI ni kuhusu Ma-*VEO* walielezwa leo pamoja na hili ambalo Watanania sasa mna thamani ya ardhi yenu muitumie. Goli la nne hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika goli la tano, nadhani sasa hivi Serikali yetu inashambulia, nadhani mtalisikia wakati wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Muswada huu katika jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitapenda kuchangia hasa katika hoja moja inayohusu uuzaji wa ardhi tupu. Pengine inawezekana nisingevutika sana kuchangia Muswada huu isipokuwa hoja hiyo nilipoiona sikuwa na budi kuomba nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi yetu kimsingi ni mali ya umma, ni mali ya Serikali, ni ardhi ambayo inamilikiwa chini ya taratibu za kimila, lakini pia inamilikiwa katika sheria za kiserikali. Katika nyakati zote hizi, wananchi walio wengi wanamiliki ardhi katika misingi ya kimila na maeneo kwa mfano ya Mkoa wa Kagera, ardhi za kimila huwa haziuzwi hata kama hazikuendelezwa. Lakini kwa taratibu hizi ambazo tunakwenda nazo sasa, tunaelekea mno katika taratibu za kuiweka ardhi katika mazingira ya kuwa ni mtaji na kuweza kuomba mikopo hali ambayo inafanya ardhi iende katika kuthaminishwa na kuweza kuwa thamani pengine ya kitu kama mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakuwa na wasiwasi mkubwa kwamba inawezekana sasa ikawa ni wakati wa wale ambao ni wajanja kuanza kuchukua nafasi hii kwa haraka haraka mara baada ya sheria hii kuwa Muswada, kwenda kuvivamia Vijiji na kupora ardhi za Wanavijiji ambao wao hawaelewi nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi katika maeneo ninayoyafahamu mimi yaliyo mengi zinamilikiwa na Vijiji vyenyewe, ziko chini ya Serikali za Vijiji, hapa badala ya hii sehemu inayomwambia kwamba huyu mwenye kuweza kuuza ardhi hii aeleze yeye mwenyewe mipango atakayokwenda kufanyia ardhi. Kwa hiyo mnunuzi aseme, atakapoinunua ardhi ile ataifanyia kitu gani. Mimi nahisi kwamba sasa kunaanza kutokea mvurugano wa matumizi ya ardhi.

Kwa hiyo, katika kipengele hiki ni kwamba Serikali Kuu kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji iweke utaratibu wa kila eneo litatumika kwa kitu gani. Wakati ambapo mmiliki yupo hai au hajakuwa tayari kuuza aitumie ardhi ile kwa matumizi yake mwenyewe. Lakini atakapokuwa amefikia mahali anasema ninataka kuuza, basi ionekane katika mipango ya kile Kijiji, ile ardhi kama inatakiwa ijengwe shule basi ni shule, kama ni kiwanda basi kijengwe kiwanda, kama ni makazi yawe ni makazi na kama ni eneo la kubaki wazi liwe ni eneo wazi kusudi isije ikawa ardhi ikawepo tu kwa yule ambaye anayeinunua ndio apange mipango gani anataka kutumia kwa ile ardhi badala ya Serikali yenyewe kuwa imewekea ardhi matumizi yake. Hilo nilikuwa naomba lizingatiwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika maeneo ya Vijiji vile vile lazima tuzingatie kwamba tunao wakulima hawa wa zana ndogo ndogo, majembe ya mkono, pia tunao wafugaji ambao ni wachungaji. Katika eneo langu mimi ninayo matatizo makubwa sana kati ya watu hawa. Pale ambapo wanachunga na pia kuna mashamba, ni taabu kubwa sana, migogoro ya kila mara inahitaji hekima na busara kuwapatanisha hawa kukaa pamoja.

Sasa tunapokuwa tunasema mwenye ardhi aiuze, mimi ninakuwa na mashaka sana hawa wachungaji watakwenda kuchungia wapi mifugo yao? Sasa ni lazima kile Kijiji kihakikishe kwamba kimetenga maeneo ambayo wafugaji wataweza kuchunga mifugo yao, lakini vile vile na wakulima wawe na uhakika kwamba watalima wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi hii lazima iwekewe taratibu ili kusudi isije ikafika wakati tukajikuta hatuna ardhi tena, bali kila ardhi ina mwenye nayo na Serikali ikihitaji kufanya kitu chochote kile haiwezi kuiendeleza kwa sababu tayari ina mwenye nayo ambaye ameinunua. Lakini si hivyo tu, Serikali ikajikuta inatakiwa kutoa gharama kubwa sana za kulipa fidia kwa hawa watu binafsi ambao wamechukua ardhi na hawaiendelezi.

Sasa wasiwasi wangu ni kwamba wakati mtu amechukua ardhi kubwa ambayo hana uwezo wa kuiendeleza pengine kwa njia ya kuimiliki kimila au kwa njia ya kuimiliki kisheria, uwezo wake ni kuiendeleza eneo dogo tu, sasa eneo lile lililobaki yeye anaamua kuliiza kwa thamani anayoitaka yeye.

Muswada unasema hii ardhi tupu isiuzwe kwa watu tofauti zaidi ya mara tatu bila kuendelezwa. Kwa hiyo, muuzaji ataiuza kwa mara ya kwanza, haiendelezwi, mara ya pili, haiendelezwi na mara ya tatu. Maana yake ameambiwa isizidi mara tatu.

Kwa hiyo, kuna watu watatu tofauti wanaoweza wakahamisha ule umilikaji bila kuwa na swali lolote. Lakini hapo hapo linawekwa lingine kwamba mnunuzi asifanye makubaliano yasiyo na ahadi ya kuiendeleza ardhi iliyonunuliwa bila maendeleo. Haya maelezo yanajikanganya. Ni lazima muuzaji ardhi kwa kushirikiana na Serikali yake ieleweke ardhi ile ni kwa ajili ya shughuli gani ili atakayekwenda kuinunua ni lazima ainunue kwa ile shughuli iliyopangiwa pale.

Lakini vile vile ni nani atakayekuwa anatumiza kumbukumbu kwamba ardhi hii iliuzwa mara ya kwanza kwa fulani, ikauzwa mara ya pili kwa fulani, ikauzwa mara ya tatu kwa fulani, ni nani atakayetunza kumbukumbu hizi? Basi kama ni hivyo, Muswada uweke wazi kwamba ni lazima Serikali za Vijiji zishiriki ipasavyo na zitunze kumbukumbu kusudi pale itakapokuwa imetokea ardhi hii inavyouzwa mara kadhaa kuwe na namna ya kuweza kuzuia ule uuzaji. Vijiji viwe na mamlaka ya kuzuia uuzaji wa holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mahakama, hasa Mahakama za Mwanzo zihusishwe katika kila maeneo kuona kwamba zinasimamia hili la uuzaji ambao ni wa lengo tu wa kujipatia pesa. Lakini ikibidi kuwe na muda kati ya muuzaji wa kwanza, wa pili na watatu. Vinginevyo yule muuzaji wa tatu



atanyang'anywa ardhi aliyoinunua kwa wale ambao wamekuwa nayo tangu mtu wa kwanza, wa pili na yeye sasa ni wa nne, kwa sababu inauzwa mara tatu, si zaidi ya mara tatu. Yeye atakuwa sasa ana muda pengine anaambiwa wewe usiuze tena lakini kwa nini asiuze tena wakati mtu wa kwanza aliuza, wa pili akauza na wa tatu akauza? Kwa nini yeye asiuze tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuwe na muda kati ya mnunuzi wa kwanza na wa pili na pia kutolewe sababu ni kwa nini mnunuzi wa kwanza anataka kuuza kabla ya kuiendeleza na mnunuzi wa pili kwa nini anauza kabla ya kuiendeleza? Kama si hivyo mchezo huo utakuwa ni mchezo ambao hauna mwisho na kwa kweli Serikali haitaweza kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naridhika tu kwamba ardhi ingebaki ni mali ya umma kusudi matumizi yake yaweze kuwa yanasimamiwa na umma. Ndio maana nasema kuwe na muda ili kama waendelezaji watatu wanakuwa wameshindwa ardhi ile irudi kwa Serikali, isiendele kuwa inauzwa tu na haina mwisho.

Lakini vile vile ardhi isiyo na kitu haina uchungu na haina mipango. Kwa hiyo, inakuwa ni ardhi iliyokuwepo pale ambayo hata mwenyewe wala haijali, kwa sababu yeye anachotaka ni apate pesa ngapi. Wasemaji wenzangu wamesema muuzaji mwingine anaweza kuanza kwa laki tano. Mwingine akasema milioni 2, kwa sababu inategemea yule anahitaji pesa kwa haraka gani na kwa jambo gani.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba suala hili liangaliwe sana tunaposema kuuza ardhi tupu ni lazima umakini wa hali ya juu sana uwepo ili kuhakikisha kwamba isije ikatokea tukakuta kuna Watanzania watakaobaki hawana ardhi kabisa katika maisha yao na hawajui mahali pa kwenda na wakawepo watu wachache ambao wanamiliki ardhi halafu wengine hawana mahali pa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunao wawekezaji wengi. Lakini wawekezaji wetu wanaoingia hapa wanataka kwenda kuwekeza mahali ambapo Serikali yetu inapata faida kubwa sana. Nako ni kwenye vileo, ni kwenye mabenki, kwenye madini, kwenye ziwa, au bahari lakini nani anayekuja kuwekeza kwenye kilimo.

Mimi nadhani sasa mwelekeo wa Serikali pia uwe katika kuona kwamba tunapata wawekezaji katika kilimo ili ardhi yetu iweze kuwa na thamani. Kwa sababu ardhi inapobaki pale tu haitumiki ila mtu anaweza akaiuza ikiwa tupu. Mimi sioni thamani yake, hata kama hili litapita, lakini sioni thamani yake. Ni thamani ya shilingi ngapi ya kuuza ardhi tupu katika Mkoa wa Kagera katika pori la kule Biharamulo, utaiuza shilingi ngapi.

Pori langu la Ngenge na Rushwa utauza shilingi ngapi. Mimi sioni ile thamani zaidi ya kwamba naona kwamba uuzaji wake utakuwa mkubwa. Lakini kama hii ardhi ingeendelezwa na hawa wawekezaji wetu wakubwa ingewezesha sasa kuwa na mashamba makubwa na kuwapa ajira kwa vijana na hata kizazi kijacho kikaona thamani ya ardhi badala ya kukimbilia kuuza kikawa tayari sasa kuitunza. Kwa sababu anayekwenda kuiuza kama alishindwa kupanda miti, miti tu ambayo unaweza ukaota mbegu zinazojiokea akapanda miti kwa mpangilio. Alishindwa kupanda minazi kwa mfano, hivi inawezekana vipi huyu akiuza ardhi atakuwa na mpango gani ambao nasema atakwenda kufanyia shughuli anazoonza zinafaa, shughuli gani, za biashara, shughuli za nini, kwa sababu kilimo kimeshamshinda. Shughuli gani sasa. Stielewi hapa itakuwa ni shughuli gani. Pengine elimu ya kutosha itolewe isije ikawa sasa wengine wakafikiri kwamba ukishapata ardhi unaiuza unakwenda mjini. Kwa sababu mjini ndio mahali panapoonekana maisha yanakwenda kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka nilizungumzie ni suala linalohusu kuweka rehani. Ni jambo jema kwamba ardhi sasa inaweza ikawekwa rehani. Lakini wasiwasi pia hapo ni kwamba sasa mabenki yetu mengi au yote kwa mwelekeo wetu ni kwamba tumeyabinafsisha kwa wageni. Sasa yule mweka rehani ya ardhi ni kwamba akiona ule muda aliyokubaliana au vyovyote atakavyoona inafaa yeye, anaweza akataka kubaki na ile ardhi.

Kwa hiyo, kama ndiyo utakuwa mtindo, kijiji fulani watu 10 waliokaa pamoja wakaenda kukopa halafu baadaye wale wakaona kwamba sasa wanaweza wakajimilikisha ardhi kwa taratibu wanazoziona

zinafaa unaweza ukakuta vijiji vinaanza kupotea kimoja kimoja chini ya mabenki, baada ya hapo sijui tutakuwa tunaishi kwa namna gani.

Mimi ningelishauri sana suala hili likaangaliwa sana namna ya mtu aliyekopa kwa kutumia ardhi yake na kuipoteza ardhi yake. Kwa msingi huo suala zima la siku lazima liangaliwe. Siku 30 ni chache mno na zinazingatia Dar es Salaam, zinazingatia sheria hii pengine kwa sababu Makao Makuu yanayofanya kazi hasa yako Dar es Salaam yanazingatia pengine labda nchi nzima ni kama Dar es Salaam. Lakini wamfikie na mkulima wangu wa Ngenge na Rushwa anayekaa kule porini sana ambaye naye anatakiwa kuwa na haki ya kujitetea, siku 30 hazimtoshi. Siku lazima ziongezwe ziwe za kumpa haki kila Mtanzania naye aweze kutumia haki yake kusimamia na kutetea nafasi yake. Kwa hiyo, mimi napendekeza zisipungue siku 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo nirudie tu kusema kwamba suala la uuzaji wa ardhi tupu liangaliwe kwa makini na kwa kweli kama inawezekana hiyo ibara Na. 8 iliyokuwepo, inayobadilishwa sasa na kuweka mpya ya 8 na 9 katika Muswada wa mwaka 1999 ingebaki bila marekebisho makubwa. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kushiriki katika kuchangia Muswada huu wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Muswada huu ni mzito sana lakini pia ni muhimu sana kwa Taifa letu hili la Tanzania na mimi nataka niungane na wenzangu kwamba naunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Lakini pia niitake Serikali iwe mwangalifu sana juu ya Muswada huu na tusingalie leo tu tuangalie miaka 30, 40 inayokuja mbele. Nimelisema hili na tunayaomba haya mabenki ambayo yatachukua dhamana ya kukopesha hii mikopo na baadaye wananchi wakashindwa kuilipa na kulazimika kuuzwa kwa maeneo yale kwamba maeneo haya yasije yakanunuliwa na watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, imenipata hofu hii kwa sababu kama wananchi wale ambao watakuwa wamekopa na wakashindwa kuurudisha ule mkopo, mabenki yataweza kuyauza maeneo hayo kwa watu wengine. Kwa hiyo, kuonekana utaratibu kwamba yasijeingia mapesa kutoka nje ya nchi ambayo yataweza kununua maeneo hayo ambayo kwa wale watakuweza kushindwa kulipa madeni haya ambayo wamekopa benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikinukuu Muswada wenyewe unasema madhumuni ya Muswada huu unatoa mapendekezo ya kufanya mabadiliko katika Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ili kuweka mazingira ya kuwezesha mabenki na Taasisi za fedha kutoa mikopo kwa wananchi kwa urahisi na kwa ufanisi. Kuna vitu viwili ambavyo hapa vitatufunga kwamba tunategemea kwamba itatupa kwa urahisi na kwa ufanisi. Lakini matumaini ya ufanisi hatutajua utakuwa vipi baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sana mikopo ya benki wengi wanaokopa benki hawalizi kuilipa na tuna ushahidi sisi kule Zanzibar wananchi wengi waliuziwa nyumba zao na mabenki, kuna walishindwa kurudisha ile mikopo. Kwa hiyo, imenitisha hii wananchi wengi wenzetu huku Bara mtapoteza ardhi kwa kiwango kikubwa sana. Hili nataka nilizungumze kwa uwazi. Sisi kule Zanzibar imetukuta hii. Kuna wananchi wengi sana wameuziwa nyumba zao kutokana na kushindwa kulipa riba ya mabenki. Kwa hiyo, Serikali iwe mwangalifu kwenye suala hili, tunapisha suala zito ambayo wananchi wetu wataamini kwamba Bunge limepitisha lakini kwa kweli watakuwa hawako radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili mimi nataka nimnukuu Rais Benjamin Mkapa katika hotuba yake ya tarehe 31 Mei, 2003. Kuna sehemu ilieleza kwamba, aliwataka viongozi mbalimbali nchini kuwasaidia wananchi wafikie malengo yao yale waliyokusudia.

Kwa hiyo, tunaupitisha Muswada huu sote viongozi tukiwemo Wabunge, viongozi wa Vyama vya Siasa, Watendaji wa Vijiji tuwe wa kweli juu ya kuelezea Muswada na malengo ya Serikali katika

kuisaidia jamii katika kufikia malengo ya kimaendeleo. Kama sisi tutakuwa tunapitisha wenzetu wengine wakazungumza vingine itakuwa hatufanikishi suala hili. Tunasababisha migogoro ambayo haina maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niitake Serikali kwa sababu Muswada umeletwa na Wizara hii ya Ardhi lakini Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihusike kwa asilimia kubwa kwa sababu migogoro ya ardhi katika Vijiji katika Wilaya, Watendaji wa Vijiji na Halmashauri, wanahusika katika baadhi ya migogoro ya ardhi. Utakuta vibali vingine vinatoka tu na tunafanya hofu baadhi ya wakazi wajanja vingine wa mijini wakaenda kuyauza maeneo ya vijiji kwa kupatia mikopo hii ya fedha.

Kwa hiyo, hili naishauri sana Serikali tusipitishie tu Muswada huu lakini kuwe na usimamizi mzuri vinginevyo tutajiingiza katika matatizo makubwa sana na wenzetu wanasiasa wasije kutumia vibaya juu ya Muswada huu. Kwa sababu nimetishika, kati ya wadau ambao amewasilisha Mwenyekiti wa Kamati ni wa mabenki zaidi lakini sikuona wasomi wa nchi hii wanasema nini na hawana dhana yoyote ambayo watafirikia vibaya inaweza ikaliyumbisha Taifa hili.

Kwa hiyo, nilitaka niisitizie Serikali kwamba iwe makini sana katika kulisimamia. Ndani ya Muswada huu yapo mapendekezo ambayo yatahusu Sheria ya wakopaji wadogo wadogo hususan uwekaji wa rehani wa ardhi inayomilikiwa kimila. Hapa patolewe ufafanuzi thabiti, kimila aina gani. Ni maeneo gani au ni ile familia tu kwamba labda mume ana wake wanne na watoto wale pengine 20 au mila ile ni ya kikabila au vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu jambo lolote ambalo litafanywa zaidi ya mtu mmoja lina matatizo. Kwa hiyo, hili suala liwekewe ufafanuzi wa kutosha na faida kubwa kwa umma zaidi, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba itakuwepo kinga ya kulinda hawa wakopaji wadogo wadogo. Lakini hii haijasaidia, kwa sababu wakopaji wadogo wadogo wengi ambao tutaweza kupambanisha sisi ni kama pengine wanaofanya biashara ndogo ndogo (Wamachinga). Haiwezekani akaenda kukopa afanye biashara na tunaporudisha mikopo pamoja na kwamba tuna kawaida ya kupitia *voucher* zote za mishahara, tunaujua ugumu wake juu ya hawa wanaofanya biashara wadogo wadogo.

Kwa hiyo, hili ningetaka Serikali, Mheshimiwa Waziri sina wasi wasi na wewe kwa sababu hata ugawaji wako wa viwanja haukuleta mgogoro mkubwa katika jamii. Kwa hiyo, kama ulivyofanikisha ugawaji wa viwanja vile katika Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine, wacha na hili utalisemea kwa nguvu zote ili kuepusha migogoro ya wananchi na hususan kwa wakulima na hawa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tulikuwa ziarani Kagera na kwa kweli pale utakuta wengi wa wafugaji pale wametoka Uganda wametoka Rwanda. Sasa maeneo kama yale wananchi ni wapi ambao wataweza kuunganisha ardhi inayowagusa wananchi wa Tanzania na pale kuna idadi kubwa sana ya wahamiaji inayowagusa wananchi wa Tanzania na pale kuna idadi kubwa sana kutoka Rwanda. Kwa hiyo, maeneo kama hayo tusingalie ardhi iliyoko mijini kama Dar es Salaam au Wilaya nyingine. Lakini tuangalie Mkoa wa Kagera ulivyo, ni wapi wananchi watakuwa wanastahili na umilikaji wa ardhi, wakati pale kuna asilimia kubwa, wengi wa wahamiaji ni wahamiaji haramu na mifugo yao. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo nilitaka Mheshimiwa Waziri pia Serikali iliingalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limenifanya nisimame hapa, nchi yetu ya Tanzania imetoa uraia kwa wananchi wa mataifa mengine na baadhi ya Raia wale ambao wanatoka mataifa mengine wanakuwa na uraia wa nchi mbili na wakienda nchini kwao unatambulika zaidi uraia wa nchi yao kuliko nchi yetu sisi. Je, umilikaji wa ardhi kwa hawa ambao wapo Tanzania kwa muda mrefu utahesabika vipi na utafanyiwa kazi kiasi gani?

Kwa sababu mpaka leo ukienda katika nchi zao wanatambulika ni raia wa nchi zile. Je, watakuwa waaminifu kwa taifa letu? Au wanaweza kuona ni mradi, wakauza ardhi haraka wakapata fedha za kurudia kwao. Kwa hiyo, tuangalie wale Watanzania ambao tumewapa uraia na uraia wao sio wa kuzaliwa lakini walipewa uraia wa kazi.

Kwa hiyo, tuangalie je, wanamiliki ardhi kiasi gani. Je, hii Sheria wataitumia kiasi gani na hofu hii ipo, hata baadhi ya wawekezaji tunasikia taarifa kwamba baadhi ya yale maeneo ambayo walichukua

kuwekeza wameyauza kwa wengine, baada ya kupata faida, wakaondoka wamekwenda nje ya nchi. Kwa hiyo, masuala ya ardhi tuyaangalie sana vinginevyo tunaweza kuifuta ardhi kwenye muda mfupi sana na wananchi wetu wakawa manamba kama alivyosema Mheshimiwa Joel Bendera na Wabunge wengine wengi. *(Makofi)*

Hii inawezekana, huko nje watu wana fedha nyingi hawana cha kufanyia. Wanaweza kuuzia kwenye hizi *bureau* ambazo zinachenji fedha baadaye wananchi wakashindwa kulipa mikopo ile ya kununulia ardhi, Tanzania ikanunuliwa na watu 10 tu kutoka Marekani, kutoka Arabuni na maeneo mengine. Kwa hili suala Mheshimiwa Waziri ulisimamie kwa nguvu zote na kwa ufafanuzi uliokuwa sahihi.

Jambo lingine kubwa ni kuondoa hofu ile ya wananchi na moja ni kuanza kutolewa vibali watu kumiliki ardhi wengine. Kitu cha kwanza kabla ya kufanya kazi kwa Sheria hii. Serikali ichukue mikakati ya kutoa maeneo na kila mtu amilikishwe eneo lake kwa mujibu wa Waraka fulani ambao unatoka Serikalini kumhakikishia kwamba hii ardhi ya eneo hili hapa ni la Mheshimiwa fulani au hii ni ya mwananchi fulani. Ili asitokea mjanja mwingine akaitumia nafasi ile akasema hili eneo ni langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma gazeti sasa hivi hapa la leo la Nipashe. Kuna mpangaji mmoja amekaa katika nyumba kwa zaidi ya miaka 20 ameua nyumba na yeye ni mpangaji tu na hili ni tatizo litatokea kwa ardhi. Kuna watu watatoka Dar es Salaam, watakwenda kuuza ardhi Mbeya. Kwa hiyo, Serikali iwe mwangalifu sana kwa hili, vinginevyo wananchi watakosa imani na Serikali yao. Vinginevyo tutawapa nafasi wapinzani na nataka kuhakikisha kwamba kwenye kampeni wataitumia hii. *(Makofi)*

Wataambia Serikali yenu leo wanauza ardhi. Kwa hiyo, dhana kamili iwekwe katika elmu kabisa kwa kupewa wananchi juu ya dhana sahihi ya nini Serikali inakusudia juu ya Muswada huu. Vinginevyo tutawaweka wananchi wetu katika matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimalizia Muswada unasema ili haya yote yafanyike bila kuathiri taratibu zilizopo kwenye Sheria wakati huu mabadiliko yatafanyika kwenye taratibu za kuendesha mashauri ya dharura na pia kwenye kanuni zilizotayarishwa na Waziri kuhusu taratibu za uwekaji rehani wa nyumba au ardhi isiyohamishika.

Mheshimiwa Waziri, hiki kipengele kimenipa sababu nikuunge mkono sana. Lakini pia kinahitaji usimamizi, ukisimamia kwa dhati, kwa sababu umetuthibitishia kwamba haitakuwepo athari. Ikitokea athari umebeba mzigo nzito kwa Taifa hili kwa Watanzania wote na umechukua dhima kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu. *Population* ya Watanzania inaongezeka kila siku. Tusione leo, tuangalie miaka 40 inayokuja, siyo hii 40 ambayo tumeshafikia. Lakini tuangalie je hatima ya Taifa hili itakuwa wapi? Kuna watu wanachukua zaidi ya eka 60,000 na kwamba hapa Mswahili asipite itakuwa ni matatizo.

Kwa hiyo, dhana hii ningemwomba Mheshimiwa Waziri, ningemomba watendaji wa Wizara yake, watendaji wa Halmashauri waone kwamba athari haitokei kwa wananchi juu ya Muswada na Sheria hii vinginevyo na sisi mtatubebesha lawama kubwa kwa wananchi. Tutaondoka tutakuwa tumechukua jukumu kubwa, *population* ya wananchi inazidi na watakuja kukosa eneo la kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kagera, ni mfano hai kabisa, pale sasa Wanyarwanda, Waburundi, Waganda ndiyo walioshika nafasi kubwa sana. Mifugo yao pale ndiyo inayofanya kazi kwa eneo kubwa sana. Hatuamini kama wananchi wa kawaida watakuwa na haki kupatia mikopo kwa ardhi ya kule na tunaamini kwamba kuna maeneo mengine ya Tanzania yako sawa sawa na ilivyo Kagera. Tumekwenda Ngara, tumetembelea Bukoba na maeneo mengine. Kwa hiyo, sheria hii na Kanuni hizi na haya maamuzi ambayo yatafanywa na hizi Mahakama zetu, wajitahidi kuwafanyia haki wananchi hasa wale wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Magereza tunayotembelea, wengine wako ndani mahabusu kwa migogoro ya ardhi. Sasa hivi maadam kuna fedha hizi, watu wengi hata vijana watazidi kwenda mahabusu, wakati Serikali ina mikakati ya kupunguza mahabusu na wafungwa. Lakini sheria hii inaweza ikasababisha

vijana wengi na baadhi ya wananchi kwenda ndani na magereza kufurika kwa sababu kuna fedha, watu watagombania ardhi.

Kwa hiyo, watendaji wa vijiji vya Halmashauri wawatendee haki wananchi wanyonge waliokuwa katika maeneo yao hasa kwa kusimamia wasiwatafute wenye nguvu wakawapa haki na wakawanyima haki yao wale wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nautakia mafanikio Muswada huu, nimitakie Waziri kazi nzuri na kweli ni suala zito, tuwatake wananchi wetu watuelewe nini malengo na wasikimbilie kwenye mikopo kama hakuna lazima ya kukopa. Serikali isimamie kuwasaidia wakulima wetu wadogo wadogo ili waepukane na migogoro hii ambayo inaweza kutokea hapo baadaye.

Baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu na ningependa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Watendaji wake na bila kumsahau Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji wake kwa kazi nzuri waliyofanya, kurekebisha vipengele vingine vya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ambayo mimi ninaona kama imezidi kupanua wigo wa haki ya mwanamke na familia yake kwa sasa hivi katika miliki ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu wanawake wengi hasa wale ambao wako kwenye sehemu za miji na wako kwenye sehemu ambazo ziko pembezoni mwa miji mikubwa, waume zao kwa sababu ya utamaduni ambao umetoa mfumo dume katika miliki ya ardhi walikuwa wanatoa hati za nyumba, wanapeleka rehani katika mabenki na bahati mbaya mabenki yetu yalikuwa hayaulizi kama kuna mwanamke kwenye ile familia ambaye pia ana haki ya kuhakikisha kwamba kuna mkopo unaochukuliwa ambao utakuwa ni faida kwa familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake kuna kesi nyingi sasa hivi za akinamama Mahakamani ambazo wamekwenda kupinga kuuzwa kwa nyumba zao na mabenki yetu kwa sababu waume zao walikwenda kisirisiri wakachukua mikopo na wengine ile mikopo wamechukua wakahama miji, wakaenda kwingine wakaoa watoto wadogo wadogo wakala zile pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi naona sasa hii Sheria imefika mahali pake. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali yetu iangalie mfumo ambao utatumika ili wadau wote ambao ni Watanzania waume na wanawake pamoja na watoto wajue haki yao ambayo wamepewa na Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba kwamba katika Bajeti inayokuja Wizara hii itenge pesa nyingi sana ya kutengeneza vipindi vya Redio kupitia Redio zote nchi ni *Community Radios*, Redio Tanzania na Redio nyingine ili kuweza kutoa vipindi wakati muafaka na iwe ni wakati wa saa za jioni ambao pia na akina mama tunaweza tukasikiliza hivyo vipindi ili tuelewe haki zetu katika Sheria hii, bila hivyo hii Sheria nzuri sana tutaipitisha itakwenda kwenye ma-*shelf* na bado tutaendelea kunyanyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nieleze kitu kimoja mimi hapa nina wasiwasi. Wasiwasi wangu ni kwamba tunasema kwamba ardhi itatumika kama dhamana ya kuweza kutupa sisi mikopo. Sasa nikaanza kujiuliza mimi ninayetoka Morogoro, wale wenzangu wanaoishi kule Bunduki kule milimani juu, wenzangu wanaoishi Tunonguo, wana vishamba vidogo vidogo. Sasa vile vishamba sijui watavitumiaje ili waweze wakapa mikopo. Uwezo wa kuweza kulipa gharama za kufanyia evaluation au kufanyia *survey* ili waweze wakapata hati miliki unakuwa haupo. Matokeo yake ni kwamba hawa wataona kwamba wenzao wa mijini wananufaika. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba watauza vile vishamba vyao na tutaanza kuona sasa kunaanza kujitokeza kwa *squater* nyingi sana katika miji yetu.

Mimi naanza kuona hilo na natabiri hilo kwamba wengi watauza mashamba yao, atamwambia mke wake twende. Watakwenda watatafuta popote tu kujenga kule karibu na mji, watajenga kijumba kidogo kidogo, ikifika mahali kama zile hela zinakwisha mwanamme anamtoroka mama anamwacha na watoto na matokeo yake ni kwamba watoto wengi wataingia mitaani. Kwa hiyo, tuangalie pia hii sheria kwa wale ambao wako kwenye *remote places* kama hizo ambazo ninazisema sasa hivi. Hii Sheria itawanufaisha namna gani. Hilo sijui kama tumeliangalia vizuri.

Lingine ninalopenda kuzungumzia hapa ni wale wafugaji. Wafugaji wapo na wanayo haki ya kuzunguka na wanyama wao kutafuta malisho na maji. Itafika mahali kila Mtanzania ataamua kuanza kukamata eneo lake anaanza kuzungushia wigo, ng'ombe akipita pale aanze kukamatwa. Sasa hawa wenzetu sijui itakuwaje.

Mimi naomba Wizara hizi mbili zinazohusika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo iangalie namna ambayo wanaweza wakasaidiwa hawa wenzetu, kwa sababu nao wanasaidia kipato kikubwa sana katika pato la nchi. Waweze nao sasa wakapewa maeneo, wakasaidiwa kuwa na *mini ranches* na *ranch* zikaweza kuwekewa yale mahitaji muhimu kama malambo, shule pamoja na kwamba haya maeneo basi tusiwasukume kule ambako ni maeneo ambayo hatuwezi tukalima kwa sababu kama eneo haliwezi likawa ni eneo la kilimo hata majani ya malisho ya ng'ombe hayatakuwepo.

Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba watakaa pale baada ya muda itabidi waondoke na migogoro itaanza kuzuka kati ya wakulima na wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba katika historia ya nchi hii na Sheria tulizonazo, mimi kama mwanamke naona kuna sheria mbili muhimu sana. Sheria hii ambayo tunaizungumzia hapa pamoja na Sheria ya Ndoa.

Sasa mimi naona kwamba ili uweze kupata kueneza ule wigo wa uelewa hii Sheria itakuwaje kama tunaweza tukatengeneza mihutasari ya hizi Sheria ikaingia katika *curriculum* za shule kwenye somo la uraia. Kwa sababu wale ndiyo raia na ndiyo wananchi wa kesho waweze kukua wakijua thamani yetu, ya ardhi. Waweze kujua wajibu wao katika ndoa ni nini.

Kwa sababu akinamama wengi, wasichana wengi, wanaolewa wamemaliza *form four* wengine *form six* hata wengine ni *graduates*, wanafika kwenye vituo vyetu vya Sheria wakiomba msaada. Lakini unapomwelimisha anashtuka anasema kwamba kama sheria ilikuwepo kama hii mbona sijui? Sasa hiyo ndiyo tunasema kwamba tumekuwa na mazoea ya kuwa na Sheria nzuri sana nchi hii lakini tunaziweka kwenye ma-*shelf* hatuhakikishi kwamba zinawafikia wale walengwa.

Napenda nishauri pia hizi sheria vile vijarida vyake, viwekwe katika library zote za Mikoa, *library* zote za Shule za Sekondari na *library* za Vyuo vyote vya *High Education* kwenye *Universities* ili wanafunzi wetu na watoto wetu waweze wakasoma, wakue wakijua sio kwamba waje wakashtukie tu kwamba kulikuwa na Sheria, kumbe ni sheria ambayo angeweza akajifunza kwa wakati muafaka ambako alikuwa na *time* ya kusoma na kuuliza maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahia hii Sheria. Lakini naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, kuna akinamama mpaka sasa hivi ambao hawana mashamba, mashamba yao yameuzwa. Kesi zao ziko Mahakamani, wengine wanalalamika kwa viongozi wa Vijiji, kwa ma-DC. Sasa sheria hii itawasaidiaje kuweza ku-*recover the lost property* kwa sababu hawana pa kwenda. Nafikiri huko waliko kama wanasikiliza sasa hivi wanakuwa na matumaini kwamba kuna kitakachofanyika.

Mimi naomba Serikali iangalie kwamba wale akinamama ambao wamepoteza haki zao basi waweze kurudishiwa haki zao kwa sababu kwa nini wamange mange mijini, wamangemange vijijini wakiomba pa kulala na watoto wao kwa sababu mtu mmoja tu ambaye anaamini kwamba ndiye mwenye haki ya kutoa maamuzi ameuza shamba au ameuza nyumba akawaacha kwenye mataa. Mimi hilo ndiyo rai yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, linakuja suala lingine kwenye ndoa za mitala. Hata tukisema kwamba hata wale ambao kuna imani yao ya dini uwapende wanawake wote ni uongo. Unapokuwa na wanawake wanne au zaidi ya mmoja, ni lazima yule mwanamke mdogo anapendwa kuliko mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, itafika mahali yule mama mtu mzima akawekwa pembeni yule mwingine mdogo akaenda na mume wake kule benki akaenda kutia sahihi kwamba waweke rehani shamba lao au nyumba yao. Kwa sababu hata mambo yakija kuharibika yeye bado ni mtoto mdogo anaweza akaondoka akapata ndoa kwingine. Lakini wale wengine wanapoteza. Hili linaonekana kama mchezo lakini haya mambo yapo na sasa hivi hata hapa Dodoma kuna mama aliyekuja kuomba msaada kwangu nimwelekeze aende wapi kwa sababu mume wake amechukua hati zote za nyumba hapa Dodoma akaziweka rehani akachakua mkopo, akahamia Dar es Salaam akajenga nyumba nzuri, akaoa wanawake wadogo wawili akaishi nao kule. (Makofi)

Yule mama amekuja kushtukia nyumba inapigwa bei, inapigwa mnada na ilikuwa bahati nzuri tu aliponiona nikamwambia sasa wewe unajua nenda ukatafute *advocate*, kwenda Mahakamani kaweke na wewe *Court injunction*. Nikamwelimisha nikampa na kitabu akasoma. Sasa hivi anaendesha hiyo kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo mnaona kwamba ni hadithi lakini ni kweli yapo. Napenda niulize *definition* ya *undeveloped land*. Tunasema kwamba ardhi ambayo inakuwa haijaendelezwa kwa muda wa kipindi fulani, mwenye ile ardhi atanyang'anywa. Lakini tunapozungumzia *development* kuna *development* ya kujenga nyumba, kuna *development* ya kulima mazao ya kudumu na mazao ya muda mfupi. Kuna wengine wanalima mahindi inafika baada ya miaka miwili, mitatu, wanaamua kupumzika wasilime kwa miaka miwili kwa ajili ya kurudisha rutuba. Sasa huyu ataitwa naye ni mzembe?

Sasa katika hii *definition* kwa sababu vijijini hawataelewa *definition* ya *development* ninaomba hiyo *definition* iweze ikawekwa *clear* kwamba uendelezaji wa ardhi maana yake ni nini, mijini, vijijini na kwenye *remote places* na kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa tu kusema kwamba naomba nisisitize tena lile la elimu. Elimu sisi Wabunge tutoe, elimu itolewe mashuleni, hata tupitie pia kwa madhehebu ya dini, Masheikh, Mapadri, waelimishwe, hawa si ndiyo wanaofungisha ndoa, wanaweza wakatoa hii elimu.

Naomba hata kama vyama vya siasa, Chama Cha CCM kinajitahidi, hata vyama vingine wajitahidi pia kutoa elimu kwa wananchi wao kwa sababu wanapokuja kupatikana na tatizo la kwamba wamekwenda kinyume na sheria wasije wakafikiria kwamba wananyanyaswa na Serikali ya CCM, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba sheria hii ni nzuri inatetea hadhi ya mwanamke kama tunapata elimu, inatetea haki za watoto kama tutapata elimu na ninaomba hiyo elimu itiliwe mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. (Makofi)

**MHE. ABDILLAH O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Nianze na kuunga mkono hoja hii hasa katika kile kipengele kinachosema kwamba ardhi itaendelea kuwa mali ya umma na kwamba atakayepewa ardhi kama hataiendeleza basi anaweza akanyang'anywa.

Pia naomba sheria hii mara tu ikipitishwa na Rais basi Mheshimiwa Waziri aje aanze kutekeleza kipengele hiki kwenye shamba la Mkonge la Kabisela. Maana shamba lile limetelekezwa sasa ni pori mashahidi wajumbe wa Kamati ya Mazingira wameona jinsi lile pori lilivyokuwa nene na mamia ya heka hayafanyi kazi na Watanzania pale wanataka lile shamba walime mangolomwa ni aina fulani ya mtama, wananchi wanataka lile shamba walime mtama ni pori kama wameshindwa kulima katani. Kwa hiyo, sheria hii ikipitishwa Waziri aje aanze kutekeleza kipengele hiki kule Mtwara kwa Kabisela kuchukua lile shamba kuwapa wananchi. (Makofi)

Lakini la pili ni swali kwamba sheria hii inasemaje juu ya barabara iliyopo pale kwa miaka 20-30 ambapo sehemu ile akaja kuchukua mtu kama kununua akaamua kufunga ile barabara kiholela, hii sheria inasemaje? Kama alivyofanya mwekezaji wa shamba la Kabisela amefunga barabara zote kiasi ambacho mtu akitaka kwenda kilometa tano basi itabidi utumie kilometa 60 kuzunguka mpaka kufika, kumbe unapokwenda ni kilometa tano tu. Sheria inasemaje kuhusu barabara iliyokuwepo pale kwa miaka 30-40 mtu amenunua anafunga kienyeji?

La mwisho, naiomba Serikali isiwe kama wauza nyanya maana muuza nyanya, nyanya nzuri hupeleka sokoni kuuza zilizovunjikavunjika au mbaya mbaya zile hupeleka nyumbani akala. Sasa na sheria hii isiunge mkono habari hizi za kwamba ardhi nzuri na zenye rutuba wakauziwa wawekezaji kutoka nje sisi Watanzania tukapewa sehemu yenye *chidwadwa*. Kwa Wamakonde sehemu yenye *chidwadwa* ni sehemu ambayo hata ukitia mbolea mahindi hayastawi. Naiomba Serikali katika mpango huu isiwe kama wauza nyanya. Naunga mkono Muswada huu, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilisema huyo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho nilikuwa nimempa dakika 15 lakini ametumia kama dakika nne, tano.

Kabla sijaahirisha Bunge, nina maelezo yafuatayo. Waheshimiwa Wabunge Muswada huu wa Ardhi kama unavyojadiliwa tuliletewa Bunge lililopita lakini baada ya mashauriano ndani ya Serikali, Kamati na wadau mbalimbali Serikali iliona marekebisho yalikuwa mengi kwa hiyo wakachapa Muswada huu hapa ambao nadhani wote mmeupata, *Bill Supplement No.1* ya tarehe 9 Januari, 2004. Kwa hiyo, huu ndio ambao mnaombwa muendeleo kuujadili lakini pia ndio utakaopitishwa kama ni kupitishwa kesho, tutakwenda kifungu kwa kifungu kwa hii *Bill Supplement No.1*.

Sasa baada ya maelezo hayo, niseme tu wachangiaji waliobaki ni wengi nadhani tutaendelea kesho, wale ambao hawakupata nafasi nina hakika kesho wanaweza kupata nafasi.

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.34 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 10 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi*)





